Ijumaa Mei 10, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0579914

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




UKURASA 13

## MDUDE KARUDI

CHAMA Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimesimulia namna bodaboda walivyomuokota kada wake, Mdude Nyagali...

UKURASA 5





## MAPAMBANO

ASKARI Polisi na wa Magereza, wamepigana makonde hadharani katika eneo la stendi kuu ya mabasi barabara kuu...

UKURASA 4

# TUTAKUENZI

UKURASA 2,3,7,8,24



**ABDIEL:** "Baba alikuwa mzalendo kwa nchi yake, mwenye uthubutu, mtu aliyependa kuvunja mipaka, alikuwa na mipaka ya fikra, uelewa na ya mazoea."

**ASKOFU SHOO:** "Alikuwa mtu aliyethamini sana maridhiano ya Watanzania wote, licha ya tofauti za matajiri, maskini, wenye mamlaka na wasio na mamlaka, hakuwa na kiburi".

**MBOWE:** "Marehemu hakuwa kiongozi wa serikali wala kiongozi wa siasa, lakini alikuwa na unyenyekevu wa kipekee, utajiri wake haukumtia kiburi bali ulimwongezea unyeyekevu".

**SPIKA NDUGAI:** "Mzee Mengi ulikuwa na upendo, baba wa yatima, wajane, watu wasiojiweza na wagonjwa, alikuwa msaada mkubwa kwa watu, serikali pamoja na Bunge".

**MEMBE:** "Mengi alipenda na alitaka kuiona Tanzania ikiwa nchi ya amani, utulivu, inayoheshimu sheria, katiba na uongozi bora".

**MAJALIWA:** "Mzee Mengi ni mmoja wa watu wazalendo kabisa kutokea katika historia ya nchi yetu.

**DK. BASHIRU:** "Naomba nitumie fursa hii kumuombea msamaha kijana wangu Makonda, mimi"

Mwili wa aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, ukishushwa kaburini na kifaa maalum wakati wa mazishi yake jana jioni, kijijini kwake Kisereni, Kata ya Machame, Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA MAJARIBUNI** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6



HUZUNI 1942 - 2019



# FAMILIA: Tutakuenzi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MTOTO wa kiume wa aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Regnald Mengi, Abdiel Mengi, amesema baba yake kabla ya kufariki dunia aliwaachia mambo mengi kama familia ambayo amewaonyesha, amewafundisha na amewapa dira.

Akisoma historia na wasifu wa marehemu baba yake, Abdiel Mengi alisema: “Sisi kama familia tuna mambo mengi ambayo ametuonyesha, ametufundisha, ametupa dira ambayo hatuna lingine zaidi ya kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa yale ambayo alitufanyia.”

Alisema ukweli haufichiki, hasa kutokana na ukarimu na wema wa watu wote kuchangia katika wasifu wa baba yao Dk. Regnald Abraham Mengi umewapa changamto katika kuandika wasifu wa baba yao.

Alisema baba yao amefanya mambo mengi sana na siyo rahisi kuyazungumzia yote kwa wakati mmoja, lakini baada ya kutafakari hayo wameona mwishowe wachukue nafasi hiyo kuzungumzia sifa zake za msingi tatu.

“Sifa yake ya kwanza ni uzalendo, baba yetu Regnald Abraham Mengi alikuwa mzalendo kwa nchi yake, kwa Afrika, kwa ubinadamu, vile vile kwa mapenzi ya Mwenyenzi Mungu,hali iliyomfanya awe mtu wa kujitoa zaidi kuliko kuchota.

“Sifa ya pili alikuwa ni mtu mwenye uthubutu. Katika kuishi na baba yangu mara nyingi nilipata kushuhudia tukio ambalo baba yangu anakuwa anaanzisha jambo na kulitangaza hasa, wakati mwingine hata kabla hajafahamu zaidi undani wa hilo jambo.

Zaidi alieleza: “Kuna msemo unasema, unaenda na jambo utalifahamu mbele kwa mbele, baba aikuwa na sifa hiyo, kabla ya yote alikuwa anajiuliza kwa nini nifanye au kwa nini? Baba alifanya mambo mengi kama uwezeshwaji wa wazawa, walemavu, uhifadhi wa mazingira na aligusia amani ya nchi na mambo mengi muhimu na mengi kati yake mpaka leo hii utatuzi wake unafanyiwa kazi.”

Aidha, Abdiel Mengi ameitaja sifa ya tatu ya baba yake alikuwa mtu anayependa ku-break through (alikuwa ni mtu aliyependa kuvunja mipaka).

Alisema marehemu baba yake alikuwa na mipaka ya fikra, mipaka ya uelewa, mipaka ya mazoea na mengine mengi, akitoa mfano dunia ilipomwambia, “mzee wetu wewe ni mtoto wa masikini, umezaliwa masikini, utaishi katika hali ya umasikini na vile vile utakufa katika hali ya umasikini. Mzee wetu alivunja mpaka huo,”

Alisema hata Dunia ilipomweleza kwa sababu yeye ni mzawa, hataweza kufanikisha shughuli fulani fulani, mzee wao pia alivuka mpaka huo hata pale dunia iliposema bepari hawezi kuwa rafiki wa masikini.’

Kutokana na maono ya marehemu baba yake, Abdiel Mengi amesema amejaribu kuyaweka yote hayo na hizo sifa tatu na akizitohoa labda kwenye tungo moja, anaweza akasema mzee wao alikuwa mzalendo aliyethubutu kuvunja mipaka.

Alisema watayaishi aliyokuwa akiyafanya baba yao.



Abdiel Mengi

## Mbowe akemea kauli za ubaguzi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KIONGOZI wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe, jana aligeuka mbogo dhidi ya viongozi aliodai wana matendo na kauli za kibaguzi zinazobagua watu akisema suala hilo sio jambo jema.

Mbowe aliyasema hayo wakati alipopewa nafasi ya kutoa salaam zake katika ibada ya mazishi ya aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Regnald Mengi iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

“Tuna nchi moja tunayostahili kupendana, kuheshimiana na tunastahili kuona kila mmoja ni sehemu halali ya nchi yetu. Wote kwa pamoja tunapaswa kuungana kukemea kauli za kubaguana, tusianze kubaguana kwa itikadi, dini au makabila yetu, tupendane na tutambuane kama Watanzania.

INAENDELEA UK.7



Freeman Mbowe

## Membe asifu mchango wake sekta binafsi

**Na Salome Kitomari**

ALIYEKUWA Waziri wa Mambo ya Nje, Benard Membe, amesema Dk. Reginald Mengi, atakumbukwa kwa kuamini kuwa maendeleo ya kweli Tanzania na duaniani hayatoki serikalini bali sekta binafsi ambayo ndiyo gurudumu la maendeleo.

Akizungumza jana wakati muda mfupi kabla ya ibada ya kuaga mwili wa Dk. Mengi katika Usharika wa Moshi mjini, alisema siku zote Mengi alisema kazi ya serikali ni kutengeneza miundombinu ya kuwezesha sekta binafsi kusuguma guruduma la maendeleo mbele.

“Hakuna nchi duniani ambayo inaleta maendeleo bila kuikumbatia sekta binafsi, wafanyabiashara binafsi, wawekezaji, wamachinga, watu binafsi na makampuni. Hayo ndiyo yanaleta maendeleo ya kweli,” alisema.

Alisema Mengi aliujua uchumi kwa kuwa alijua nafasi ya sekta binafsi na serikali na kwamba walikuwa marafiki kutokana na uelewa huo, na kwamba hadi sasa anaamini ndilo litaisaidia nchi.



Bernard Membe

“Mengi kila mara kwenye mkutano na ukikaa naye binafsi alisema kiongozi mzuri ni yule ambaye anakubali hajui, ukiwa na kiongozi anayekubali kwamba sijui atakuwa na sifa mbili kubwa, moja atapenda kujifunza ili ajue, pili atasikiliza vilio vya watu ili avitatue. Ukijifanya kujua kila kitu, Mzee Mengi anakwamba wewe siyo kiongozi bora,” alisema alipoulizwa funzo alililipata.

Kwa mujibu wa Membe, “Mengi alisema kuwa tajiri ni mtihani unaopewa na Mungu, kwa kuwa angaweza kutoa msaada au utajiri kwa yeyeote lakini huchagua ampe nani ampe akigundua ana mkono mrefu, na kwamba ukiwa na mkono mfupi Mungu hakupi utajiri.”

“Mafunzo haya Mengi hakuficha kwa rafiki zake, ndugu zake, familia yake, vyama vyote, aliamini mtihani aliyopewa ni kutoa alichonacho kwasababu kwa kumuhofia Mungu alikuwa anasema nikienda huko nikauliziwa nilitumiaje utajiri wangu, nilitaka nijibu kwa Mungu niliutumia kama ulivyotaka,” alisisitiza.

INAENDELEA UK. 7

## Bashiru amwombea msamaha Makonda

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KATIBU Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amemwombea msamaha wa ‘toba’ Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam Paul Makonda kutokana na kauli yake aliyoitoa wakati wa kuaga mwili wa aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi katika viwanja vya Karimjee.

Dk. Bashiru alimuombea msamaha Makonda wakati alipopewa nafasi ya kutoa salaam zake katika ibada ya mazishi ya Dk. Mengi iliyofanyika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini wa KKKT.

“Naomba nitumie fursa hii kumuombea msamaha kijana wangu Makonda, mimi namfahamu lakini hii ni mara yangu ya pili nimemsema hadharani. Lakini mara ya kwanza nilimsema Simiyu, akaja akalia ofisini, nikasema ubadilike na kwa kweli ameanza kubadilika. Bado ni kijana mzuri, shupavu lakini tunahitaji kuwasadia vijana wetu,”alisema Katibu Mkuu wa CCM.

Akimzungumzia marehemu Dk. Mengi, Dk. Bashiru alisema alikuwa na mchango mkubwa katika kulijenga taifa ambapo katika

INAENDELEA UK.7



Dk. Bashiru All



# Majaliwa aongoza mazishi



Kassim Majaliwa

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, jana aliongoza maelfu ya watu waliojitokeza kwenye ibada na baadaye mazishi ya Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, yaliyofanyika kijiji cha Kisereny, Machame, Moshi mkoani Kilimanjaro.

Dk. Mengi alizikwa kifalme kijijini kwao majira ya saa 11:19 jjoni baada ya ibada ya mazishi kufanyika mjini Moshi, Kanisa Kuu la Kiinjili la Kilutheli (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini na kuhudhuriwa na maelfu ya waombolezaji waliokuwa wamejaa ndani na nje ya kanisa hilo.

Nipashe ilishuhudia idadi kubwa ya wakazi wa Moshi wakiwa wametanda katika barabara ya kanisa hilo na ile ya stendi ya mabasi Moshi, wakisikiliza mahubiri ya ibada ya Dk. Mengi.

**KUWASILI**

Mwili uliwasili kanisani majira ya saa 2: 08 asubuhi kwa msafara ukitokea nyumbani kwake Machame ulikolala tangu juzi ulipowasili kutoka Dar es Salaam.

Baada ya kufika kanisani ambako wakati huo kulikuwa na umati wa watu uliofika tangu saa 12:00 asubuhi, mwili huo ulishushwa na kuingizwa ndani ya kanisa.

Kabla ya ibada kuanza, wananchi walipata fursa ya kumuaga Dk. Mengi ambapo vilio vilitawala na wengine walipita kwenye jeneza lake wakiwa na mabango ya kumsifu likiwemo moja lililoandikwa jina la kitabu chake cha I Can, I Must, I Will ambapo ndani yake lilichorwa picha ya gari.

Wakati wa kuaga kundi la watu wenye ulemavu lilipofika mbele ya jeneza la Dk. Mengi lilishindwa kuzuia hisia zao na kuangua vilio huku wengine wakiishiwa nguvu na kubebwa.

Enzi ya uhai wake, Dk. Mengi aliwadhamini na kuwasaidia watu wenye ulemavu na alianzisha taasisi ya Dk. Mengi Foundation Disability na mwaka huu alitoa tuzo za I Can, tuzo zilihudhuriwa na Makamo wa Rais Samia Suluhu.

Shughuli ya kuaga mwili wa Dk. Mengi katika Kanisa la KKKT Moshi ilianza saa 2:25 asubuhi hadi saa 7:00 mchana ibada ya mazishi kanisani hapo ilipoanza na kumalizika saa tisa alasiri.

Umati wa watu uliojitokeza kanisani hapo ulisababisha ilipofika saa 4:35 asubuhi ratiba ya kuaga iende sambamba na utoaji wa salamu za rambirambi kutoka makundi kutoka taasisi mbalimbali ili kwenda na muda uliopangwa.

Baada ya kufika muda huo wakati waombolezaji waliokuwa nje ya kanisa wakiendelea kuaga, kiongozi wa shughuli hiyo ilibidi atangaze kusitisha kwa muda hadi baadaye ili waliopo ndani nao wapate nafasi hiyo sambamba na utoaji wa salamu za rambirambi na ndipo kundi hilo liliendelea.

**MOSHI YASIMAMA**

Shughuli mbalimbali yakiwemo maduka ya wafanyabiashara yanayozunguka stendi kuu ya mabasi Moshi karibu na kanisa hilo yalifungwa kwa muda na wahusika kuungana na Watanzania wengine kumuaga Dk. Mengi.

Licha ya manyunyu ya mvua kuanza lakini idadi kubwa ya waombolezaji waliokuwa nje, waliendelea kukaa ili kushiriki ibada ya mazishi.

Ndani ya kanisa hilo walikaa familia, ndugu na viongozi mbalimbali wa serikali na wafanyakazi wa IPP huku ndani ya uzio kanisani hapo kukiwa na mahema na nje ya kanisa kukiwa na kundi kubwa la watu likiwa limesimama.



Paul Makonda

Baada ya waombolezaji kumaliza kuaga ilipofika saa 6:06 mchana mke wa Dk. Mengi, Jacqueline Mengi na watoto waliongozwa na mdogo wa marehemu, Benjamin Mengi kuaga mwili huo.

**VIONGOZI WALIOHUDHURIA**

Baadhi ya viongozi waliohudhuria ni pamoja na Spika wa Bunge, Job Ndugai, Spika wa Bunge la Afrika Mashariki, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Bashiru Ally, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, Waziri wa Ardhi, William Lukuvi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, Mbunge wa Muleba, Anna Tibaijuka, Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye, Waziri wa zamani wizara ya Mambo ya nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Bernald Membe, Waziri Mkuu Mstaafu, Frederick Sumaye na wakuu wa mikoa, wilaya mbalimbali.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliwasili kanisani hapo saa 6:24 mchana akiambatana na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira na ndio ibada ya kumuombea Dk. Mengi ilianza kabla ya kwenda kuzikwa Machame.

Wakati mwili wa Dk. Mengi ukipelekwa Machame kwa mazishi, wananchi kutoka vijiji vya huko walikuwa wamesimama pande mbili za barabara wakiusubiri.

**KUFARIKI**

Dk. Mengi alifariki dunia usiku wa kuamkia Alhamis iliyopita nchini Dubai, Falme za Kiarabu na kurejeshwa Tanzania Jumatatu ya wiki hii na siku iliyofuata wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam walipata nafasi ya kumuaga wakiongozwa na Rais John Magufuli na Jumatano alisafirishwa kwenda nyumbani kwake Machame kisha jana kabla ya mazishi, ibada ya mazishi ilifanyika Moshi na baadaye kurudishwa machame kwa mazishi.



Askofu Dk. Fredrick Shoo

## Spika akemea vikali matumizi mitandao

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai amelaani vikali baadhi ya watu katika mitandao ya kijamii kumuandika vibaya marehemu Dk. Regnald Mengi akisema hata wao ndivyo hivyo wanavyofanyiwa katika mitandao hiyo, huku akiwataka Watanzania kutoamini kile wanachokisoma katika mitandao.

Ndugai ameonya kuwa ni vizuri kwa watu pamoja na wapakwa mafuta wa bwana, wanapopata mashaka kwa vile ambavyo wanavisoma katika mitandao hiyo, wawaulize ili waweze kupata ukweli halisi, kwa kuwa nao wanania njema.

"Sisi sote ni wenzenu na ni miongoni mwenu na Watanzania wenzenu, sasa tunageukaje kuwa watu wa ajabu tena haiwezekani. Kwa niaba ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatoa salaam za kumuaga na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa maisha yake yaliyogusa watu wengi ndani

INAENDELEA UK.7



## Askofu Shoo: Mengi alithamini maridhiano

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, amesema marehemu Dk. Mengi alikuwa mtu aliyethamini sana maridhiano ya Watanzania wote, licha ya tofauti za matajiri, maskini, wenye mamlaka na wasio na mamlaka.

Katika mahubiri yake jana, wakati akiongoza ibada ya mazishi ya Dk. Mengi, Askofu Shoo alisema maisha ya mwanadamu yana ukomo wake hapa duniani na tukitambua hilo tunapaswa kuishi kwa unyenyekevu mkubwa, kuacha kujivuna na kiburi.

Alisema Mungu alimjalia hekima marehemu Dk. Mengi kwa kuwa hakuwa na kiburi na alipenda watu wote na kuwa na moyo wa kuwasaidia bila kujali dini wala itikadi zao au kwa misingi ya kikabila

"Na kama kuna kitu ambacho tunaweza kuiga na kukienzi ni hii roho yake ya upendo na kutokuwabagua watu. Kama kuna dhambi ambayo Watanzania tunapaswa kutubu ni dhambi ya kubaguana ili taifa letu lipokee baraka kutoka kwa Mungu. Dhambi nyingine inayotakiwa kutubu kama taifa ni ile ya wenye nafasi kuwakanyaga walio wadogo," alisema Askofu Shoo

Aliwataka Watanzania kuachana na dhambi hizo na kuwahimiza zaidi kujifunza kutoka kwa marehemu Dk. Mengi, kwani alikuwa na fedha za kununua haki, lakini hakuwahi kufanya hivyo.

Aliongeza kuwa Dk. Mengi siku zote alikuwa akisema utajiri alionao ni Mungu alimpa kwa ajili ya kuwafikishia watu wengine ambapo ni moyo wa ajabu sana na hakuwahi kuwa mbinafsi.

Dk. Shoo alisema Watanzania tumekuwa mabingwa wa kupotosha ukweli na pindi tunapojua ukweli hatutaki kuusimamia ukweli na kuwataka kubadilika na kusema na kusimamia ukweli.

Askofu Dk. Shoo ambaye pia ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT, alieleza masikitiko yake kuhusu viongozi wenye umri mdogo akiwaelezea kwamba wamekuwa wakijitutumua kama chatu.

"Ipo siku bwana atawashusha na kuwataka kubadilika na kuwa na unyenyekevu, msitumie nafasi zenu kuwanyanyasa watu wengine, nimekuwa nikifanya maombi kila siku ili waweze kubadilika,"ameeleza Askofu huyo

# Polisi na Magereza wapigana kavukavu

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

POLISI na askari wa Jeshi la Magereza wilayani Masasi Mkoani Mtwara, wamepigana makonde hadharani katika eneo la stendi kuu ya mabasi barabara kuu iendayo Tunduru.

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Blasius Chatanda, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 6 mchana baada ya askari polisi kumkamata askari Magereza ambaye inadaiwa alikuwa anaendesha pikipiki bila ya kuvaa kofia ngumu.

Hata hivyo, Kamanda Chatanda hakutaja majina ya askari huyo na polisi.

Chatanda alisema baada ya kutokea kwa ugomvi huo, Polisi walifyatua risasi hewani na kurusha mabomu ya machozi hali ambayo ilisababisha taharuki kubwa kwa wananchi wilayani humo.

Alisema muda kidogo walitokea askari Magereza watano ambao walifika eneo la tukio kwa ajili ya kumuokoa mwenzao, ndipo polisi na askari wa Magereza walipoanza kupigana.

Kamanda Chatanda alisema polisi huyo alikuwa doria katika operesheni ya kawaida ya ukamataji wa vyombo vya moto hasa pikipiki maarufu kama bodaboda, ambao wamekuwa wakiendesha bila ya kufuata sheria za usalama barabarani.

Alisema baada ya Polisi huyo kumshika askari magereza ambaye alikuwa kiendesha pikipiki bila ya kuvaa kofia ngumu na kumtaka kwenda kituo cha polisi au kuiacha pikipiki yake, alipinga ndipo mzozo ulipoanza.

"Baada ya muda kidogo kundi la askari magereza walifika kumuokoa mwenzao mara baada ya kumuona ameshikwa na Polisi, pia kundi la askari polisi walifika nao kumuokoa mwenzao, ndipo makundi hayo mawili ya jeshi walipoanza kuchapana makonde na kufyatua risasi hewani," alisema Kamanda Chatanda.

Kamanda Chatanda alisema kufuatia tukio hilo, Jeshi la polisi linaendelea na uchunguzi wa kujua chanzo zaidi ya vurugu hizo ikiwamo kufanya vikao vya dharura kati ya Jeshi la Polisi na Magereza, na kwamba uchunguzi utakapokamilika sheria itachukua mkondo wake.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti walieleza kuwa waliwaona polisi waliokuwa wamebeba silaha wakimvamia askari magereza ambaye alikuwa amevaa nguo za kiraia akiendesha pikipiki, na kumtaka kuelekea kituoni.

## Serikali yaahirisha ujenzi barabara Dar-Chalinze

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imeahirisha ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam hadi Chalinze yenye urefu wa kilometa 144 kwa kiwango cha 'expressway' hadi miradi mingine inayoendelea itakapokuwa imekamilika.

Akiwasilisha bungeni jana hotuba ya makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alisema mradi huo pia unahusisha ukarabati kwa kiwango cha lami sehemu ya Mlandizi - Chalinze unaofanyika kwa awamu na hadi Machi mwaka huu, mkataba kwa ajili ya ukarabati wa kilometa 12.4 ulikuwa umetiwa saini na maandalizi yanaendelea.

Alisema barabara ya Kwa Mathias-Msangani

INAENDELEA UK.5


**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**(IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA)**

**AT ARUSHA**

**CIVIL CASE NO. 16 OF 2017**

**TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED.................................................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**PROMOTION OF RURAL INITIATIVES AND DEVELOPMENT ENTERPRISES LIMITED ...........................................................DEFENDANT**

**NOTICE OF MENTION**

TO: PROMOTION OF RURAL INITIATIVES AND
DEVELOPMENT ENTERPRISES LIMITED
P.O BOX 13900
ARUSHA.

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the High court at Arusha on **14th** day of **May, 2019** at 09: 00 am in the forenoon.

YOU may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time for mention, the court may proceed in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of the **COURT** this **30th** day of **APRIL, 2019**

HIGH COURT OF TANZANIA

***J. F Nkwabi***

**DEPUTY REGISTRAR**

**ARUSHA**

# Kada wa Chadema alivyookotwa na bodaboda porini

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimesimulia namna bodaboda walivyomuokota Mkufunzi wa Chadema Kanda ya Nyasa, Mdude Nyagali, katika uchochoro msituni akijikokota kuomba msaada na kumpatia huduma ya kwanza.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chadema, John Mrema alisema Mdude aliokotwa majira ya saa tatu asubuhi akitoka eneo la msituni katika kijiji cha Mwakwenje katika Kata ya Inyala akijikongoja kuingia katika chochoro akiomba msaada.

Alisema vijana hao wa bodaboda walipomuona na kwa sababu hakuwa na nguvu ya kuzungumza walimsachi katika mifuko yake na kuona vitambulisho vyake kimoja cha Chama chake na cha kupigia kura.

"Jana usiku saa tatu tulipata taarifa kutoka kwa raia, kwamba kuna mtu ameokotwa na vijana wa bodaboda akiwa aneo la msituni kwenye kauchochoro akiwa anajikongoja akijaribu kuomba msaada ila alikuwa hawezi kuzungumza kwa sababu alikuwa amefungwa mdomo na uso na kitambaa cheusi,"

"Baada ya vijana hawa wa boda kumuokota walimpekua wakamkuta na vitambulisho viwili na wakakuta majina ya Mdude ndiyo wakajua ndiye.

# Serikali yaahirisha ujenzi

INATOKA UK. 4

(Km 8.3) kwa kiwango cha lami upo katika hatua ya ununuzi.

Waziri Kamwelwe alisema upambuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Morogoro – Dodoma yenye urefu wa Km 260 taratibu kwa ajili ya kumpata mhandisi mshauri wa kufanya kazi hiyo zinaendelea.

"Ujenzi wa Barabara ya New Bagamoyo (Morocco) Junction Mwenge - Tegeta yenye urefu wa Km 17.2 hadi Machi, mwaka huu, mkataba wa upanuzi wa sehemu ya Morocco na Mwenge Km 4.3 ulikuwa umetiwa saini kwa ufadhili wa Serikali ya Japan," alisema.

Katika hotuba yake hiyo, Waziri Kamwelwe pia aligusia ujenzi wa barabara za juu (flyover/interchange na maboresho unaoendelea katika Jiji la Dar es Salaam.

Alisema ujenzi wa barabara ya juu katika makutano ya Tazara umekamilika huku ile ya makutano ya Ubungo ukiwa umefikia asilimia 28.

"Kazi ya uhamishaji wa miundombinu iliyoathiriwa na mradi wa Ubungo Interchange imekamilika na mkandarasi anaendelea na ujenzi wa barabara za makutano," alisema.

Waziri huyo alisema mradi wa arabara ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) unalenga kuipanua barabara hiyo kuwa ya njia sita na utajumuisha miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya tatu, ambapo hadi Machi 2019 usanifu wa kina ulikuwa unaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia (WB).

# Urafiki wa JWTZ, Ujerumani kuimarika

**Na Beatrice Moses**

JESHI la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) litaendelea kupokea misaada zaidi kutoka kwa Serikali ya Shirikisho la Ujerumani kupitia Mpango wa kusaidia majeshi rafiki.

JWTZ itaendelea kunufaika baada ya Ujerumani kukubali kuongeza kipindi cha kutoa misaada kwa miaka minne zaidi kuanzia mwaka 2021 hadi mwaka 2024.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Mkurugenzi wa Mawasilano ya Rais, Ikulu Gerson Msigwa, imebainisha kuwa uamuzi huo umebainishwa jana na Balozi wa Ujerumani Dk. Detlef Waechter.

Imeelezwa kuwa Balozi Waechter alibainisha hatua hiyo katika mazungumzo yake na Rais John Magufuli, Ikulu jijini Dar es Salaam

Balozi Waechter aliambatana na wajumbe kutoka Wizara ya Ulinzi na Wizara ya Mambo ya Nje ya Ujerumani, ambapo pamoja na mambo mengine wameahidi kujenga hospitali kubwa yenye viwango vya daraja la nne (level 4) mkoani Dodoma.

Dk Waechter alisema pamoja na ujenzi huo, pia kupitia timu ya ushauri ya wataalam wa kijeshi (GAFTAG) Ujerumani itaendelea kufundisha madaktari wa jeshi na kutoa vifaa vya matibabu. Pia itaongeza kutoa mafunzo ya ulinzi na vifaa vya ulinzi wa amani.

Ilibainishwa kuwa katika makubaliano ya ushirikiano unaoishia 2021 Ujerumani kati ya Juni 2017 na Machi 2019 imejenga Hospitali ya Kanda Monduli mkoani Arusha ambayo imewekewa vifaa vya tiba vinavyotumia teknolojia ya kisasa na inatarajiwa kuwa hospitali ya rufani ikisaidiana na Hospitali ya Kijeshi ya Lugalo iliyopo jijini Dar es Salaam.

Ujenzi wa hospitali hiyo unatajwa kuwa umegharimu Sh. bilioni 5 na milioni 947 ambapo kati ya hizo Sh. milioni 346.8 zimetolewa na Serikali ya Tanzania.

Kupitia urafiki huo kumefanyika upanuzi na uboreshaji wa Chuo cha Sayansi na Tiba cha Lugalo,ujenzi wa karakana za jeshi katika Mkoa wa Dar es Salaam, Dodoma, Shinyanga na Mwanza, ujenzi wa udara ya dharura ya Hospitali kuu ya Jeshi Lugalo.

Ilielezwa kua pia kumefanyika ujenzi wa mabweni ya wanafunzi katika hospitali ya Kanda Bububu Zanzibar, uboreshaji wa hospitali za kanda zilizopo Zanzibar, Mbeya, Mwanza na Tabora, msaada wa magari na vifaa tiba.

Rais Magufuli aliishukuru Serikali ya Ujerumani kwa kuendeleza na kukuza uhusiano na ushirikiano na Tanzania.


MINISTRY OF EDUCATION,SCIENCE AND TECHNOLOGY
AGENCY FOR THE DEVELOPMENT OF EDUCATIONAL MANAGEMENT (ADEM) - BAGAMOYO

**INVITATION FOR APPLICATION TO A DIPLOMA IN EDUCATION MANAGEMENT AND ADMINISTRATION (DEMA) AND DIPLOMA IN SCHOOL INSPECTION (DSI) FOR THE ACADEMIC YEAR 2019/2020**

**Applicants are invited from suitable qualified candidates to pursue a two year Diploma courses in Education Management and Administration and Diploma in School Inspection offered by the Agency for the Development of Educational Management (ADEM). Applicants should specify the campus they wish to study, either at ADEM-Bagamoyo, ADEM-Mwanza or ADEM-Mbeya. The course commences in October, 2019**

**1. BASIC INFORMATION**

**A: Target groups: Applicants should be in-service teachers, school heads or educational managers and administrators at Ward, District, Regional or Zonal levels. These include**

(i) District Education Officials (District Education Officers, Statistics and Logistics Officers, District Academic Officers and Teachers Service Commission Officials.
(ii) Ward Education Coordinators (WECs).
(iii) Heads of Schools (Primary and Secondary).
(iv) Teachers from pre-primary, primary schools, secondary schools and colleges who have been in the teaching service for not less than three years.
(v) Managers and Owners of Non-Government Schools such as Religious, Military, Private and Investors in education service.
(vi) Workers in Non-Government Organizations (NGOs) dealing with education, etc.
(vii) School Quality Assurers ( School Inspectors)

**B: Requirements for DIPLOMA IN EDUCATION MANAGEMENT AND ADMINISTRATION (DEMA).**
Applicants should be IN-SERVICE teachers or education officers who hold any of the following qualifications, with a minimum of three years working experience:

- Grade A Teacher Certificate with a minimum of four passes in CSEE
- Diploma in Education from any recognized institution.
- Bachelor degree and above, in education
- Certificate in Education Leadership, Management and Administration (CELMA) offered by ADEM

**C: Requirements for DIPLOMA IN SCHOOL INSPECTION (DSI)**
Applicants should be IN-SERVICE teachers or education officers who hold any of the following qualifications, with a minimum of five years working experience:

- Grade A Teacher Certificate, with a minimum of two credits in CSEE.
- Diploma in Education
- Bachelor degree and above, in education
- School Quality Assurer (School Inspector)

**2.REQUIRED ENCLOSURES:**

a) Curriculum Vitae including name, address, telephone, educational background and professional career.
b) Photocopies of Certificate of academic and professional qualifications
c) Photocopies of professional qualifications in Education certificates (Teacher Grade A, Diploma or Degree)
d) Non-refundable application fee of Tshs. 10,000/= paid through:
(i ) NMB Bank by filling Pay-in-Slip and quote Control Number 991250002327
(ii) M-Pesa, Tigo-Pesa under Government Payment Control Number 991250002327

**3. MODE OF APPLICATION:**

a) Candidates must **APPLY DIRECT TO ADEM in response to this advertisement.by FILLING THE FORM PROVIDED** at ADEM website or writing an applican letter. Applicants who were not selected for Academic Year 2018/19 are allowed to re-apply for academic year 2019/20. .

****APPLY DIRECT TO ADEM BY FILLING THE FORM PROVIDED ****

b) Applications must be written in English.
c) Applications must reach the undersigned **not later than 30th July, 2019.**
d) Only successful candidates will be informed by the end of **AUGUST, 2019.**

4. **All applications done direct through ADEM should be addressed to:**
**The Chief Executive, ADEM, P. O. Box 71, BAGAMOYO**

5. **For more information visit our website: www.adem.ac.tz or contact the following addresses:**

**BAGAMOYO MAIN CAMPUS**
**E-mail: adem@adem.ac.tz**
**• Fax: +255 23 2440216**
**• Tel: +255 23 2440225/2440022**

**MWANZA CAMPUS**
**E-Mail: ademwz@adem.ac.tz**
**Fax: +255 28 2540185**
**Tel: +255 28 2540185**

**MBEYA CAMPUS**
**P.O.BOX 187, MBEYA**
**E-mail: ademby@adem.ac.tz**
**Tel/Fax: 025 2502467**

**6: For further clarifications about programmes and services offered by ADEM, use the following mobile phones numbers:**

1. 0789 257 861
2. 0767 197 564
3. 0786 674 512
4. 0658 351 111

215220202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari muhimu Dar dhidi ya dengue

**TAARIFA** kwamba wakazi wengi wa Jiji la Dar es Salaam wanaugua ugonjwa wa homa ya dengue, zinapaswa kutushtua na kuchukua hatua za tahadhari.

Imeelezwa kuwa kwa kipindi cha Januari hadi Mei mwaka huu, jumla ya watu 1,200 katika mkoa mzima wa Dar es Salaam wameugua homa ya dengue na mtu mmoja kupoteza maisha.

Wagonjwa kadhaa wamebainika kutoka maeneo ya Ilala, Kariakoo, Upanga, Kisutu, Buguruni na Tabata wilayani Ilala. Mengine ni Ubungo, Mbezi wilayani Ubungo na Msasani, Masaki na Kinondoni wilayani Kinondoni.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Yudas Ndugile alitoa takwimu hizo hivi karibuni wakati akizungumza na Nipashe kuhusu hali ya ugonjwa ilivyo katika jiji hilo, lenye wakazi takribani milioni tano kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

Dk. Ngudile alibainisha kuwa wametoa tahadhari kadhaa katika kuudhibiti,ikiwamo za kuangamiza mazalia ya mbu kama vifuu, makopo, vyungu chakavu, matairi chakavu,na kufukia madimbwi kwenye maeneo ya makazi.

Ni vyema kuzingatia tahadhari zilizotolewa ikiwa ni pamoja na kusafisha maeneo ya ofisi, shule, vyuo, gereji, stendi za mabasi, masoko, maeneo ya mama lishe, baa, sehemu wanazouza vinywaji, hoteli, migahawa na hosteli za wanafunzi.

Pia wananchi wametakiwa kuepuka ugonjwa huo kwa kuzuia kung'atwa na mbu kwa kulala ndani ya chandarua chenye dawa, kupaka mafuta ya kufukuza mbu mikononi na miguuni na kuvaa nguo ndefu kufunika mwili kama mikono, miguu na mgogo.

Tumesikia Serikali kwa upande wake imechukua tahadhari kwa kufanya upuliziaji dawa za kuua mbu katika maeneo ya shule, vyuo, gereji, masoko, kwa mama lishe, kwenye baa, hoteli, migahawa, hosteli za wanafunzi na stendi za mabasi.

Hivi karibuni akiwasilisha bungeni hotuba kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, pamoja na mambo mengine naye aliwatahadharisha wananchi kuhusu ugonjwa huo.

Waziri Ummy aliwataka wananchi kuwa makini wapatapo homa wahakikishe wanakwenda kupata huduma katika vituo vya afya ili wapimwe na kupatiwa tiba sahihi.

Waziri alibainisha kuwa wizara imeshakamilisha mpango mkakati wa kudhibiti ugonjwa huo ambao unajumuisha kujenga uwezo wa watumishi wa afya katika kutambua, kupima, matibabu na udhibiti wa mbu wanaoueneza.

Homa ya dengue hutajwa pia kama homa ya kuvunja mifupa kwa sababu inaweza kuwafanya watu wawe na maumivu makali hadi wahisi kama mifupa yao inavunjika.

Dalili za ugonjwa huu huanza kujitokeza ndani ya siku tatu hadi kumi na nne baada ya kuambukizwa, ambapo aliyeambukizwa hupata homa kali, kuumwa na kichwa, kuota vipele kwenye ngozi na maumivu kwenye misuli na maungio au kuvuja damu.

Tunasisitiza kwamba wataalam wa afya wamekuwa wakituhamasisha kuwa kinga ni bora kuliko tiba, hivyo tuzingatie kwa kuzitekeleza mbinu za tahadhari tulizopewa ili kuepuka kuugua ugonjwa huu hatari.

Pia wananchi waache kupuuzia ugonjwa huo, bali wachukue hatua kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya na serikali kwa kuwa ugonjwa huo ni hatari kwa maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mabaraza ya Ardhi Kata yaboreshwe

Na Sabato Kasika

**MABARAZA** la Ardhi ya Kata yalianzishwa kwa lengo la kuhakikisha kesi au mashauri yanayohusu migogoro ya ardhi kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiji au mitaa yanapatiwa utatuzi wa kisheria katika ngazi za chini. Hiyo ni kwa kuzingatia sheria na kanuni ziheshimu mipaka yake kiutendaji.

Kimsingi, lengo la kuanzishwa mabaraza hayo lilikuwa sahihi, lakini mifumo iliyowekwa ya upatikanaji wa viongozi wanaoendesha mabaraza hayo, imeonekana kukosa nguvu hivi sasa, katika wakati huu dunia inapogeuka kuwa kijiji.

Watu wengi wana wana ufahamu mkubwa wa sheria, hivyo wanatambua haki zao au hata mipaka ya mamlaka mbalimbali za kisheria.

Mabaraza hayo yalianzishwa mwaka 1985 kwa Sheria ya Bunge Namba Saba, wakizingatia kwamba migogoro mingi ya ardhi ipo katika ngazi za chini, ambako wananchi wengi wanaishi au kuendesha shughuli zao ndogo zinazowapatia vipato, zikiwamo biashara, kilimo na ufugaji.

Kwa maana hiyo, chombo hicho katika hatua hiyo, kingesaidia kupatikana ufumbuzi wa kisheria na kupunguza wingi wa kesi kama hizo, kwenye ngazi za wilaya, mkoa na Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi.

Nadhani umefika wakati kwa serikali kuangalia uwezekano wa mabaraza hayo kuongozwa na watalaam wenye weledi mkubwa wa sheria.

Hivi sasa, wenyekiti wa mabaraza wanaweza kuwa watu maarufu wakati makatibu kwenye baadhi ya kata, ni maofisa wasio na weledi katika eneo hilo la kitaaluma.

Kwa sasa, kwenye baadhi ya kata, makatibu ni Maofisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya kata, ndio wameteuliwa kuongoza. Ni mfumo ambao sidhani unafaa kuendelea.

Ikumbukwe kuwa, sheria iliyounda Mabaraza ya Kata imeweka ukomo wa mashauri ya kusikilizwa katika ngazi hiyo, ikiwa na thamani ya shauri linalopokelewa na kusikilizwa hapo. Viongozi wanaweza kujibebesha majukumu wasiyoyastahili kisheria.

Wadau, wanapaswa waishauri serikali ibadilishe mfumo wa viongozi wa mabaraza hayo, ili halmashauri za miji na wilaya ziweke utaratibu wa kuyasimamia moja kwa moja, kwa kuteua wanasheria kutoka halmashauri na makatibu wakawa wajumbe wenye elimu, angalau astashahada ya sheria. Kumekuwapo migogoro kwenye baadhi ya Mabaraza ya Ardhi Kata, katika maeneo mengi nchini.

Mmoja wa wadau, Oliver Limwagu, anakumbusha wakati fulani Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alitishia kufuta mabaraza hayo mkoani mwake, baada ya kugundua kuwa ni vyanzo vikubwa vya migogoro.

"Wakati mwingine baadhi ya viongozi wamejikuta wakikwaruzana na wateja, kwa sababu mmoja kati ya washitakiwa au walalamikaji wanatoa siri wakati mashauri yakiendelea, jambo ambalo limekuwa likizalisha migogoro pia," anasema Limwagu.

Anasema, mabaraza ya viongozi wasio na weledi kuna wakati yanajikuta yakishughulikia mashauri yasiyowahusu kisheria, ikiwamo migogoro ya ardhi inayosajiliwa au thamani yake inazidi Sh. milioni tatu.

"Yanapojitokeza mazingira kama hayo, sijui kama uwepo wa mabaraza una maana na endapo hali itaendelea hivyo, kuna hatari kubwa ya kuibua migogoro mikubwa zaidi katika siku zijazo, hasa kutokana na ardhi kupanda thamani kila kukicha, huku mabaraza yakiwa hayatambui.

"Mahakama ni kama familia zetu, mume, mke na watoto wana mipaka yao. Kwa nini Mabaraza ya Kata yasiwe na mipaka kiutendaji?" anahoji.

Wakili Godfrey Francis, anasema mazingira ya mwaka 1985 kuanzishwa Mabaraza ya Kata, yaikuwa sahihi, lakini muda uliopo uana sura ya kupitwa na wakati. Mfumo wa uendeshwaji wake, usimamizi na utoaji haki, unapaswa kuboreshwa.

"Ikumbukwe kuwa, kubadilishwa mfumo wa uendeshwaji wa Mabaraza ya Kata, hauwezi kubadilishwa kisiasa kupitia matamko ya viongozi wa kisiasa majukwaani, bali kufanyia marekebisho Sheria ya Mabaraza ya Kata (Amendment)," anasema Francis

Ushauri wake ni sheria iruhusu wenyeviti wa Mabaraza ya Kata, wawe wataalamu wa sheria, kama wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya walivyo, ni wanasheria kwa taaluma. Anahoji kwanini kwenye kata wasiwe wanasheria?

"Sheria iruhusu uwakilishi wa mawakili kwenye kata kama kwenye mahakama za mwanzo wanataka waruhusu mawakili basi na kwenye mabaraza ya kata ni wakati muafaka umefika mawakili waruhusiwe ili matatizo yanayojitokeza sasa hivi ya sijitokeze tena," anasema.

Anasema hivi sasa, Mabaraza ya Kata yapo chini ya usimamizi wa halmashauri na kwamba huo ni mgongano, akitoa mfano, kesi inayoanzia Baraza la Kata, inaweza kupingwa maamuzi yake na kujikuta jalada limefika Mahakama Kuu, ambayo haipo chini ya usimamizi wa halmashauri.

Mdau mwingine, Esha Dismas, mtaalamu na Mshauri wa Sheria Vijijini, anakiri muundo wa sasa wa Mabaraza ya Ardhi ya Kata, umepitwa na wakati na njia pekee ni kuyafanyia mabadiliko.

==================

HUZUNI 1942 - 2019

# Bashiru amwombea msamaha Makonda

INATOKA UK. 2

uhai wake alihimiza zaidi kupanda miti ili kutunza mazingira na kuwataka wananchi kumuenzi kwa kupanda miti katika kipindi hiki.

Dk. Bashiru alisema marehemu aliweka katika kukuza maarifa na taarifa ambapo uwekezaji wake katika vyombo vya habari umekuwa na mchango mkubwa wa kujenga taifa na hasa utaifa na umoja wetu.

Alisema kuwa, vyombo vyake vimesaidia kukuza Kiswahili kama lugha ya Taifa kupitia radio na kudai kuwa Taifa bado ni teketeke tusipojihadhari tunaweza kupoteza misingi yetu ya Taifa hivyo mchango huo unapaswa kuendelezwa. Katibu mkuu huyo alisema katika kipindi cha mwezi Aprili mwaka huu, marehemu alimpigia simu nyingi na kukubaliana wakutane na hakujua ni nini anachotaka wazungumzie lakini kulikuwa na ubishano wa muda mrefu wapi wakutane na lini ambapo yeye aliomba mfuate nyumbani au ofisini lakini marehemu alikataa na kuahidi yeye mwenyewe atamfuata nyumbani.

"Kitabu cha Dk. Mengi ni lazima kitafsiriwe hivyo kupitia Bakita (Baraza la Kiswahili Tanzania) chini ya usimamizi wa Wizara ya Habari na Utamaduni kitabu hiki kitafsiriwe ili Watanzania wote waweze kukisoma kwa lugha ya Taifa" alisema Dk. Bashiru.

**MAKONDA AOMBA RADHI**

Baada ya kauli hiyo ya Dk. Bashiru kumuombea msamaha RC Makonda, Askofu Shoo alimwita Mkuu huyo wa mkoa na kutangaza madhabahuni kwamba ametoa msamaha kwa kiongozi huyo.

Askofu Shoo akasema, "Basi mwanangu utusamehe kama tumekukosea, naomba tu utapata nafasi nyingine ya kuzungumza hapa ni madhabahuni, tumesema kwa ajili ya upatanisho... Mheshimiwa Mbowe nakuomba, waimba nyimbo ya ndugu wakipatana vyema mahali wanapokaa...wanashikana mikono."

Baada ya dakika chake, Makonda akasema, "Mheshimiwa baba Askofu na Kaka yangu Mbowe, wananchi mlioko hapa akiwamo na kiongozi wetu wa serikali nashukuru sana kwa kunipa maelekezo na maonyo ya baba Askofu lakini niwashukuru sana kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kusimama na kuomba radhi kwa niaba yangu, huo ni upendo wa hali ya juu sana.

"Lakini nimshukuru sana kaka yangu Freeman Mbowe ambaye mimi na yeye tunafahamiana kwa muda mrefu sana na mbele yetu ni baba yetu kipenzi Regnald Mengi, kuyatamka yale ambayo yalimkwaza, naye nampa shukrani sana angeweza kukaa kimya.

"Lakini la mwisho kwangu, ninahisi tafsiri inaweza kuwa ni tatizo. Ni mimi niombe radhi kwa tafsiri hii kwa sababu nimemsifia mchaga katikati ya Wachaga. Sio mchaga tofauti na kabila jingine, nitaendelea kumuenzi mzee Mengi kwa mema yote aliyoyafanya hasa katika mkoa wetu kwa kuwahudumia walemavu. Kwa sababu amebaki kuwa alama ambayo haitafutika daima,"



Waziri Mkuu kassim majaliwa akiweka shada la maua kwenye kaburi la marehemu Dk. Reginald Abraham Mengi, wakati wa mazishi yake, yaliyofanyika kijiji kwao, Kisereni, Kata ya Machame, wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## Spika akemea vikali matumizi mitandao

INATOKA UK. 3

ya nchi na nje ya mipaka ya nchi.

Alisema wakati wa uhai wake, Dk. Mengi alionyesha kwa vitendo kwa vijana wa Tanzania kuwa, kwa juhudi na maarifa inawezekana kuondokana na umaskini na kuwa tajiri wa mali.

"Mzee Mengi ulikuwa na upendo, ukawa baba wa yatima, wajane, watu wasiojiweza na wagonjwa, umefanya mengi yenye heshima kubwa na kama mnavyojua hivi sasa Bunge linaendelea Jijini Dodoma lakini kwa heshima yako, Wabunge wenzangu wamenituma na kuacha shughuli zote na kuja kutoa heshima za Wabunge wote kwa kazi kubwa uliojitolea kuwafanyia Watanzania wote,"alieleza Ndugai

Kwa mujibu wa Ndugai, marehemu Dk. Mengi alikuwa msaada mkubwa kwa watu, serikali pamoja na Bunge, licha ya kumiliki vyombo mbalimbali vya habari zikiwamo redio, magazeti na televisheni.

## Mbowe akemea kauli za ubaguzi

INATOKA UK. 2

'Kauli za kuambiana kuna kabila fulani hayawezi kuwatetea walemavu, sio za kweli, ni za kibaguzi na lazima zikemewe na naomba wale wote walioguswa na kauli zile tutoe msamaha kwa kumuenzi marehemu, lakini tujifunze kusema ukweli na ukweli utatuweka huru,"alisema Mbowe

Mbowe ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Hai, alisema marehemu Dk. Mengi alikuwa mnyenyekevu na kauli zake mara kwa mara zililenga kujenga, kupatanisha kutoa matumaini na hakuwa mtu wa kukata tamaa, hivyo tunapaswa kumuenzi kwa kuyaiga.

Alisema katika mazingira ya kawaida ya binadamu, vitu viwili hujenga kiburi ambavyo ni mamlaka yasipotumiwa vizuri hujenga kiburi na fedha zisipotumika kwa ustaarabu hujenga kiburi.

Katika salaam zake, Mbowe alisema marehemu hakuwa kiongozi wa serikali wala kiongozi wa siasa, lakini alikuwa mnyenyekevu wa kipekee, tena wa ajabu sana na uwezo wa utajiri wake haukumtia kiburi ila ulimuongezea unyenyekevu na misaada kwa wengi aliowajua na asiowajua.

# Membe asifu mchango wake sekta binafsi

NATOKA UK. 2

Kwa mujibu wa Membe, alipenda na alitaka kuiona Tanzania ikiwa nchi ya amani, utulivu, inayoheshimu sheria, katiba na uongozi bora

Alisema hakuwa na ubaguzi kwa kuwa hakujali unatoka chama gani, bali alichoangalia ni msingi aliyoisimamia na aliunga mkono.

"Katika shughuli zetu za siasa zinazokuja mbele ya safari, miaka nenda rudi tumepotea mtu aliyekuwa anatoa mchango kwa vyama vyote kwa lengo la kuwa na utawala bora, sheria, kuwahimiza watanzania kuwa maendeleo ya kweli hayatoki serikalini bali sekta binafsi," alisema.

Membe alisema alifahamiana naye toka mwaka 1999 na wamekuwa marafiki wa karibu na hasa alivyokuwa Waziri wa Mambo ya Nje (wakati huo) kwa miaka tisa.

"Alikuwa mshauri wa mabalozi na alifanyakazi vizuri na wizara na siyo kwa kushauri mabalozi kuhusu sekta binafsi na biashara, lakini alikuwa kiungo cha serikali na sekta binafasi, serikali na mabalozi na hasa kuhusiana na sekta binafsi kama gurudumu halisi la maendeleo," alisema.

Alisema kwaka 2009 na 2010 Saomali ilikumbwa na njaa kwa watuz aidi ya watu milioni 10, Rais Jakaya Kikwete alimteua Mengi kuwa mwenyekiti wa wafanyabiashara wa kutafuta michango kutoka kwa wafanyabiashara, ambayo ilisaidia sana wananchi wa nchi hiyo.

"Alifanyakazi kubwa kupata michango mbalimbali, tulipata malori ya chakula na bidhaa ambayo yalipeleka chakula kupitia Kenya, na kuwasaidia waafrika wenzetu ambao walikuwa wanakabiliwa na njaa. Ni mchango wake mkubwa ambao Wizara ya Mambo ya Ndani tulifurahi sana na hatuwezi kusahau," alisema.

Kwa mujibu wa Membe, kila mwezi Mengi alialika mabalozi wawili hadi watatu nyumbani kwake kwa chakula, na kila mwaka balozi zikiadhimisha siku ya uhuru wao Mengi hakukosekana kuhudhuria.

"Mimi nilikuwa nachapa siasa yeye anachapa uchumi kwa sekta binafsi, tunaweza kumuuita alikuwa kiongozi wa mabalozi Tanzania, kwani mbali na jitihada za kusaidia watnzania wengine, kujitolea na kufanya ambayo mtu mwingine hawezi kufanya, na mbali ya kumuheshimu Mungu kupitia mali zake alitoka nje ya mipaka ya Tanzania na kusaidia watu wenye shida," alibainisha.

Kwa mujibu wa Membe, Tanzania na dunia imempoteza mtu wa watu aliyekuwa na moyo wa upendo na unyenyekevu.

Membe alisema walikuwa na urafiki mkubwa hadi ngazi ya familia kwa kipindi cha miaka 12, na aliunga mkono jitihada zake zote ikiwamo za kugombea urais mwaka 2015.

"Mzee Mengi hakuwa mbaguzi yeyote aliyeonyesha nia nzuri ya kugombea nafasi ya juu alimuunga mkono. Mimi aliniunga mkono kama alivyowaunga mkono wengine, wapo waliokataa ila mimi nilikubali," alisema.

# Serikali yaahidi kuenzi mazuri aliyofanya Mengi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, jana aliongoza maelfu ya watu katika shughuli ya kuhitimisha safari ya mwisho duniani ya aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk.Regnald Mengi aliyezikwa nyumbani kwake Kisereni, Kijiji cha Nkuu Sinde, Wilaya ya Hai, akieleza kuwa serikali itaendelea kuyaenzi aliyokuwa akiyafanya marehemu.

Akitoa salaam za serikali katika ibada ya mazishi ya Dk. Mengi, Majaliwa aliwaeleza waombolezaji kuwa amekuja Kilimanjaro na salaam kutoka kwa Rais Dk. John Magufuli na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ambao wote wanawaombea, lakini wanawapa pole kwa msiba huo mzito.

"Huu ni msiba mkubwa, mzito kwa kumpoteza kama ambavyo baba Askofu Mkuu (Dk. Shoo) kasema. Huyu mzee Mengi ni mmoja wa watu wazalendo kabisa kutokea katika historia ya nchi yetu. Nimuombe Mwenyenzi Mungu aendelee kutupa nguvu ya kumsindikiza katika nyumba yake ya milele," alisema Waziri Mkuu

Katika hotuba yake, Waziri Mkuu alisema hakuna mtanzania asiyejua mchango uliotolewa na Dk. Regnald Mengi wakati wa uhai wake kwa ajili ya kuwasaidia watanzania na taifa zima.

Alisema serikali itaendelea kuyaenzi yale yote yaliyokuwa yakifanywa na Mwenyekiti huyo mtendaji wa IPP.




Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), John Mrema akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa taarifa ya kupatikana kwa mfuasi wa chama hicho, Mdude Nyagali, baada ya kudaiwa kutekwa na watu wasiojulikana Jumamosi jioni wiki iliyopita mjini Vwawa-Mbozi mkoani Songwe. Mdude alipatikana katika eneo la Inyala Mbeya Vijijini. Kushoto ni Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Chama hicho, Tumaini Makene. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Hoja 8 za upinzani bajeti wizara ujenzi

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni, imeitaka serikali kuzitolea ufafanuzi hoja nane zinazohusu masuala ya ujenzi, uchukuzi, mawasiliano na utawala bora.

Akisoma bungeni jana hotuba ya Msemaji Mkuu wa kambi hiyo katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, James Mbatia, kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, Mbunge wa Mrimba, Suzan Kiwanga (Chadema), alizitaja hoja hizo kuwa ni pamoja na serikali kutelekeza mradi wa gesi na kuanza kutekeleza mradi mpya wa umeme wa maji katika Mto Rufiji (Stiegler's Gorge).

Alisema nchi iliaminishwa na serikali kwamba inaingia katika uchumi wa gesi na kukajengwa bomba la gesi kutoka Dar es Salaam hadi Mtwara, lakini ripoti za kitaalamu zimebainisha kuwa bomba hilo linatumika kwa asilimia sita tu ya uwezo wake.

"Jambo la kusikitisha ni kwamba mradi huu umepigwa chini na sasa tunakimbizana na ujenzi wa Stiegler's Gorge. Kambi Rasmi ya Upinzani inapata shaka sana na umakini wetu katika kuhakikisha tunafikia uchumi wa kati," alisema.

Kiwanga pia alisema kambi yao inahoji kuhusu kile inachoamini kutozingatiwa kwa misingi ya utawala bora katika kuupa zabuni mbalimbali Wakala wa Majengo Tanzania (TBA).

Alisema hivi karibuni kumekuwa na malalamiko mengi kutoka serikalini kutokana na utendaji usioridhisha wa wakala huo, lakini kambi yao inaamini malalamiko hayo ni matokeo ya wakala huo kupewa zabuni kwa kulazimishwa na kutofuata taratibu za utoaji zabuni.

"Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kufahamu hiyo miradi inayotoka wizara na idara na taasisi za serikali inaletwa tu kwa TBA kama zawadi au kuna utaratibu wa kufuata sheria ya ununuzi unafanyika, kama utaratibu haufanyiki ni hatua gani za kinidhamu kwa wahusika zinachukuliwa?" alihoji.

Kiwanga alisema kambi yao pia inasikitika kuona serikali inaboresha viwanja vya ndege pasi na kuboresha huduma zinazotolewa kwenye viwanja hivyo, akitolea mfano ujenzi wa hoteli za kisasa ili uboreshaji wa viwanja uende sambamba na kutoa fursa ya ajira kwa Watanzania.

Kiwanga alisema kambi inaiasa serikali kuangalia kwa umakini uamuzi inaoufanya wa kuhamisha majukumu ya Wakala wa Ndege za Serikali ya kusimamia ndege za serikali kwenda Ofisi ya Rais, wakiamini jambo hilo ni hatari kwa matumizi ya fedha za umma kwa kuwa fungu 20 yanakohamia majukumu hayo haliruhusiwi kukaguliwa.

Kambi hiyo pia ilihoji kuhusu mauzo ya nyumba za serikali 7,921 yaliyofanyika kati ya mwaka 2004 na 2008, ikiitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) ichunguze suala hilo.

Katika hotuba hiyo, upinzani pia uliitaka serikali kuhakikisha inatenga bajeti inayotekelezeka ikibainisha kuwa kati ya Sh. trilioni 2.3 zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya wizara hiyo, ni Sh. bilioni 391.162 (asilimia 17) zilizotolewa hadi Februari mwaka huu.

Kiwanga alisema kambi yao pia inahoji sababu za serikali kuamua kutekeleza mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kwa kutumia malighafi ya nje badala ya kufungamisha na uchumi wa nchi kwa kuhakikisha chuma cha ndani kinatumika.

Kambi hiyo pia iliitaka serikali kueleza sababu za kutofanyia kazi ushauri wake kuboresha huduma za bandari nchini, ikileleza kuwa Bandari ya Dar as Salaam imeendelea kufanya vibaya kulinganishwa na bandari za nchi jirani.

Kambi hiyo pia iliitaka serikali kueleza sababu za kufanya vibaya kwa Shirika la Mawasiliano (TTCL) ilhali imetoa fedha nyingi kwa kampuni za simu kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na kampuni ] zilizonufaika kwa kiwango kikubwa na uwekezaji huo ni Halotel, Vodacom na TTCL.

## Matatani tuhuma za kusafirisha 'unga' D'Salaam

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI wawili wa jijini Dar es Salaam wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam wakikabiliwa na tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroine gramu 501.11.

Washtakiwa hao ni, mkazi wa Vingunguti Fon Kabwe na Mfanyabiashara Abass Seguye, na walisomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega.

Wakili wa Serikali, Faraji Nguka alidai walitenda kosa hilo Septemba 20, 2016 eneo la kituo cha mabasi Ubungo, jijini Dar es Salaam.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, hakimu aliwataka washtakiwa hao kutojibu lolote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza shauri lao mpaka Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) atakapotoa kibali.

Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi haujakamilika na kesi iliahirishwa hadi Mei 23, mwaka huu.

## Serikali yaahirisha ujenzi barabara

INATOKA UK. 4

(Km 8.3) kwa kiwango cha lami upo katika hatua ya ununuzi.

Waziri Kamwelwe alisema upambuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Morogoro – Dodoma yenye urefu wa Km 260 taratibu kwa ajili ya kumpata mhandisi mshauri wa kufanya kazi hiyo zinaendelea.

"Ujenzi wa Barabara ya New Bagamoyo (Morocco) Junction Mwenge - Tegeta yenye urefu wa Km 17.2 hadi Machi, mwaka huu, mkataba wa upanuzi wa sehemu ya Morocco na Mwenge Km 4.3 ulikuwa umetiwa saini kwa ufadhili wa Serikali ya Japan," alisema.

Katika hotuba yake hiyo, Waziri Kamwelwe pia aligusia ujenzi wa barabara za juu (flyover/interchange na maboresho unaoendelea katika Jiji la Dar es Salaam.

Alisema ujenzi wa barabara ya juu katika makutano ya Tazara umekamilika huku ile ya makutano ya Ubungo ukiwa umefikia asilimia 28.

"Kazi ya uhamishaji wa miundombinu iliyoathiriwa na mradi wa Ubungo Interchange imekamilika na mkandarasi anaendelea na ujenzi wa barabara za makutano," alisema.

Waziri huyo alisema mradi wa arabara ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) unalenga kuipanua barabara hiyo kuwa ya njia sita na utajumuisha miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya tatu, ambapo hadi Machi 2019 usanifu wa kina ulikuwa unaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia (WB).

HABARI KITAIFA

# Bosi wa Bandari Saccos aja juu tuhuma uporaji viwanja

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Bandari Saccos, Stella Mutayabarwa, amepuuza madai ya wakazi wa Pemba Mnazi wilayani Kigamboni jijini Dar es Salaam kuvamia viwanja vyao na kuweka mipaka upya mwezi uliopita.

Akizungumza na Nipashe, Mutayabarwa alisema taarifa kwamba alivamia viwanja vya wanakijiji katika Kata ya Pemba Mnazi ni za uongo kwani uongozi wa vijiji vya Puna na Potea ndiyo umeuza maeneo mara mbilimbili. "Hivi unadhani taasisi kubwa kama Bandari Saccos inaweza kuvamia maeneo ya vijiji bila utaratibu kweli?" alihoji na kuendelea: "Waulize viongozi wa Puna."

Alisema maeneo ya Bandari Saccos yaliuzwa kwa watu wengine na viongozi wa vijiji vya Puna na Potea na kwamba taasisi yake ililazimika kuchukua hatua ili kuzuia uvamizi huo.

"Wanakijiji ni lazima wafurahi wakiona taasisi kubwa kama Bandari Saccos inakuja katika maeneo yao kwani itawaletea maendeleo kupitia uwekezaji itakaofanya," alisisitiza. Mwenyekiti huyo aliwataka viongozi wa wilaya mpya ya Kigamboni kuepuka kuchochea migogoro ya ardhi.

Viongozi na wanavijiji wa Puna na Potea walisema viongozi wa Bandari Saccos ulienda katika maeneo yao Aprili mwaka huu ukiwa na askari polisi wenye silaha za moto na kuondoa alama zote za mipaka ya viwanja vyao na kuanza kuweka mipaka upya.

Katika nyaraka za vikao na barua za kutafuta suluhu zilizoandikwa kwa uongozi wa wilaya ya Kigamboni, Mwenyekiti wa kijiji cha Puna, Ngobi Meza, aliuomba uongozi wa Manispaa kuzuia uvamizi wa Bandari Saccos kwani ilikuwa inavuruga utaratibu tangu mgogoro huo uanze mwaka 2016.

"Katika uchunguzi wetu, tumebaini kwamba ni kweli Bandari Saccos walinunua eneo kutoka kwa Rwegasira, lakini taasisi imeongeza eneo lake kwa kuvamia maeneo ya watu wengine na kuweka alama baada ya kuondoa zile za awali jambo ambalo limeleta mgogoro," alisema Meza katika barua yake ya Februari 2018 kwenda kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni.

Akiwataja baadhi ya watu ambao viwanja vyao vimevamiwa ni Ahmad Mussa, Iddi Mohamed, Jones Kilimbe, Valerie Kilimbe, Charles Kubeja, Masanja Kasubi, shija Shinganaji na Muddy Kaunda.

Mwenyekiti huyo wa Puna alisema baadhi ya wamiliki hao wana hati halali za wizara ya ardhi, na kwamba wanalipia kodi viwanja vyao kila mwaka.

Katika barua ya Aprili 3, 2019 alimuandikia Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Meza alionya kwamba uvamizi unaoambatana na nguvu ya polisi unaweza kuleta maafa katika vijiji vyao kama weye mamlaka hawatachukua hatua.



Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Mwanzo Temeke, Bridgeter Pilla, akizungumza katika warsha ya utoaji taarifa ya utendaji kazi wa kamati za kuzuia ukatili dhidi ya watoto shuleni, iliyoandaliwa na asasi ya kiraia ya Ekama Development Tanzania, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wazazi wahimizwa malezi bora kwa watoto

**Na Sabato Kasika**

WAZAZI wametakiwa kusimamia vyema malezi bora ili kusaidia kutokomeza vitendo vya ukatili ambavyo baadhi ya watoto wamekuwa wakifanyiwa au kufanyiana wenyewe.

Mbali na hilo, wamekumbushwa kuzingatia kaulimbiu ya mke wa Rais wa Awamu ya Nne, Mama Salma Kikwete isemayo, 'mtoto wa mwenzio ni wako' kwa kutoa taarifa wanapoona ukatili unafanyika au unataka kufanyika.

Hayo yalisemwa na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Mwanzo Temeke, jijini Dar es Salaam, Bridgeter Pilla, wakati akifungua warsha ya utoaji wa taarifa ya utendaji kazi wa kamati za kuzuia ukatili dhidi ya watoto shuleni. Warsha hiyo iliandaliwa na asasi ya kiraia ya Ekama Development Tanzania na kushirikisha watu 150 wakiwamo maafisa wa ustawi wa jamii, polisi walimu, wanafunzi, wazazi na viongozi wa dini.

"Wazazi tusiwe wakali kupita kiasi, tuwafanye watoto kuwa marafiki wanaweza kutupa taarifa nyingi za vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa shuleni, mitaani na hata nyumbani," Hakimu Pilla alisema.

Alisema bila kufanya hivyo wanaweza kuharibiwa vibaya kwa kulawitiwa au kubakwa na matendo mengine mabaya na mwisho wa siku ni kuhatarisha maisha yao huku uwezekano wa kukomesha vitendo hivyo ukiwapo. "Wapo baadhi ya wazazi ambao kesi za ukatili dhidi ya watoto wao hufikishwa mahakamani, lakini hawaji kutoa ushahidi, sababu kubwa ni kwamba wanamaliza kesi kimya kimya na watuhumiwa nyumbani," alisema. Alisema mtindo huo unasababisha ukatili kuendelea kuwapo kwenye jamii na kwamba hata tabia ya wazazi kupigana mbele ya watoto haifai, hivyo waliozoea kufanya hivyo waache.

"Unakuta, mke anampiga mume au mume anampiga mke mbele ya watoto, hii ni tabia mbaya sana... mnawajenga vibaya watoto wenu jaribu kubadilika na kuwalea watoto katika maadili mema," alisema.

Aidha, alisema amewahi kupata kesi ya watoto waliokuwa wakiteswa na mama wa kambo kwa kupasuliwa nazi vichwani mwao, lakini mume na majirani wakawa hawatoi taarifa." Mtoto wa mwenzio ni wako'," alisisitiza.

## Prof. Mbarawa atumbua bosi DDCA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amefanya mabadiliko ya Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA) kuanzia juzi.

Prof. Mbarawa amefanya uamuzi huo baada ya kutengua uteuzi wa aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa DDCA, Domina Msonge.

Kufuatia mabadiliko hayo, Mhandisi Gonsalves Rwegasira Rutakyamirwa anakuwa Kaimu Mtendaji Mkuu wa DDCA.

Kwa mujibu wa taarifa ya wizara hiyo, kabla ya nafasi hiyo, Mhandisi Gonsalves alikuwa akifanya kazi Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA), akisimamia miradi ya maji ya pembezoni.

## Bima ya kulaza mama, watoto yaanza

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo kwa kushirikiana na Kampuni ya Bima ya Milvik, imezindua huduma ya bima mkononi ya kulazwa mama na watoto kwa watumiaji wa Tigo Pesa.

Huduma hiyo inawapatia watumiaji wa Tigo Pesa bima nafuu inayowalinda wao na watoto wao hadi watano kwa kuchangia gharama nafuu kwa mwezi kwa kila mtoto.

Meneja Mkuu wa Milvik, Benengere Lavisse, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu bima hiyo, alisema mteja wa bima hiyo atarejeshewa gharama za matibabu kama fidia kwa kila usiku utakayolazwa.

"Kwa kushirikiana na Tigo tumeona kuboresha huduma hii ya bima mkono inayowezesha wananchi wa maisha duni kupata huduma ya matibabu ndani ya siku tatu baada ya kutibiwa," alisema Lavisse.

Alisema toka wamezindua huduma ya kulazwa mwaka 2016, wateja wao wamekuwa wakiwaomba kuboresha kwa kujumuisha watoto kwa gharama nafuu. "Tumesikiliza mahitaji ya wateja wetu na kwa kushirikiana na wadau pamoja na Mamalaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania (Tira), tumefanyia kazi kuleta huduma hii ya bima ya kulazwa kwa watoto," alisema Lavisse. Naye Ofisa Mkuu wa Huduma ya Tigo Pesa, Hussein Sayed, alisema walifanya utafiti wa jinsi wanavyoweza kuongeza ushiriki wa jamii katika huduma za kifedha na hususani kwa wanawake na kaya.

Alisema matokeo ya utafiti yanaendana na mfumo ambao umeundwa na timu ya Milvik hivyo ninafurahi kutangaza maboresha huduma hiyo rasmi.

Naye Balozi wa Bima Mkononi, Zamaradi Mketema, alisema kama mama anaona umuhimu wa bima hiyo kwa watoto wake ambao wakiugua ana uhakika wa kupatiwa matibabu kwa gharama nafuu anayochangia.

# Neema ujenzi reli ya kusini

BUNGE limeelezwa kuwa serikali imeshakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya kutoka Mtwara-Mbambabay-Mchuchuma-Liganga yenye urefu wa kilometa 1,092.

Vilevile, imeelezwa kuwa mshauri mwelekezi wa kifedha na uwekezaji amepatikana, huku mkataba na mshauri wa uwekezaji ukitarajiwa kutiwa saini Juni mwaka huu.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, alipojibu swali la Mbunge wa Mtwara Vijijini (CCM), Hawa Ghasia.

Katika swali lake, Ghasia alihoji lini ujenzi kutoka Mtwara-Mbambabay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma utaanza.

Akijibu swali hilo, Nditiye alisema mshauri wa uwekezaji atakuwa na jukumu la kuunadi mradi huo kwa wawekezaji mbalimbali, ikizingatiwa kuwa mradi huo unatekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP).

"Hii ni katika kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika ujenzi wa reli nchini, hivyo baada ya kukamilika kwa utaratibu wa kumpata mwekezaji kwa njia ya PPP, ujenzi wa reli hii utaanza," alisema. Aliongeza kuwa wamekuwa wakipokea wawekezaji wanaohitaji kuwekeza katika reli hiyo na wamekuwa wakiwaelekeza kufuata sheria na taratibu za ununuzi kwa miradi inayotekelezwa kwa mfumo wa PPP.

"Taratibu hizo zinawaelekeza kuandaa na kuwasilisha wazo lao la kufanya uwekezaji kwa Shirika la Reli (TRC) ambalo litawasilishwa na TRC katika wizara yetu baada ya kuwa wamejidhirisha," alisema.

Nditiye alisema baada ya kuchambuliwa kwa kina na wizara, litawasilishwa katika kitengo cha PPP kilichoko Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi wao. "Wizara ya Fedha na Mipango kupitia kitengo hicho wakimaliza uchambuzi na kuridhia, mwekezaji atatakiwa naye kufanya upembuzi yakinifu wake ambao baadaye utalinganishwa na upembuzi yakinifu uliofanywa na serikali kabla ya kukamilisha taratibu za uwekezaji," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alisema ujenzi huo utakuwa na maana kama upanuzi wa bandari utakuwa umekamilika.

"Mpango uliokuwapo ulikuwa wa kujenga gati tatu lakini hadi sasa kuna gati moja, je, ni lini serikali itakamilisha ujenzi wa magati yote," alihoji.

Akijibu swali hilo, Nditiye alisema wameanza kupanua bandari ya Mtwara na watahakikisha mradi unakamilika kama ilivyopangwa.

"Kwa upande wa barabara, hivi karibuni mkandarasi atatangazwa wa kukarabati barabara hiyo," alisema.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo (wa tatu kushoto), akikagua matofali yanayofyatuliwa kwaajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma, jana. **PICHA: PAUL MABEJA**

## Serikali kununua injini mpya vivuko Ukerewe

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano iko katika harakati za kununua injini mpya kwa ajili ya vivuko vya Ukerewe na Nyamisati-Mafia ili maeneo hayo yawe na vivuko vipya.

Vilevile, imeelezwa kuwa serikali ina mkakati wa kuhakikisha huduma za usafiri zimeboreshwa katika maeneo yote nchini na kipaumbele ni kwenye maeneo yenye mahitaji maalum ili kuchochea kwa haraka shughuli za uchumi.

Waziri wa wizara hiyo, Isack Kamwelwe, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipojibu maswali la nyongeza kwa Mbunge wa Ukerewe (CCM), Joseph Mkundi.

Mbunge huyo alisema kuwa baada ya ajali ya Kivuko cha MV. Nyerere, serikali iliahidi kutengeneza kivuko kipya kwa ajili ya kusaidia wananchi wa eneo hilo.

"Ni hatua ipi imefikiwa ya ujenzi wa kivuko kitakachofanya safari Bugolola na Ukara?" mbunge huyo alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Kamwelwe alisema baada ya ajali, serikali ilishatangaza tenda na mkandarasi amepatikana.

"Mkataba umeshapatikana, sasa hivi tunaendelea kununua injini haraka ili kitakapokamilika kifungwe na kile cha Nyamisati-Mafia," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Musukuma, alitaka kujua ni lini serikali itajenga gati katika Kijiji cha Izumacheli.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa wizara hiyo, Atashasta Nditiye, alisema serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) imeandaa programu ya namna bora ya uboreshaji wa huduma za usafiri katika Ziwa Victoria kwa lengo la kubaini maeneo yote yanayohitaji ujenzi wa ama bandari au gati.

Alisema utekelezaji wa mpango huo unaendelea pamoja na ujenzi wa gati, maghala ya kuhifadhi mizigo na majengo ya abiria katika Bandari za Magarine (Muleba), Nyamirembe (Chato), Mwigobero (Musoma) na Lushamba (Geita) unaendelea.

"Naomba niwaambie wananchi wa Izumacheli mkoani Geita kuwa serikali inatekeleza mpango wake kwa awamu kutokana na ufinyu wa fedha.

"Hata hivyo, serikali itatoa kipaumbele kwa eneo hili katika awamu zinazofuata ili kuruhusu kukamiliki kwanza kwa miradi iliyokwishaanza katika Ziwa Victoria," alisema.

## Serikali yafafanua ulipaji kodi jengo la Tanapa

SERIKALI imesema Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ndiyo yenye jukumu la kulipa kodi ya jengo la Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) linalotumiwa na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ACPHR).

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, alipojibu swali la Mbunge wa Gando (CUF), Othman Omar Haji, kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema mahakama hiyo inatumia jengo la Tanapa lililoko Arusha kwa mkataba wa upangaji kati ya Tanapa na wizara hiyo ulioanza Desemba Mosi, 2008 kwa kodi ya Dola za Marekani 38,998.89 kwa mwezi.

"Je, kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na mahakama hiyo ni nani mwenye jukumu la haki za binadamu na nani mwenye jukumu la kulipa kodi ya jengo hilo?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Ole Nasha alisema mnamo mwaka 2007, serikali na Umoja wa Afrika ziliingia mkataba wa uenyeji wa mahakama hiyo na wizara hiyo ndiyo msimamizi na mtekelezaji mkuu wa mkataba huo kwa niaba ya serikali.

"Ibara ya 5(1) ya mkataba kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Afrika kuhusu uenyeji wa mahakama hiyo inaeleza kuwa Tanzania kwa gharama zake inawajibika kutoa majengo kwa ajili ya ofisi ya mahakama na makazi ya Rais na Msajili wa mahakama hiyo,"alisema.

Alisema hiyo pia inaipa Tanzania jukumu la kutoa ofisi ya muda kwa ajili ya mahakama husika wakati ikiendelea na taratibu za kupata jengo la kudumu la mahakama.

"Kutokana na kipengele hicho, serikali iliingia mkataba na Tanapa wa kukodisha majengo yake ili kuwa ofisi ya muda ya Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu," alisema.

Naibu waziri huyo alisema ni dhahiri kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mambo ya Nje ndiyo yenye jukumu la kulipa kodi hiyo kutokana na makubaliano yaliyofikiwa.

Hata hivyo, alisema suala la kulinda haki za binadamu ni suala la kila mtu na kila taasisi sehemu yoyote duniani.

"Kimsingi, hata Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inahusika moja kwa moja katika kulinda haki za binadamu," alisema.




**Habari zote na Augusta Njoji,**
DODOMA

## HABARI ARUSHA




Mchuuzi wa mbogaboga katika soko la Tengeru, Neema Saimon, akiandaa bidhaa zake tayari kwa kuwauzia wateja wake, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Viwango Tanzania, Kenya waaswa ukaguzi mpakani

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, amelitaka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Shirika la Viwango la Kenya (KEBS) kuhakikisha wanaharakisha ukaguzi wa bidhaa maeneo ya mpaka wa Namanga ili kuondoa malalamiko ya ucheleweshaji bidhaa za wafanyabiashara.

Mwaisumbe aliyasema hayo alipokuwa katika mpaka wa Namanga, kwenye Kituo cha Pamoja cha Forodha (OSBP), wakati wa utoaji wa mafunzo yaliyoandaliwa na TBS kwa waagizaji wa bidhaa na mawakala wa forodha wanaotumia mpaka huo.

Alisema ucheleweshwaji wa bidhaa maeneo ya mipakani husababisha malalamiko kwa wafanyabiashara hali inayosababisha wapate hasara inayotokana na kupoteza muda mpakani hapo.

Mwaisumbe alisema kama TBS na KEBS, wakishirikiana watarahisisha utoaji wa huduma bora kwa wafanyabiashara na kuepuka wafanyabiashara kukaa muda mrefu.

"Acheni urasimu kwa wafanyabiashara, kagueni bidhaa zao kwa wakati ili kuondoa malalamiko ya wafanyabiashara kuhusu ucheleweshwaji wa bidhaa maeneo ya mipakani,"alisema.

Akizungumza kuhusu changamoto ya ukubwa wa mpaka, alisema watahakikisha mpaka huo unaimarishwa ili kudhibiti uingizwaji holela wa bidhaa katika maeneo hayo.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Jabir Abdi, alisema kuanzishwa kwa kituo hicho cha forodha, kumeleta ufanisi kwa TBS kwa kuwa kumerahisisha utoaji wa huduma

Pia alisema mafunzo hayo ni endelevu na yamefanyika katika mikoa mbalimbali na kusisitiza wafanyabiashara kuhakikisha bidhaa zao zinakuwa na ubora ili kuondoa usumbufu maeneo ya mipakani.

Katibu wa Chama cha Mawakala wa Forodha mpaka wa Namanga, Jackon Karinda, alisema changamoto wanazokumbana nazo wafanyabiashara hao mpakani hapo ni ushindani wa biashara za marumaru kati yao na wafanyabishara wa Kenya, kwa sababu bidhaa za viwandani kutoka Tanzania kwenda Kenya hawazikubali, hali in-

# Meru kunufaika na mochwari ya kisasa

**Na Woinde Shizza,**
ARUSHA

WANANCHI wa Wilaya ya Arumeru, wapo mbioni kuondokana na adha ya ukosefu wa chumba cha kuhifadhia maiti, baada ya serikali kuwajengea mochwari mpya ya kisasa.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Jerry Muro, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Meru, Cosmas Kalasala, alisema ujenzi wake utagharimu Sh. milioni 160.

Alisema mpaka sasa ujenzi umekamilika kwa asilimia 80 na wanatarajia kukamilisha ujenzi huo hivi karibuni ili wananchi waweze kutumia jengo hilo na kuondokana na usumbufu wa kwenda kuhifadhi miili nje ya wilaya.

Mkuu wake, Muro alisema Serikali imeona tatizo hilo na kutoa fedha za mfuko wa Jimbo na kujenga chumba hicho katika hospitali hiyo.

"Fedha hizi za maendeleo ya mfuko wa jimbo ni za maendeleo ya wananchi wa Meru, hivyo tumefuata utaratibu wa kushirikisha wananchi tukachukua fedha hizi kwa ajili ya kuwajengea wananchi wetu chumba cha kuhifadhia maiti za wapendwa wao," alisema.

Alisema wananchi hao walikuwa wanapata tabu ndugu zao wanapofariki, kwa kuwa hospitali ya wilaya haikuwa na huduma hiyo kwa kipindi kirefu, hivyo walikuwa wanalazimika kwenda kuhifadhi miili katika Hospital ya mkoa ya Arusha ya Mount Meru, ambapo ni zaidi ya kilometa 20 kutoka Hospitali ya Wilaya.

Muro alisema jengo hilo linalojengwa ni kubwa na likikamilika litakuwa na uwezo wa kuhifadhi miili 45 hadi 50, na wanatarajia kulizindua rasmi katika mbio za Mwenge wa Uhuru mapema mwezi ujao.

## USAHIHI

**Katika gazeti hili toleo la juzi ukurasa huu, tuliandika kimakosa kuwa Mkuu wa Majeshi, Jenerali Venance Mabeyo ni Brigedia Jenerali. Tunasikitika kwa kosa hilo,**
**-Mhariri**

# Amri wavamizi wa Monduli kuondoka

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANANCHI waliovamia eneo la Tandamu linalotumika kukusanya maji ya kunywesha mifugo, katika Kata ya Engutoto iliyopo wilayani Monduli, wametakiwa kuondoka eneo hilo mara moja.

Eneo hilo la Tandamu ambalo lilikuwa linanywesha mifugo ya kata za Monduli, Engutoto na Lashaine limevamiwa na watu na kujenga nyumba pamoja na shughuli za kilimo, baada ya kujaa tope licha ya serikali kutoa zaidi ya Sh.milioni 650 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya bwawa hilo.

Akizungumza wakati wa ziara yake wilayani humo ya kukagua utekelezaji ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Arusha, Loata Sanare, ambaye pia aliongozana na watendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, waliuagiza uongozi wa halmashauri kuwaondoa watu hao ambao wanataka kuchukua haki ya wananchi wanyonge kwa nguvu.

"Nimefika eneo hili kwa ajili ya wananchi wanyonge ambao wanatuma ujumbe mfupi wa maneno kwa njia ya simu, kwenda kwa viongozi wa CCM Taifa... na wameniagiza nije kutatua kero hii na mimi nawahakikishia hatutakubali hati ya wananchi wanyonge kupokonywa na watu wenye nguvu ya fedha, lazima twende na falsafa ya Rais Magufuli ya kuhangaika na kutetea haki za wananchi wanyonge," alisema.

Loata alisema haiwezekani eneo hilo la wazi ambalo ni maalum kwa ajili ya kunywesha mifugo livamiwe na watu mpaka wajenge nyumba bila halmashauri kuchukua hatua zozote kwa sababu kwa kufanya hivyo ni kushindwa kumsaidia Rais, ambaye anahangaika na shida za wananchi wanyonge.

"Kuanzia sasa mkurugenzi na watumishi wa idara ya ardhi niombe mhakikishe watu wote waliovamia eneo hili na kujenga nyumba pamoja na wengine kulima mahindi waondoke mara moja kwa sababu ni eneo la umma na siyo mali ya mtu binafsi au kikundi cha watu wachache wenye maslahi binafsi," alisema.

Aidha alisema atazungumza na Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, ili atembelee eneo hilo na kujionea lilivyovamiwa na kuharibiwa, na hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa wote waliohusika.

# Siasa kwenye vyama vya ushirika yakera wakulima

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAKULIMA wa kahawa wa mikoa ya kanda ya Kaskazini ,wamesema kuwa baadhi ya vyama vya ushirika vimeingiza siasa inayoshusha thamani ya zao la kahawa.

Aidha, siasa hizo zimeathiri upatikanaji wa ruzuku ya asilimia 20 inayotokana na uuzwaji wa zao la kahawa, jambo ambalo limekuwa likishusha thamani na ubora wa zao hilo.

Mratibu wa mafunzo kwa wakulima wa mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, Agatha Shirima, aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa kuhitimisha mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa ugani.

Maofisa hao wanatakiwa kwenda kusambaza elimu hiyo kwenye kata mbalimbali, ili kutekeleza mpango wa ufufuaji na uendelezaji wa zao la kahawa kwa halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

Aidha, changamoto nyingine kwenye zao hilo ni wakulima kutozingatia kanuni bora za kilimo, kukosekana kwa huduma za ugani.

Wakulima hao wameiomba serikali kuandaa sheria ndogondogo za udhibiti wa zao hilo ili mkulima aweze kuzalisha kahawa yenye ubora na ambayo inazingatia kanuni bora za uzalishaji wa zao hilo ili kuliteka soko la kimataifa.

"Tunaiomba halmashauri kuandaa sheria ndogo ndogo ambazo zitaambana mkulima kuzingatia kanuni za uzalishaji wa kahawa bora, pia tunaiomba halmashauri kuwapatia wakulima asilimia 20 ya ruzuku inayotokana na uuzaji wa kahawa ili mkulima anufaike na kilimo chake cha zao la kahawa," alisema Shirima.

Katika mafunzo hayo changamoto zilizoibuliwa ni uhaba wa maofisa ugani ambao wengi wao wamepangiwa majukumu ya kusimamia vijiji na kata.

"Tunajua kuna uhaba wa watumishi katika halmashauri nyingi,tunaiomba serikali na hata halmashauri yetu kuangalia suala la kuajiri maofisa ugani, kwani ni watu muhimu sana kwa maendeleo ya kijiji na kata kwa ujumla kutokana na yeye kuwajibika kwa kiasi kikubwa katika utoaji elimu kwa mkulima na umuhimu wa kuwa na vitalu ndani ya vijiji," alisema Shirima.

Kwa upande wake, Afisa Kilimo mkoani Kilimanjaro, Edson Mchau, alisema serikali inatambua uhaba wa watumishi hususani maofisa ugani, na kwamba linafanyiwa kazi huku akizitaka halmashauri kuendelea kuwatumia wataalamu wachache waliopo.

Naye, mkulima wa kata ya Mbokomu, Anthony Makundi, alisema siasa zimekuwa chanzo kikubwa cha kutokuwepo kwa Ruzuku ya asilimia 20 kwa wakulima ambayo awali ilikuwa inapitia kwenye vyama vya ushirika.

Alisema tangu siasa zishike hatamu kwa baadhi ya vyama vya Ushirika kutawaliwa na siasa kumekuwa na propaganda za kimaneno pasipo na utekelezaji kwa vitendo, jambo linalomfanya mkulima kukata tamaa ya kulima zao la kahawa.




Meneja wa Bidhaa za Simu wa Tigo, Mkumbo Myonga (kushoto), na Meneja Uhusino wa kampuni ya kutengeneza simu ya Tecno, Eric Mkomoya, wakionyesha simu janja za kisasa aina ya Tecno Spark 3 na Spark Pro, baada ya kuzinduliwa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC awavuta wawekezaji viwandani

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI mkoani Kilimanjaro imewahakikishia wawekezaji wa viwanda kupata umeme kwa kipindi chote cha mwaka.

Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Annah Mghwira, aliyasema hayo alipozunguma na Nipase ofisini kwake, kueleza jinsi mkoa umejipanga kuwakaribisha na kuwavutia wawekezaji.

Alisema umeme unaozalishwa mkoani humo unatosheleza mahitaji ya viwanda na upo wa ziada, na kuwatoa hofu wawekezaji wanaoonyesha nia na waliopo.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa mkoa, ni vyema wawekezaji wakafika mkoani humo kujionea hali halisi kuliko kuhadithiwa kwa kuwa pamoja na umeme pia kuna miundombinu mizuri na imara.

Aidha, alilaani matukio ya uhujumu wa miundombinu ya umeme unaofanywa na watu wasioitakia mema nchi, na kwamba jamii inapaswa kuungana na serikali kuwataja watu hao ili hatua za kisheria zichukuliwe.

"Nasikitika kuona baadhi ya watu wanahujumu miundombinu kwa kuiba umeme, wezi wa mafuta ya 'transfoma' pamoja na nyaya za umeme, wanaofanya hivi waache mara moja, atakapokamatwa ni lazima ashitakiwe kwa kuhujumu uchumi na wananchi tunaomba ushirikiano katika kuwabaini," alisema Mghwira.

Kuhusu madeni ya Shirika la Ugavi wa Umeme (Tanesco), zikiwamo taasisi za umma na watu binafsi, Mghwira alisema kinachopaswa kutekelezwa ni utekelezaji wa agizo la Rais la kukata umeme.

Kwa upande wake, Meneja wa Tanesco Mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi Mahawa Mkaka, alisema umeme unaozalishwa mkoani humo ni megawati 135 na matumizi ni megawati 42.

Alisema kuwa changamoto ambayo shirika hilo inaipitia kwa sasa ni uwepo wa madeni makubwa kwa wateja wake yakiwamo taasisi za umma ambapo wamekuwa wakizikatia huduma.

Meneja huyo alisema kuwa changamoto nyingine ni ulinzi wa miundombinu ya shirika hilo ambapo baadhi ya watu wasio waaminifu wamekuwa wakiharibu miundombinu, wakiiba nyaya za umeme mafuta ya transfoma huku wengine wakiiba vyuma na wezi wa umeme.

## Mbinu za zamani za utunzaji mazingira zatakiwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI imekubali kurejea mbinu zilizotumiwa na wazee kuhifadhi mazingira ambazo hazikuleta athari ya mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza na wadau wa mazingira kwa niaba ya mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, alisema wazee wa zamani watasaidia katika kujua aina ya miti ya kuotesha ili kuhifadhi uoto wa asili.

"Wazee wanajua aina gani ya miti ambayo inahifadhi maji na inatakiwa kuoteshwa sehemu gani na wakati gani hivyo wataalam wakitumia wazee mkoa huu utarudisha hali yake ya zamani," alisema.

Alisema wakifanya utafiti wa kina kwa kutumia mawazo ya wazee watajifunza njia bora na rafiki ya kutunza mazingira ndani ya jamii, bila kuharibu mazingira na maisha yataenda kama ilivyokuwa hapo awali.

Warioba alisema nishati mbadala zimekuwa ni gharama kubwa kwa maisha na nchi wenye kipato cha chini hali ambayo inapeleka wananchi kuendelea kuharibu mazingira.

Mkurugenzi wa Shirika la Foresta Tanzania, Richard Mhina, alisema shirika linahifadhi mazingira mkoani Kilimanjaro kwa kutumia wananchi kulima kilimo kisichoharibu mazingira.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, shirika hilo lina vikundi 411 ndani ya mkoa huo vinavyohusika na utunzaji wa mazingira na kwamba kwa mwaka huu wanaotesha miti milioni 1.6.

Kwa upande wao baadhi ya wananchi, Nicolus Eusebus na Alfonce Mushi, walisema ikiwa wataalamu watarudi na kukaa na wazee kurejesha kijani mkoani humo.

"Tatizo la njaa au ukame halitakuwepo kwani mvua zitanyesha kwa wakati… vyanzo vyetu vya maji vitazidi kutiririsha maji na kuleta neema ya mboga mboga na matunda," alisema Nicolus.

# NI HUZUNI









# Dk. Reginald Mengi umetangulia, matendo yako yatabaki daima



HUZUNI 1942 - 2019

MAKONDA:

# Nitamuenzi Dk. Mengi kwa kuwalisha wenye ulemavu

• Alilia alivyomfikia hadi 'ndani ya kiatu'



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alipoteta jambo na Dk. Reginald Mengi, katika tukio lililowakutanisha. **PICHA: MAKTABA**

**Na Mwandishi Wetu**

KATI ya watu wanaotamani kuvaa viatu vya Marehemu Dk. Reginald Mengi, ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda.

Anatamani kumuenzi kwa kusaidia watu wasiojiweza na kula chakula na watu wenye ulemavu kila mwaka. Hiyo si bure. Ana mambo kadha wa kadha, kuanzia ya kikazi hadi binafsi, akiwa mbele yake kama baba mlezi.

Makonda anasema Dk. Mengi hakuwa tu tajiri aliyekuwa kwenye mkoa wake, bali ni mlezi wake, rafiki na aliyekuwa amesimama kuhakikisha anatimiza ndoto zake.

"Dk. Mengi alikuwa ni mtu anayesimama kuona ndoto yangu inatimia, aliniamini, alinipenda na kunifanya sehemu ya familia na kijana wake, kwa sababu alitamani kuniona nafanikisha kila hatua niliyokuwa napiga," anasema Makonda.

Anachojumuisha kwa sasa Makonda, kuwa Watanzania wamempoteza baba, rafiki, mwajiri ambaye alikuwa mkombozi wa watu wengi. Anaahidi kuwa kila mwaka atajitahidi kutoa chakula kwaajili ya watu wenye ulemavu kama ambavyo, alikuwa akifanya Dk. Mengi.

Mkuu wa Mkoa, anakiri sasa ana jukumu la kuhakikisha anawashika mkono watu wenye uhitaji, ili kuhakikisha anamuenzi Dk. Mengi kwa vitendo kwa moyo wake wa kupenda kusaidia wengine.

> "Sijawahi kutegemea kuona Mchaga anatoa pesa kwa walemavu, ni jambo gumu. Mchaga anampa pesa yatima ni jambo ambalo haliwezi kuelezeka.

"Dk. Mengi alipenda kuniona nafanikiwa kwenye kila hatua. Alipenda kunitia moyo na kunishauri katika yale ambayo nilikuwa nafanya, kwa kumuenzi nitahakikisha nakuwa Makonda ambaye Dk. Mengi alipenda kumuona," anasema.

Pia, anamtambua Dk. Mengi kwamba ni mwamba wa Kaskazini, sikio kwa waliokata tamaa na ambaye alikuwa tayari kuwa mfano kwa wanyonge, maskini na amepigana vita vizuri.

"Sijawahi kutegemea kuona Mchaga anatoa pesa kwa walemavu, ni jambo gumu. Mchaga anampa pesa yatima ni jambo ambalo haliwezi kuelezeka.

"Mchaga anakubali kumpa mali mtu hata asiyekuwa na ndoto, matumaini siyo jambo rahisi. Kwa hili, nazidi kusema siyo tu tumepoteza Mchaga bora katika Wachaga wote, bali tumepoteza Mtanzania aliyekuwa zaidi ya kabila lake," anasimulia Makonda.

Anasema, mwaka jana aliandaa tukio la chakula cha pamoja na viongozi wa dini na alitamani kuitimiza ndoto hiyo ambayo alikuwa nayo, lakini hakuwa na fedha.

"Watu wanadhani kila ninachofanya Makonda, serikali inanipa fedha. Hapa chakula na walemavu, ni nje ya ratiba za majukumu ya kazi za mkoa. Hivyo, nilipanga kufanya na kutafuta fedha kwa utashi wangu," anasema.

Makonda anafafanua, alilazimika kwenda kukopa fedha kwa rafiki wa mke wake Sh.milioni 50 na shilingi milioni 50, kwa mtu mwingine na kuandaa shughuli hiyo.

"Nilifanya shughuli nikiwa nina madeni ya kutosha tu, lakini niliamini nafanya kwa sababu kuna kusudi kubwa alililoweka Mungu mbele yetu, hasa kwa watu ambao ni watumishi wa Mungu," anasema.

Makonda anasema, baada ya kumaliza shughuli hiyo wakati wa mwaka mpya, Dk. Mengi alimpigia simu kwa ajili ya kumpa salamu za mwaka mpya na masuala mengine waliyozungumza.

Makonda anasema, alijaribu kumshirikisha suala hilo, ndipo alipoahidi kulipa deni lote la sh. milioni 147, kwa ajili ya shughuli ambayo ilishafanyika.

"Hakika nilimshukuru na yeye aliniambia nisijali, kwa sababu kazi niliyoifanya si chakula cha jioni, tu bali ni Karamu ya Bwana. Namkumbuka Dk. Mengi kama mtu aliyekuwa karibu katika kila jambo nililokuwa nafanya," anasema.

Pia, anasema Dk. Mengi alikuwa kipaza sauti cha watoto wa mitaani, yatima, wenye ulemavu na wasio na uwezo na alijitoa bila kujali kuwa atapata chochote kutoka kwao.

Alikuwa na mchango mkubwa katika sekta zote muhimu kama michezo, biashara, mazingira na kuajiri Watanzania wengi.

"Ukimuongelea Dk. Mengi kwenye uadilifu na kupiga vita rushwa utamkuta na amewapigania walemavu wengi nchini. Kwa ufupi, ni mzee wa kwanza wa kichaga niliyemfahamu ambaye alikuwa anatoa fedha zake kusaidia wengine bila kusubiri malipo.

"Mchanga ambaye hakuwa mchungu kutoa fedha yake na alifanya hivyo, bila ya kuwa na ndoto ya kugombea chochote bali kwa moyo wa upendo," anasimulia Makonda.

Anasema, licha ya kuwapo watu wengi wenye moyo wa kusaidia, lakini wengi wapo kwa ajili ya malengo binafsi ya kunufaika na misaada wanayotoa kama kugombea nafasi za uongozi.

"Kwa upendo ambao Dk. Mengi aliuonyesha kwa Watanzania wengi kama shujaa wetu na sikio la watu waliokata tamaa, tujitokeze kwa wingi kusherehekea maisha yake," anaeleza Makonda

Pia,anatamka Dk. Mengi alikuwa mtu ambaye hakukubali kukatishwa tamaa na mazingira. Licha ya kufikisha umri wa miaka 75, alikuwa na ndoto ya kuanzisha kiwanda kikubwa cha kuunganisha magari nchini na kuanzisha kiwanda cha dawa.

Kwake yeye binafsi, mbali na kumpatia msaada wa masomo, alikuwa mtu aliyemfanya kama baba yake na alimshauri na kumpongeza katika mazuri aliyokuwa akiyafanya. Lingine analolitaja ni wakati familia ya Makonda na Maria walipofanikiwa kumpata mtoto wao wa kwanza mwaka jana, alikuwa mfanyabiashara mkubwa wa kwanza kwenda nyumbani kwake kumpongeza.

"Ni mtu mwenye upendo wa hali ya juu na hata nilipopata mtoto, alikuwa mfanyabiashara mkubwa wa kwanza kuja kwangu na kunipa hongera na kufanya ibada ya maombi nyumbani kwangu na familia yangu. Ni kitu ambacho kilinifanya nimuone mwenye upendo wa hali ya juu," anasema.

Makonda anasema, Dk. Mengi alikuwa tajiri ambaye kwa kutumia nafasi yake, angeweza kumpatia zawadi aliyotaka kumpa bila kwenda nyumbani kwake. Lakini, alienda akawafanyia maombi na kuwapa ushauri.

"Nimempoteza baba mlezi, mshauri na kiongozi ambaye alikuwa na upendo wa hali ya juu kwa watu wote," anatamka Makonda.



HUZUNI 1942 - 2019

BETTY MKWASA:

# Kama sio Dk. Reginald Mengi, nisingefika mahali nilipo

- Anakumbuka ushauri, alivyomtibu mwanawe
- Mzee aliserebuka kufurahia Tuzo yake CNN

**Na Mary Geofrey**

MSHINDI wa Tuzo ya CNN na aliyewahi kuwa Mkuu wa Wilaya za Mvomero mkoani Morogoro na Bahi mkoani Dodoma, Betty Mkwasa, ameelezea namna Dk. Reginald Mengi alivyomuwezesha kushika nafasi hizo.

Alimfahamu Dk. Mengi, akiwa mtangazaji wa wakati huo Radio Tanzania (RTD) na baadaye kituo cha runinga cha Channel Ten.

Alimfahamu kama mmiliki wa kampuni za IPP na walikuwa wakionana katika utekelezaji wa majukumu.

Wakati huo Dk. Mengi alikuwa ameanza kutafuta watangazaji wa kituo cha runinga cha ITV na yeye alimtafuta kwa ajili ya kumpa kazi hiyo.

"Akaniambia anataka nikatangaze kwenye runinga yake ya ITV taarifa ya habari na nilimkubalia na kuanza kufanya kazi kuanzia Juni 30, 1995" anasema Betty.

Wakati akiwa ITV, Betty anasema aliitwa na Dk. Mengi na kumwambia amebaini kuna watu wengi hawafahamu kuhusu ugonjwa wa Ukimwi na nini hasa tiba ya ugonjwa huo.

Alimwambia kuwa anataka aanzishe kipindi cha kutangaza habari za Ukimwi, ili kutoa elimu kwa jamii kuhusu kujiepusha na kujikinga na ugonjwa huo.

"Nilimwambia kuwa naweza kufanya kazi hiyo kama ambavyo alinielekeza na akanitaka niandae jina la kipindi kwa ajili ya kuanza kazi hiyo," anasema.

Betty anafafanua kuwa aliendа kujadiliana na mwandishi wa habari ambaye sasa ni Mkurugenzi wa Vyombo vya Habari na Mawasiliano Internews, Wanceslaus Mushi, na kukiita kipindi hicho jina la 'Ukimwi ndio huu'.

"Tulimtajia Dk. Mengi lile jina la kipindi na aliahidi kuwa atakuwa akitoa fedha zake mfukoni kwa ajili ya kukiendesha na tulisafiri mikoani, kwa ajili ya kuandaa kipindi kwa fedha zake binafsi bila kutegemea za kampuni," anasema.

Wakati wanafanya kipindi kile, walipata watazamaji wengi na watu walikipenda, kwa sababu kilitoa elimu kwa jamii kuhusu Ukimwi.

Kupitia kipindi hicho, alifanikiwa kushinda tuzo ya mwandishi bora wa habari za afya iliyotolewa na Shirika la Habari la Kimataifa la Marekani (CNN).

Anasema tuzo hiyo aliipata mwaka 2003, akiwa ni mwandishi wa kwanza Tanzania na Afrika.

"Namshukuru Dk. Mengi, aliniwezesha kuwa mtangazaji bora wa habari za afya na kunifanya kupata tuzo iliyonipa heshima kubwa na kuliwakilisha taifa langu," anasema Betty.



Dk. Reginald Mengi (aliyekaa anaangalia kulia), alipobadilishana mawazo na wafanyakazi wa IPP, katika moja ya hafla aliyowaandalia. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

> **"Namshukuru Dk. Mengi, aliniwezesha kuwa mtangazaji bora wa habari za afya na kunifanya kupata tuzo iliyonipa heshima kubwa na kuliwakilisha taifa langu.**

Kupitia tuzo hiyo, alionekana kwa viongozi, akiwamo Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, aliyemteua kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro mwaka 2006.

Baadaye alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma kabla ya kuanza kufanya shughuli zake binafsi.

"Namshukuru sana Dk. Mengi kama si yeye kuniita na kuniambia nifanye kipindi kile, pia kunikaribisha kwenye kampuni yake ya IPP. Naamini nisingeonekana kwa Rais kushika nafasi nilizokuwa nimepewa," anasema Betty.

Anaeleza kuwa, Dk. Mengi alikuwa mwenye moyo wa kutoa sana, si mchoyo wa mali zake na alikuwa tayari kumsaidia mtu yeyote aliyemueleza shida yake.

Pia, anamkumbuka alikuwa mwalimu mzuri wa kufundisha watu kuhusu maisha, kujituma, kufanya juhudi katika kila jambo na kutokata tamaa.

"Hakika kila aliyekutana na Dk. Mengi na kueleza shida zake alisaidiwa. Wale ambao wanaweza kusema walikosa msaada wa Dk. Mengi ni kwa sababu tu hawakuweza kumfikia, lakini ilikuwa kama ukibahatika kumuona ni lazima akusaidie," anasema.



Betty Mkwasa.

Kwa upande wa maisha yake anaeleza, kuwa alimsihi kuendelea kufanya kazi kwa bidii hata kama ameolewa, kwa sababu familia inaendeshwa na watu wawili.

"Mimi alinisihi na kuniambia hata kama nimeolewa nifanye kazi nipate fedha za kuendesha maisha yangu, kwa sababu kuna leo na kesho kama mume hayupo watoto watanitegemea mimi, hivyo namheshimu kama mshauri wangu mzuri," anaeleza.

Anakumbuka kitu kikubwa alichomfanyia katika maisha yake, ni kumsaidia fedha za matibabu ya mtoto wake wa kwanza Raymond Mkwasa, ambaye wakati huo alikuwa akiugua ugonjwa wa moyo.

Mtoto wake huyo alitibiwa kwa fedha za Dk. Mengi hadi akafanikiwa kupona na sasa anaendelea na majukumu yake bila tatizo lolote.

"Raymond aliyekuwa na ugonjwa wa moyo amepona kabisa, ni mkubwa na anafanya kazi kama Factory Manager katika kampuni Sunshine,"anasema Betty.

Betty ambaye ni mke wa kocha wa zamani wa klabu za Yanga na Ruvu Shooting, Charles Mkwasa, anasema hawezi kumsahau Dk. Mengi kwa upendo wake na moyo wa kuwasaidia wengine.

Aliacha kazi ITV mwaka 2006 na mwezi mmoja baadaye aliteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro.

Bado kuna ushuhuda unaosimama, siku Betty alipopata tuzo ya CNN akifungua pazia barani Afrika, ilikuwa furaha ya aina yake, alipoonyesha dhahiri kufurahishwa na kurukaruka kwa bashasha ya kuwekwa rekodi hiyo.





UKAPUMZIKE MZEE MENGI...

# Hatua nne ngumu za msiba hizi hapa

**Na Beatrice Moses**

KUPOKEA taarifa za msiba, kupokea mwili, kuaga mwili, kushuhudia ukiingizwa kaburini na kuzikwa, ni hatua ambazo hutia simanzi.

Wengi wanajua, wengi wamekutana nayo na hakuna mgeni katika hilo, lakini uvumilivu wake ni mgumu mno. Takriban wote wanashindwa kuvumilia, wakilia na wengine kufikia kupoteza fahamu. Ni uchungu mkubwa.

Hatua hizo ndizo wamepitia ndugu, rafiki, wafanyakazi na jamaa wa Dk. Reginald Mengi, tangu walipopokea taarifa za kifo chake tarehe 2 mwezi huu hadi ulipowekwa katika nyumba ya milele, jana nyumbani kwao, Machame, Moshi.

Dk. Mengi alifia Dubai katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na mwili wake kuletwa nchini Mei 6 mwaka huu. Mamia ya wakazi wa Dar es Salaam, walijitokeza kuupokea bila ya kujali hali ya mvua iliyotawala mazingira siku hiyo.

Ni msiba uliowakamata wengi, walio karibu naye na wasio karibu naye. Wote kwa pamoja walitekwa na hisia moja ya kumpoteza mpendwa wao wa kipekee, ambaye aligusa moja kwa moja maisha yao,

Yameshuhudiwa mengi, Dar es Salaam, pia kwao Moshi na sehemu nyingi za nchi. Wapo waliodiriki walau kulishika gari, wengine walitandika nguo barabarani na kuna walioweka maua katika gari.

Wapo waliopigwa na butwaa na kila aina ya huzuni ilionyeshwa, wake kwa waume, huku kinamama walilia walau kupewa jeneza walibebe.

Ndani ya ofisi za taasisi alizomiliki, pia alizoshirikiana nazo kulizizima kwa kila namna ya huzuni, kauli kuu ni 'baba' na 'mwenyekiti' kaondoka.

**HUZUNI KUSHUSHWA**

Hayo yote yanakabiliwa vipi? Ni ukweli dhahiri kwamba hali ngumu inawakumba watu wengi wanaposikia taarifa za kifo cha kushtukiza, iwe ajali au ugonjwa. Mara wanapoambiwa, hutamani iwe ndoto, yaani isiwe taarifa ya kweli.

Kwa waliomuona Mzee Mengi alipoondoka akiwa anapiga hatua kwa miguu yake, walishindwa kujizuia kuporomosha machozi, baada ya kushuhudia sasa anarudi ndani ya jeneza.

Mtaalamu wa Saikolojia na Uhusiano wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Chris Mauki, katika chapisho lake, anazungumzia namna ya kukabiliana na nyakati anazozitaja: Huzuni; sononeko, maumivu ya moyo; na maombolezo, kama ambayo inawakabili jamii na wapenzi wa Dk. Mengi.



Marehemu Dk. Reginald Abraham Mengi

> **Sio mara zote neno hili 'kwaheri' linafurahiwa. Mara nyingine linaleta maumivu makubwa na huzuni moyoni.**

Dk .Mauki anasema, ni ukweli dhahiri kwamba japokuwa maisha yana nyakati nzuri na zenye kumbukumbu za kufurahisha, lakini zipo nyakati zinazowaletea watu huzuni, maombolezo na sononeko.

"Japokuwa nyakati hizi haziji mara kwa mara maishani mwetu na yamkini vipindi vyake ni vya muda mfupi, lakini kama hauna ujuzi wa nini cha kufanya nyakati hizi zinapokujia, basi fahamu kwamba zitakutesa sana," anaeleza.

Dk. Mauki anasema ni vigumu kuzuia nyakati hizo zisitokee, kwani kuwa mambo ambayo, ni lazima kutokea na hayakwepeki.

"Tulia, tuliza hisia zako, kaa chini na upumue kwa mafundo makubwa, pumua ndani na pumua nje taratibu ukiitoa hewa uliyoiingiza, fanya hivi kwa muda kidogo huku ukijiambia 'wacha tu itokee.' Jiambie...haina shida, hili litapita na kila kitu kitarudi kuwa sawa," anaeleza mtaaluma huyo kupitia Andiko Lake.

Anasema, kwa kufanya hivyo na kujaribu kila mara, mtu ataona inafanya kazi na anarudisha nguvu zake zilizopotezwa na maumivu ya kwanza.

"Unapokutana na machungu, maumivu au magumu mengine, jambo la kwanza kabla ya kuiangalia hofu na hatari iangalie fursa chanya mbele na kujiambia kwamba hakuna anayekufa au atakayepoteza uhai na kwamba maisha yanaweza kuendelea.

"Yapo mazingira ya bahati mbaya ambazo hutokea maishani, zipo nyakati tunapata hasara, zipo nyakati tunaumia, tunauguza, tunafiwa na kuwapoteza tuwapendao," anasema Dk. Mauki.

Anabainisha kuwapo nyakati ambazo kutokana na kuishi vizuri na marafiki, mnashibana kiasi kwamba ikitokea mauti, mnalazimika kuachana, labda wanasafiri au kuhama eneo fulani na kuambiana 'kwaheri.'

"Sio mara zote neno hili 'kwaheri' linafurahiwa. Mara nyingine linaleta maumivu makubwa na huzuni moyoni. Kinachotakiwa, ni kufahamu nini cha kufanya ili kupenya ukiwa salama," anaeleza Dk. Mauki.

Anaeleza, ipo shida pale wengine wanapopingana na ukweli huo au wanapokataa kuachilia yale yaliyokwishawatokea. Hapo wanaongeza ukubwa wa tatizo, badala ya kupunguza na maumivu yanazidi, badala ya kupunguza.

"Mara nyingine uponyaji unakuja kwa kukubaliana na ukweli na kuyaruhusu maumivu yaje kwa jinsi yanavyokuja, kujipanga kukabiliana na maumivu hayo hadi pale yanapokwisha ili yakikuacha basi yakuache jumla na sio kuendelea kukutesa muda wote unaoishi," anaeleza.

Anaongeza: "Mara nyingine usikwepe kuangukia kwenye huzuni, maana yaweza kufungua mlango mzuri kama ukiweza kukabiliana vema na huzuni ile. Hapa ninatamani kukusaidia nini cha kufanya ili ufungue mlango wa mema baada ya nyakati za huzuni na maumivu ya moyo."

**MAPENDEKEZO**

Mtaalamu huyo anasema pamoja na kutoa mbinu za kushinda sononeko na huzuni mara unapokabiliwa na jambo la kuumiza, anapendekeza mhusika 'kujiachilia' kwa kutoweka hisia nyingi kwenye hicho alichokiacha au kukipoteza (uliyempoteza).

"Tunajua kabisa kwamba huyu mtu aameshaondoka na hatorudi tena au hii hasara ni dhahiri na hakuna cha kufanya, ndiyo imeshatokea.

"Ila nafsi zetu zinashikilia hisia za kitu kile na kutotaka kuziachia na hili huongeza maumivu sana kwetu na maumivu haya yanaweza kudumu kwa muda," anaeleza.

Anasema, pia mbinu nyingime ya kujikimu ni kuweka kipaumbele kwenye furaha binafsi iliyopo hata katika nyakati ngumu na zenye maumivu makubwa ya moyo. Vipo vitu ambavyo vinatoa furaha au walau tabasamu kidogo.

Anashauri, ni vyema kujiuliza na kuangalia mazingira mtu aliyonayo, nini huwa kinampa furaha au kumfanya walau ajisikie vizuri anapokuwa katika magumu.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, kila mtu atakapoweza kuweka akili yake kipaumbele kwenye hivyo vya kumpatia furaha, ataona jinsi ilivyo rahisi kuhama taratibu kutoka kwenye hisia chungu na zenye kukuumiza alizo nazo.

Hapo, ana angalizo kwamba mtu awe makini kuchagua vitu vya kukupa furaha, haipaswi kuchagua vitu hasi au vyenye madhara, kwani ni rahisi kutumbukia katika janga la tabia ngumu au kitaalamu 'addictions" mfano ulevi au uvutaji sigara, kutafuta kujifariji.

"Hapo utajiingiza kwenye tatizo kubwa na la muda mrefu kuliko lile janga la awali. Kuwa makini kwenye uchaguzi wako wa wapi na katika kipi uitafute furaha yako, anatahadharisha.

Anaeleza kuwa jambo lingine linaloweza kusaidia kuondoa sononeko au huzuni ni kuvuta fikra za tukio lililowahi kuleta furaha kwako.

Baada ya kuwaza kitu kinachoweza kukupa furaha katikati ya maumivu na masononeko ya moyo, sasa jaribu kuvuta fikra "recall" katika matukio yaliyotokea na kumsababishia furaha aliyoiwaza kwenye hatua ya pili na kuweka rekodi ya matukio hayo, atazidi kupata nguvu ndani yako ya kustahimili nyakati unazopitia.

Anabainisha, pia inatakiwa kuendelea kuyatafuta matukio hayo kwenye maisha yako hadi utakapolipata tukio lisilozuri ila lilijeuka chanzo cha furaha.

"Kumbuka hapa tunajifunza namna ya kujitafutia nguvu itakayotuwezesha kupenya kiushindi katikati ya maumivu na masononeko ya moyo," anaeleza.

Maoni hayo, anayo mwanasaikolojia Daniel Gilbert kwenye kitabu chake cha 'Stumbling on Happiness' anayesema, watu wanapopoteza mpendwa wao, iwe mtoto, mzazi, ndugu na jamaa wa karibu, hali huwa mbaya sana siku za mwanzoni.

Maumivu ya moyo huwa makubwa kama vile mawimbi makubwa ya bahari yavumayo na wengine inawachukua muda mrefu sana, lakini wanapokaa karibu, zipo aina za furaha huibuka baada ya maumivu kwisha.

Furaha hizi zinaweza kuletwa na imani iliyowabeba katika kipindi hicho, au aina ya marafiki waliosimama nao na vitu vingine.

Anapokuwa katikati ya mapito mazito au nyakati zinazofuata baada ya mapito hayo, anaweza kuwa kipofu na usione fursa zozote za furaha.

"Usimezwe kabisa na machungu ya moyo ukaacha kufungua macho kuzitambua furaha mpya zinazozaliwa kutoka kwenye mapito yako.

"Mara ukiweza kuzitambua zitunze na uzilee ili ziendeleee kukusababishai furaha kubwa zaidi na kukusahaulisha kirahisi yale mapito yako makali," anasema.

Anahitimisha kwa kuhoji: "Je, unajua katika misiba yetu, mara nyingine tunakutana na marafiki wapya wazuri wanaokuja kufanyika furaha kubwa sana maishani mwetu na kutuacha tukisema; kama sio ule msiba nisingekutana na wewe."

Wakati tukiomba Mungu Ailaze Roho ya Marehemu Mahali Pema Peponi' ni fursa ya kutafakari mazingira ya kuturejesha katika faraja, kupitia baadhi ya mitazamo, huku tukiamini Kazi ya Mungu Haina makosa." Amen.



Marehemu Dk. Reginald Mengi, akirekebishwa tai na rafiki yake, Balozi Juma Mwapachu, alipowasili katika uzinduzi wa kitabu chake cha 'I Can, I Must, I Will, katika Hoteli ya Serena, jijini Dar es Salaam Mwezi Julai mwaka jana. **PICHA: JOHN BADI**

# HAYUPO TENA DUNIANI

1. Masikitiko jamani, Mengi we katutoka,
Hayupo tena duniani, Machozi yanatumiminika,
Hakika hatukuamini, Mengi kwamba umefutika,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani**

2. Amefia jama Dubai, Tarehe mbili mwezi wa tano,
Elfu mbili kumi na tisa, Familia mtoto wa tano,
Hana tena we uhai, Kaondoka Jumatano.
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani**

3. Hataongea milele, Serengeti Boys lieni,
Katoa kipaumbele, Kuwaimarisha michezoni,
Mmesogea we mbele, Mazuri zingatieni,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani**

4. Jina ghafla kubadilika, Ameitwa Marehemu,
Shuja ametutoka, ila tu Mungu akurehemu,
Hatuna lenye mashaka, uliotuachia ni muhimu,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani**

5. Ulisaidia wengi sana, Walemavu, wajane yatima,
Na hujasema sina, Ulitoa misaada jama,
Nasema haya bayana, Hana lenye lawama,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani**

6. Uliboresha mazingira, Kilimo uvuvi ufugaji,
Ulikuwa ni mtu imara, Mola atakuvalisha taji,
Hekima nayo busara, wema wako kipaji,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani.**

7. Biashara na viwanda, ulivimudu barabara,
Wanyonge uliwapenda, uliwaremba wakang'ara,
Hakuna lenye kupinda, Shidazo kutokukera,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani.**

8. Na vyombo vya habari, Vipo hewani hadi asubuhi,
Ni kiongozi hodari, Kugombana hajawahi,
Shughuli zilikuwa shwari, Kweli kabisa wallahi,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani**

9. Shughuli zako ni nyingi, Hatuwezi zote kuzitaja,
Ametuachia msingi, Tuendeleze kwa pamoja,
Hakujikweza kama Mangi, Matendo we yana tija,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani**

10. Hakukata tamaa, kusaidia kipaumbele,
Ulikuwa hakika mwema, Tutakukumbuka milele,
Hakuna wa kumsema, Na msirushe mishale,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani.**

11. Sote watarajiwa Marehemu, Hatuna pa kukimbilia,
Uwe na bora Elimu, utaihama tu dunia,
Majivuno siyo muhimu, Upendo ni bora sikia,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani.**

12. Nyumba ya mwisho jeneza, blanketi lake udongo,
Kubakia nje kwenye giza, Ni kweli siyo uwongo,
Watanzania Mengi kutuliza, Nimeamua kutoa utungo,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani.**

13. Yewomi jama Yewomi, Yewomi lanye yewomi,
Tunalia yule na mimi, Inabidi kufunga ulimi,
Kila mtu na lake usemi, Msiyumbishe jamii,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani.**

14. Watanzania wote, Tujipange wapenzi,
Tusitemeane mate, Tuondoeni simanzi,
Tusimame kidete, Kumbukumbu kumuenzi,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani.**

15. Tuandae shuguhuli, Yenye ukumbusho kwake,
Hakujali jama mali, Katika maisha yake,
Juhudi zake mbalimbali, Kusaidia tuwajibike,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani.**

16. Tuombeane kifo chema, Mapungufu tuacheni,
Pasiwepo lenye lawama, Tuondoke kwa amani,
Duniani ni mapito jama, Majivuno tuondoeni,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani.**

17. Ni Tamati tamatia, Mungu ampokee mbinguni,
Nasi tuendelee pia, Upendo wake jamani,
Tuendelee kuwaombea, Na apumzike kwa amani,
**Mpendwa Wetu Mengi, Hayupo Tena Duniani.**

**A• P Kavishe (mke na mume),**
**Simu: (+255) 0754 595568.**



HUZUNI 1942 - 2019

# Mzee Mengi alikuwa zaidi ya M

Na Agnes Kabigi



Dk. Reginald Mengi, katika picha ya pamoja na watendaji waandamizi wa kampuni tanzu za IPP. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

NIKIWA mwandishi wa habari, nilibahatika kufanya kazi kwenye moja ya kampuni za Dk. Reginald Mengi, The Guardian Limited.

Katika kipindi chote cha miaka tisa nilichofanya kazi The Guardian, nakiri kwamba Mzee Mengi hakuwa mwajiri wa kawaida.Mengi, almaarufu kwenye kampuni zake kama Mwenyekiti, alikuwa mshauri, baba, rafiki au kaka kwa watu wengi kulingana na umri wao.

Kwangu mimi, Mengi alikuwa baba na mshauri. Nikiangalia maisha yangu leo, ninadiriki kusema kuwa kwa mapenzi ya Mungu, msingi mzuri alionijengea mama yangu, ushauri na msaada wa kifedha wa Mengi ndio ulionifikisha hapa.

Tofauti na waajiri wengi ambao wao hujali kazi zao tu, Mengi alitupenda waajiriwa wake. Alikuwa akitusaidia kwa hali na mali, akisema sisi ni watu wa familia moja. Alikuwa akitushauri kupendana, kuthaminiana na kujaliana.

Mzee Mengi hakuishia kusema hayo kwa maneno, tu la hasha, bali alituonyesha kivitendo, kwani mwenyewe alitupenda, alituthamini na kutujali.

Mwenyekiti alikuwa akitaka wafanyakazi wa vyombo vyake vya habari wawe na maisha mazuri.

"Ninataka vyombo vya habari vya IPP, vilipe mishahara mizuri kuliko chombo kingine chochote nchini," alisema Mzee Mengi, alipokuwa anaanzisha vyombo hivyo na kweli ikawa.

Watu walijikuta wakilipwa hata mara tatu ya mishahara waliyokuwa wakilipwa kwenye vyombo walivyotoka walipoingia vya IPP. Maisha yakawa mazuri.

Mfano mwingine unaoonyesha jinsi ambavyo Mengi alivyokuwa akiwathamini waajiriwa wake, ni pale alipokuwa akisafiri nao kwenda kufanya kazi mkoani Kilimanjaro, ambako ndiko alikozaliwa.

Mwenyekiti alikuwa akisafiri na waandishi wa vyombo vya IPP kwa ndege na wakiwa Kilimanjaro, alikuwa na desturi ya kuwakaribisha nyumbani kwake 'Shanty Town' baada ya kazi, kwa ajili ya kutathmini siku hiyo, kupanga shughuli za siku inayofuatia, kujadiliana mambo kadha wa kadha na kula chakula cha jioni pamoja.

**ALIVYONIGUSA BINAFSI**

Sitakuwa nimemtendea haki Mwenyekiti, kama katika kutujali kwake wafanyakazi, sitakuwa nimeelezea pia jinsi alivyogusa maisha yangu kama Agnes na ndiyo maana ninasema kuwa, Mengi ni zaidi ya mwajiri.

Nakumbuka mwaka 1998, nikiwa mwajiriwa wa The Guardian limited, nilifiwa na mama yangu, Mary Kabigi. Katika msiba huo, Dk. Mengi akiwa amevaa nguo nyeusi (naangalia albamu ya picha za msiba wa marehemu mama hapa), aliungana na waombolezaji wengine kumlaza kwenye nyumba yake ya milele kwenye makaburi ya

> **"Nawapeni pia changamoto, kuwa siyo mafunzo ya ndani tu, jiendelezeni kwenye vyuo mbalimbali kama vile Chuo Kikuu Huria.**



Dk. Reginald Mengi, alipokaribishwa katika hafla ya wafanyakazi, katika ukumbi wa Mlimani City, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA.**

Chang'ombe, jijini Dar es Salaam.

Tukio lingine lililogusa maisha yangu binafsi: Bado nikiwa The Guardian kukawepo nyumba inauzwa. Nilitamani, lakini uwezo wa kuinunua sikuwa nayo, ingawa nilikuwa nimedhamiria kuimiliki.

Baada ya kutafakari sana nikaona, kama Mengi anawasaidia watu wengine, kwanini nisimwombe anisaidie na mimi kupata ile nyumba?

Nikatafuta miadi ya kumwona Mwenyekiti ofisini kwake, bahati nzuri nikaipata. Nilipofika ofisini kwake, kama kawaida yake akataka kusikia kazi inaendeleaje, naonaje mazingira ya kazi na nini kifanyike yaboreshwe.

Baada ya kutoa maoni yangu akataka kusikia kilichonipeleka kwake, nami bila ajizi nilitoa ombi langu. Mwenyekiti aliniuliza bei ya nyumba, nikamwambia.

Akasema kununua nyumba ni wazo zuri sana, akanipongeza. "Sasa, Agnes nikikupa fedha yote hutakuwa umenunua nyumba, nitakuwa nimekununulia nyumba. Ningependa nawe useme nimenunua nyumba.

"Hivyo, basi chukua kiasi hiki ambacho ni asilimia 40 ya bei yote. Hiyo asilimia 60 iliyobaki kapambane ukope hata kwenye kile chama chenu cha wafanyakazi cha kuweka na kukopa uinunue, deni ulipe pole pole," alisema.

Nilifurahi kupewa fedha hiyo, ingawa kiukweli binafsi nilitamani anipe zote. Niliondoka hapo nikipanga na kupangua mipango ya kupata ile asilimia 60.

Baada ya muda nikaifanikisha kwa mkopo, ambao niliulipa



HUZUNI 1942 - 2019



# Mwajiri





Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, alipowahutubia wafanyakazi wa kampuni yake katika hafla aliyowaandalia kwenye ukumbi wa Mlimani City, jijini Dar es Salaam, akitoa taarifa na somo la kampuni yao kuorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

polepole kama nilivyoshauriwa. Hakika ni kwa mchango na ushauri wake, mimi leo ni mmoja wa 'mama mijengo' wa Dar es Salaam.

**ALIELEKEZA TUKASOME**

Tofauti na waajiri wengi, Mengi alikuwa akitushauri kujiendeleza kielimu na kiuchumi. Nakumbuka siku moja alikuja ofisini ambako kulikuwa na mafunzo ya ndani yakiendeshwa akasema mafunzo ni muhimu.

"Nawapeni pia changamoto, kuwa siyo mafunzo ya ndani tu, jiendelezeni kwenye vyuo mbalimbali kama vile Chuo Kikuu Huria," alisema.

Wakati Mengi anahamasisha waajiriwa wake kusoma zaidi, baadhi ya waajiri wamekuwa wakiwakataza wafanyakazi kujiendeleza hata kwa muda wao baada ya muda kazi.

Nilimkumbuka Mengi, baada ya kuwa nimetoka The Guardian na kwenda kufanya kazi kwenye shirika lingine na kukutana na katazo kujiendeleza kielimu kwa kozi ndefu kama diploma na digrii.

Nikatamani kurudi The Guardian. Baada ya kujitafakari, nikaamua kusoma kisirisiri baada ya kazi na bahati mbaya wakati namalizia kozi yangu, mwajiri akagundua kuwa nasoma, hali iliyoleta mtafaruku kiasi cha kufikishana mahakamani. Nikasema laiti ningelikuwa The Guardian, haya yasingenipata na msaada wa ada pia ningepata.

Kwa upande wa maendeleo ya kiuchumi, Mengi alipenda sana kuhamasisha kuchukua hatua kwa kuelezea historia yake. Alikuwa akisema kuwa alitoka kwenye familia ya kawaida kabisa, lakini kutokana na njozi kubwa na juhudi alizokuwa akifanya huku akimtanguliza Mungu, amefika alipo.

Hivyo kama imewezekana kwake, ni wazi kuwa hata kwetu pia inawezekana kujikwamua kiuchumi. "Cha msingi tafuta changamoto zinazowakabili watu, kwani hizo ndizo fursa zenyewe.

Kuwa na njozi kubwa, lakini anza na kidogo ulicho nacho, usiache kuanza kushughulikia ndoto yako ukisubiri kupata mtaji mkubwa," ni moja ya kauli zake maridhawa.

Kufanya kazi The Guardian Limited, kumenipatia fursa ya kumfahamu Mengi. Kutokana na mambo niliyokuwa nikiyasikia tangu enzi nikisoma sekondari, kama mara kanunua picha ya kuchora kwenye mnada uliokuwa ukilenga kutunisha mfuko kwa ajili ya kitu kadhaa na kisha kutoichukua picha hiyo na kutaka iuzwe tena, ili ipatikane fedha zaidi, nilikuwa na picha tofauti kuhusu yeye. Alikuwa na fedha za 'kutapanya.'

Hata kuanza kwake kampeni ya Shujaa wa Kupambana na Umaskini kwa Vijana (SKUVI), ambayo alikuwa akiwataka vijana kujiunga kwenye vikundi kisha kuwapatia fedha kwa ajili kufanya kazi za ujasiriamali.

SKUVI ilishamiri kwa kasi kama moto nyikani hivyo kuzusha wasi wasi kwamba alikuwa na mpango wa kugombea Urais wa Tanzania. Niliona ni katika hali ile ile ya kuwa na fedha nyingi, kiasi cha kukosa cha kufanya nazo.

Lakini kwa kufanya kazi na Mzee Mengi, kumenionyesha kwamba hakuwa tajiri wa fedha na mali tu, bali alikuwa pia tajiri wa roho. Kutokana na roho yake kujaaa huruma na upendo, ndio maana alikuwa akichukua juhudi mbalimbali kuwasaidia wengine nao waendelee.

Ukaribu na upendo wa Mengi kwa wafanyakazi wake ndio umekuwa chanzo cha watu, pamoja na kuondoka kwenda kufanya kazi sehemu nyingine, kurudi tena kwenye kampuni za IPP.

Hata mimi nilipokuwa nikiondoka The Guardian, ilinichukua muda mrefu kufanya maamuzi, kwani nilikuwa naona kuwa kana kwamba sikuwa na shukrani, lakini ukweli ni kwamba nilikuwa naondoka kwa sababu tu nilikuwa nikitaka kubadilisha kazi.

Kwa kweli, nilipokea kwa mshtuko sana kupata habari za msiba huu, kwanza sikuamini. Nilitamani kuwa iwe ni moja ya ndoto zile za kutisha, iwe siyo kweli.

Lakini, kutokana na kutangazwa na ITV na kuendelea kumiminika kwa taarifa za msiba na mipango ya mazishi, nimeamini imetokea kweli. Narejea kauli kwamba 'Sote tu Mavumbi, na Mavumbini tutarejea." Hivyo, nabaki kumshukuru Mungu kwa maisha aliyompatia Mengi, hivyo kumwezesha kutugusa wengi kwa namna moja au nyingine.

Sina la kusema zaidi ya kumwombea Pumziko la Milele!

## Hatari msafara ulipofika 'njia panda ITV'...



Hii ndiyo hali ilivyokuwa siku hiyo.

**Na Peter Orwa**

NI jambo lililowaingia wengi katika hisia za moyoni. Mchakato wote wa mwili kushushwa kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na kuanza safari kuelekea katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo kuhifadhiwa, ulifuatiliwa kwa karibu sana na wafanyakazi wa kampuni za IPP.

Hao waligawanyika. Wapo waliopanda magari kwenda Uwanja wa Ndege kuungana na wananchi wengine waliofika huko na kwingine barabarani na kundi la pili, hasa baadhi katika vyombo vya habari, walilazimika kubaki kuendeleza majukumu yao ya kihabari.

Kuna cha kipekeee katika hilo. Utendaji wao siku hiyo dhahiri ulibadilika sana. Walionekana wanyonge muda wote, katika siku hiyo iliyokuwa ya mvua mfululizo.

Kasi ya kazi ilisuasua, kasi ya kukimbiza muda wa ukamilishaji kazi uliopangwa ililegalega. Hata anayesimamia kwa msukumo, alijikuta anaangukia huko huko, akibweteka kufuatilia msiba, anahamia katika mtandao kuina kinachoendelea juu ya mpendwa wetu.

Kamwe watumishi hawakuliacha tukio lipite hata kidogo, pamoja na kutopata fursa ya kwenda uwanja wa ndege. Walifuatilia kwa karibu kupitia nyenzo zote za habari. Hapo nina maana televisheni, kompyuta na simu.

Huzuni ziliwagusa sana, huku baadhi wakinong'onezana thamani ya Mwenyekiti wao ni zaidi ya hata ile waliomthaminisha wema wake kifikra kwa bei kubwa sana.

Hiyo ni kutokana na yale waioshuhudia kutoka barabara; vilio, kurusha maua, kusimamisha gari na bodaboda kuunda msururu kusindikiza.

Mvua nao ilichachamaaa kupitaa kiasi kila upande wa mji. Mara baada ya msafara waliokuwa wanaufuatilia kuonekana umekaribia maeneo ya Kinondoni, nako watumishi waliokuwepo katika ofisi za Mikocheni, walianza kutoka nje, mmoja baada ya mwingine, bila ya kuagana.

Ni wakati kila kitu kilisimama, kundi kubwa likishafika barabara kuu, kila mmoja akimshangaa mwenziwe kafika saa ngapi.

Muda mfupi kabla ya msafara huo kufika eneo la 'Njia Panda ITV' mvua kubwa ilifimuka, umati umefurika, watumishi wa kampuni tanzu za IPP 'wa kumwaga.'

Mvua ilikuwa inanyensha sana, lakini katika hadhira hiyo hayuko aliyeipa kipaumbele kuikimbia.Hapo ndipo nilishuhudia kuwehuka kwa watumishi.

Mmoja alijitambua kwamba 'hali si nzuri;' akaomba mwenzake amshikie kitambulisho na mengine, kwani ni hatari ya kuchanganyikiwa. Mwingine aliyechangayikiwa zaidi baada ya mwili huo kufika njia panda ya ITV na mwenzake alichukua hatua ya kunyang;anya miwani na mengine muhimu, huku yeye aking'ang'ania kuvamia gari hilo.

Lakini mwenzake alimzuia kwani aliona yuko katika hali ya hatari. Vijana wajasiriamali wa eneo hilo nao walikuwa wengi sana. Ghafla msafara huo ukiwa umezuia katika eneo hilo la Njia Panda ya ITV, kauli ya ukali kutoka kwa askari mlinzi katika msafara mweye cheo cha Inspekta, hakuna aliyekuwa tayari kumtii; "tunataka kumuona babu.'

Ghafla katika mazingira hayo ndani yamvua kubwa, lilitokea kundi kubwa la vijana wajasiriamali wa eneo la Mwenge walioshika matawi ya majani ya miti, wakiimba 'babu - babu - babu.'

Hao ni marafiki zake wakuu, ambao waliuteka msafara na kuedelea nao Lugalo. Kazini nako, kila kitu kilisimama.

Ni picha kama hiyo iliyochukua sura huko Machame alipowasili, kutoka kwa kinamama waliotaka kuubeba mwili, wapo waliolala barabarani na waendesha bodaboda nao wakimlilia babu yao.



# Mwanasheria NEMC: Unachokiona tunajivunia leo, kazi ya Dk. Mengi

• Alinifanya mwanawe, nilipougua alionyesha uzazi

**Na Mary Geofrey**

***"Katika hali ile nilishangaa kuona Dk. Mengi alivyohangaika na mimi kunitafutia tiba bora na kutuma madaktari na yeye mwenyewe akaja kuniona. Alisimamia tiba yangu kwa kiwango kikubwa, huku akinisihi kumjulisha kila hatua iliyokuwa ikiendelea..."***

UKIZUNGUMZIA Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 ya Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), huwezi kuacha kumtaja Dk. Reginald Mengi, aliyeshiriki kikamilifu katika kuiunda na kuanza kutumika rasmi mwaka 2005.

Huyo ni mwanamazingira, aliyewekwa katika nyumba yake ya milele, huku Machame mkoani Kilimanjaro, jana.

Wakati wa kuunda Sheria hiyo, Dk. Mengi alikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Nemc, nafasi aliyoishika kuanzia mwaka mwaka 1997 hadi mwaka 2006.

Mwanasheria wa NEMC, Heche Suguta, anasema baraza hilo litaendelea kumkumbuka na kumuenzi Dk. Mengi kwa mambo makubwa aliyofanya.

"Namzungumzia Dk. Mengi, ni mtu ambaye nilimfahamu kama mfanyabiashara na mwanamazingira na mtu mwenye ubinadamu wa pekee," anasema.

Namfahamu, pia ni mfanyabiashara na mtu aliyetokea familia maskini katika Kijiji cha Nkuu Machame na kupambana mpaka kuja kufikia hatua aliyokuwa nayo.

Suguta ambaye pia ni wakili wa kisheria, anasema sheria hiyo inaelezea namna ya kugawa majukumu ya usimamizi wa mazingira, kuanzia ngazi ya mtaa mpaka kitaifa.

Lengo lilikuwa ni kuhakikisha jamii kuanzia ngazi ya mtaa hadi taifa inatimiza wajibu wake katika kutunza mazingira.

Sheria hiyo iliweka uwiano mzuri wa kimajukumu hasa katika utunzaji wa mazingira na kuwa na majukumu mbalimbali kwa kila sekta nchini.

Kuwapo kwa sheria hiyo, ni jambo analosema litaendelea kumkumbuka Dk. Mengi, kwao Nemc, kutokana na juhudi zake mwaka 2005, ambayo kanuni mbalimbali, zikiwamo za tathmini ya athari za mazingira ziliandikwa na zinaendelea kutumika hadi sasa.

NEMC itaendelea kumkumbuka Dk. Mengi, kama kiongozi aliyesimamia kwa weledi mkubwa, mabadiliko katika sekta muhimu ya mazingira kwa ustawi wa watu.

Suguta anasema, katika kipindi hicho NEMC ilisikika hasa kwa sababu ya Dk. Mengi, aliyeshirikiana na utawala kufanya juhudi kubwa ya kuboresha misingi ya usimamizi wa mazingira nchini.



Dk. Reginald Mengi, alipowapa maua watoto 30 wagonjwa wa moyo, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, muda mfupi kabla ya kuondoka kwenda nchini India, kwa matibabu ya moyo. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

> **"Namzungumzia Dk. Mengi, ni mtu ambaye nilimfahamu kama mfanyabiashara na mwanamazingira na mtu mwenye ubinadamu wa pekee.**

Anaataja mambo makubwa yaliyofanyika NEMC, ni ubadilishaji wa sera na muundo wa NEMC na kuchochea utendaji kazi wa weledi katika nyanja zote za usimamizi wa mazingira nchini.

NEMC inamkumbuka Dk. Mengi, kama mwanamazingira hodari, mpiganaji asiyechoka katika kusimamia mazingira na kuhakikisha dunia ni mahali salama pa kuishi kwa wote na vizazi vijavyo.

Katika kipindi cha uongozi wake, NEMC ilibadilishwa kutoka taasisi ya ushauri na kupewa madaraka ya kisheria ya kutenda na kusimamia maagizo na sera mbalimbali za kiserikali katika sekta ya mazingira.

"Tunamshukuru nguli huyu na mwanamazingira huyu aliyejitoa sana muda wake na rasilimali zake, kwa ajili ya nchi yake," anasema Suguta.

Anasema, bodi yake ilipata uthubutu na kujiamini kikamilifu, kwa kuwa miongoni mwa watu 50 matajiri zaidi barani Afrika, lenye watu zaidi ya bilioni 1.4.



Mwanasheria wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Heche Suguta, aliyemchukulia Dk. Reginald Mengi, katika hadhi ya bosi na mzazi.

"Haikuwa kazi ndogo. Kwa hili, ninaamini ni kwa sababu ya juhudi, maarifa na kipawa cha kuona na kuanza yale ambayo wengi waliyaogopa au kudhani wameshindwa," anasema Sughuta.

**FUNZO ALILOMUACHIA**

Imani yake nyingine ni kwamba, Dk. Mengi ameacha funzo kwa vijana waamini kwamba, wanaweza kufanya chochote wanachotaka kufanya, bila ya kujali kuwa wametoka katika familia maskini.

Anasema kwamba vijana wana nafasi ya kuwa mtu yeyote anayetaka kuwa, bila ya kuzingatia kuwa wao ni ama maskini au mwenye ulemavu. Jambo kubwa ni kuwa na nia ya dhati kama ambavyo Dk. Mengi alisimamia alichokiamini.

Anamtaja Dk. Mengi katika maisha binafsi, alikuwa mwenye utu wa kipekee, katika kipindi cha miaka 10 alichomfahamu katika sura ya mzazi kwake, kwa maana alikuwa akimuita 'kijana wake.'

"Dk. Mengi naweza kusema ni mzazi wangu. Hata mara moja hajawahi kuniita jina langu, mara zote akiniita kijana wangu," anasema Suguta na kuongeza:

"Katika tukio ambalo siwezi kulisahau, ni mwaka 2016 alipougua ghafla ofisini na kupoteza fahamu. Dk. Mengi aliposikia taarifa hiyo alikuja hospitali kunijulia hali.

'Siku hiyo sitaisahau, nilikua nimefanya kazi mfululizo nikawa nimechoka sana jioni ya January 12, mwaka 2016, nikaanguka ofisini na kupoteza fahamu.

"Dk. Mengi aliambiwa na wasaidizi wake kuhusu hilo na yeye mwenyewe binafsi akanitafuta sana kwa simu asinipate, akamtuma daktari mmoja anifuate hospitali nilikokuwa nimelazwa.

"Katika hali ile nilishangaa kumuona Dk. Mengi alivyohangaika na mimi kunitafutia tiba bora na kutuma madaktari na yeye mwenyewe akaja kuniona. Alisimamia tiba yangu kwa kiwango kikubwa, huku akinisihi kumjulisha kila hatua iliyokuwa ikiendelea," anasema.

Suguta katika akiwa katika hali ya kutekwa kihisia na msiba huo, anaendelea kufafanua: "Huyo ni Mengi mpiganaji, bilionea aliyeniomba mimi nisiye kuwa bilionea nimjulishe hali yangu ya afya. Tangulia jamaa yangu, tangulia mwamba, tangulia mpiganaji na Simba uliyependa watu. Asante Mengi.

"Sitachoka kuendelea kumshukuru Mungu kwa ajili ya kunikutanisha na Dk. Mengi, ambaye alikuwa rafiki na baba kwangu. Namshukuru Mungu kwa ajili ya maisha ya Mengi.

"Huyu ni simba mpiganaji asiyekata tamaa, aliyejitolea mali na utajiri wake binafsi na kuugeuza kuwa wa watu wote wa nchi hii. Safari umeimaliza na taji tutakuvika."

Anahitimisha kwa kauli: "Dk. Mengi alikuwa na uwezo wa kuhama nchini na kwenda kuishi kokote, lakini aliendelea kuishi nchini na kutoa mchango mkubwa katika kusimamia mazingira na viwanda na maendeleo ya umma. Bravo Mengi."



# Songwe yatii agizo la JPM madini

**Na Nebart Msokwa,**
SONGWE

SERIKALI ya mkoani Songwe, imetii agizo la Rais John Magufuli la kufungua masoko ya madini kwa kufungua soko katika Halmashauri ya Wilaya ya Songwe ambayo ndiyo inayozalisha madini ya dhahabu katika Mkoa huo.

Mkoa huo ulifungua duka hilo juzi zikiwa ni siku 12 zimepita tangu Rais Magufuli alipotoa msisitizo wa wakuu wa mikoa kusimamia ufunguzi wa maduka hayo alipokuwa ziarani mkoani Mbeya.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa soko hilo, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigerdia Jenerali mstaafu Nikodemas Mwangela, alisema kuanzishwa kwa soko hilo kutasaidia Serikali kupata takwimu sahihi za uzalishaji na mauzo ya madini pamoja na ukusanyaji wa maduhuri ya Serikali.

Mwangela alisema mbali na Serikali kufaidika na kodi lakini soko hili litatumika kutatua tatizo la mitaji kwa wachimbaji wadogo kutokana na kuwapo kwa tarifa muhimu zitakazo hitajika na taasisi za kifedha kwa ajili ya kupata mikopo.

"Madini yanayopatikana katika Mkoa wetu ni dhahabu, shaba, makaa ya mawe, chokaa, fedha na madini ya ujenzi lakini tunalenga zaidi madini ya kimkakati ambayo mauzo yake yalikuwa hayaeleweki," alisema Mwangela.

Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Samuel Jelemiah, alisema baada ya ufunguzi wa soko hilo mchimbaji yeyote haruhusiwi kuuza madini nje soko na kwamba akikamatwa atachukuliwa hatua za kisheria kikiwamo kifungo.

Jelemiah alisema kuanzishwa kwa soko hilo kutaongeza maradufu mapato ya halmashauri hiyo ambayo walikuwa hawapati hapo awali kutokana na mfumo wa uuzaji wa madini hayo "Katika soko hili kutakuwa na sehemu ya ukaguzi na uthaminishaji madini pia kutakuwa na eneo la soko na miamala ambapo Mamlaka ya Mapato (TRA), Tume ya Madini, taasisi za kifedha na halmashauri watakwapo wawakilishi wao kwa ajili ya kuhakikisha wanachukua tarifa za mauzo."

Ofisa Madini wa Mkoa wa Songwe, Godson Kamidaya, alisema Wizara imefanya maandalizi ya kufanikisha utekelezaji wa jukumu la pamoja na kanuni ambazo zipo hatua za mwisho kupitiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kusainiwa kuanza kufanya kazi. Kamidaya alifafanua kuwa wameamua kufanya hivyo ili kuweka mazingira wezeshi kwa wachimbaji wadogo kushiriki kikamilifu masoko yanayoanzishwa.



Mfanyakazi wa kampuni ya usafi, akizoa mchanga kwenye Barabara ya Kawawa, eneo la Kigogo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Vijana CCM wamshukuru Rais miradi ya huduma

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JUMUIYA ya Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Idara ya vyuo na Vyuo Vikuu Mkoa wa Mbeya, umemshukuru Rais John Magufuli kwa kusaidia miradi mbalimbali ya kutolea huduma za kijamii wakati wa ziara yake mkoani humo ikiwamo elimu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mbeya jana, Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Frank Boaz, alisema wakati wa ziara hiyo vyuo na vyuo vikuu vilinufaika kwa miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa kumbi za mihadhara na mabweni ya wanafunzi.

Alisema katika ziara hiyo Rais Magufuli alizindua Jengo la Chuo Kikuu cha Mzumbe tawi la Mbeya ambalo limegharimu zaidi ya Sh. bilioni tatu na kuweka jiwe la msingi katika ujenzi wa maktaba ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (Must). "Paia alitoa zaidi ya Sh. bilioni saba kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maktaba ya Must na ujenzi wa mabweni ya kulala wanafunzi pamoja na miundombinu mingine, hivyo sisi kama vijana wa vyuo tunaamini wananchi hawajutii kumchagua mheshimiwa Magufuli," alisema Boza.

Vilevile, alisema Rais Magufuli aliweka jiwe la Msingi la ujenzi wa miundombinu mipya ya Chuo cha Walimu Mpunguso wilayani Rungwe ambao unajumuisha kumbi za mihadhara, nyumba za walimu na mabweni ya wanafunzi.

Alisema mbali na miundombinu ya elimu, pia Rais aliweka mazingira ya kuboresha sekta ya afya kwa kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya na Hospitali za Wilaya za Chunya na Rungwe.

Vilevile, alisema miradi mingine ambayo ni kwa ajili ya kuwasaidia wananchi ni pamoja na miundombinu ya barabara ambazo alizindua na zingine kuweka mawe ya msingi pamoja miradi ya maji ambayo inalenga kutatua changamoto za wananchi.

Alisisitiza kuwa Idara ya Vyuo vikuu ya CCM itaendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu mambo mbalimbali ambayo hayaeleweki ili kila Mtanzania ajue kinachofanywa na Serikali.

# Wanaume Mbeya wahusishwa ukatili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA kuwa wanaume wa Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa wanaoongoza kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kisaikolojia na wenza wao ikiwemo kunyimwa haki ya tendo la ndoa.

Hayo yalisemwa juzi na Mratibu wa Dawati la Jinsia Mkoa wa Mbeya, Mrakibu Msaidizi wa Polisi, Janeth Masangano, alipokuwa akizungumza na gazeti hili kuhusiana na vitendo vya ukatili wa kijinsia na watoto mkoani hapa.

Masangano alisema katika siku za hivi karibuni ofisi yake imekuwa ikipokea malalamiko ya unyanyasaji wa kijinsia kutoka kwa wanaume hatua ambayo imedhihirisha kuwa jamii imekuwa na uelewa kuhusu usawa wa kijinsia na harakati za kupingana na ukatili.

Alisema kuwa wanaume wengi wamekuwa wakifanyiwa vitendo ambavyo vimekuwa vikipelekea msongo wa mawazo na kwamba hali hiyo inawaathiri kisaikolojia kitendo ambacho ni miongoni mwa vitu vinavyotafsiriwa kuwa ni ukatili.

"Baadhi ya wanaume wananyimwa haki ya kupata tendo la ndoa, baadhi wanapigwa na wake zao lakini pia wapo wanaonyanyaswa kiuchumi, mwanamke anaweza kuwa ana kipato kikubwa kuliko mwanamume akaamua kutumia mwanya huo kumnyanyasa mwenza wake," alisema Masangano.

Katika hatua nyingine Masongano aliwataka wazazi kutopigana mbele ya watoto wao kwa madai kitendo hicho kinaathiri kisaikolojia watoto wao na wanapokuwa na tofauti wajaribu kutafuta suluhu bila ya kugombana.

Alisema migogoro ya ndoa haiwahusu watoto kwani inapaswa kumalizwa na wazazi wenyewe au kutafuta sehemu ambayo ni faragha na kumaliza tofauti zao bila watoto kujua kinachoendelea.

Akizungumzia ajira kwa watoto, alisema bado changamoto hiyo ipo katika Mkoa wa Mbeya hasa katika maeneo yanakofanyika shughuli za uchimbaji wa madini na kuwataka wazazi na walezi kutowaruhusu watoto kuajiriwa au kujiajiri wakati wakiwa na umri mdogo.





# Bahi yapewa 5 usimamizi ujenzi vituo huduma afya

**Na Paul Mabeja,** BAHI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amepongeza uongozi wa Wilaya ya Bahi kwa usimamizi mzuri wa ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya unaoendelea katika Halmashauri hiyo.

Akizungumza kati ziara yake ya kikazi wilayani humo, Jafo alionyesha kuridhishwa kwake wakati anapokea taarifa ya wilaya hiyo kuhusu maendeleo ya ujenzi wa miradi ya afya na kisha kutembelea ujenzi wa hospitali ya wilaya ambayo ipo katika hatua ya lenta.

"Hakika Bahi mmefanya kazi nzuri, mmejenga kwa kasi ya ajabu huku ubora ukizangatiwa katika majengo yote na bado mmesimamia matumizi mazuri ya fedha za mradi kwa kuwapa vibarua kazi hii ya ujenzi, "alisema na kuongeza:

"Niseme wazi kuwa Bahi mmenifurahisha kwa sababu mmeweza kutafsiri vizuri mfumo wa ujenzi pasipo kutumia mkandarasi yaani "Force Account" ambao unatumia fedha kidogo na mmetumia nguvukazi mliyonayo ya mgambo kufyatua matofali na vibarua ambao ni vijana kutoka hapa hapa Bahi kujenga majengo ya afya, hongereni sana kwa hili," alisema Jafo.

Sambamba na kuwapongeza viongozi hao, pia aliwataka kumaliza tofauti zilizopo kati ya Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo na Mbunge kwa kuwasisitiza kila mmojawao kutekeleza majukumu yake pasipo kuingiliana wala kukwamishana.

"Lengo letu sote ni kuleta maendeleo kwa wananchi kwa hiyo Mwenyekiti wa Halmashauri tekeleza majukumu yako pasipo kumuingilia Mbunge na Mbunge naye aendelee kutekeleza majukumu yake ya kibunge tena anafanya vizuri sana na miradi yote hii mnayopata ni jitihada zake bungeni kwa hiyo msimkwamishe, mpeni ushirikiano wa kutosha," alisema Jafo.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Bilinith Mahenge, alimueleza Waziri Jafo kuwa Bahi ni moja kati ya Wilaya za Dodoma zinazofanya vizuri katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alisema ujenzi wa vituo vitatu vya afya umeshakamilika na vitafunguliwa hivi karibuni wakati hospitali ya wilaya ikiwa katika hatua ya lenta.

"Pamoja na changamoto chache ambazo tunakutana nazo katika utekelezaji wa miradi hii kama vile ushiriki mdogo wa wananchi katika kuchangia nguvu kazi, kukosekana kwa Mhandishi wa Halmashauri, lakini tumekabiliana nazo kuhakikisha hazikwamishi ujenzi wa miradi yetu ya afya," alisema Munkunda.



Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, akizungumza na wakazi wa Kata ya Kikuyu katika mkutano wa hadhara, kwa ajili ya kutatua migogoro ya ardhi ya eneo hilo, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Bil. 27/- sasa kufunga umeme mkoa mzima

**Renatha Msungu,** BAHI

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 27, kwa ajili ya kufunga umeme katika wilaya za Mkoa wa Dodoma pamoja na vijiji vyake, lengo ni kusaidia wananchi kufanya shughuli za uzalishaji mali.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, wakati wa ziara yake ya kutembelea maeneo ambayo hayana umeme.

Dk. Kalemani alisema fedha hizo zimetolewa na Serikali kikiwamo kifaa cha umeme tayari (UMETA) 280 ambavyo vinatumika kufunga umeme kwa gharama ya Sh. 27,000.

Alisema kutokana na hilo ana uhakika hadi Julai mwaka huu vijiji takribani vyote vitakuwa na umeme.

Waziri Kalemani alifafanua zaidi kuwa wananchi waandae Sh. 27,000 ambazo ni malipo ya kuunganisha umeme kabla Tanesco haijaja kuwawashia umeme.

"Naomba mjiandae na hizo fedha, Tanesco wakija inahitajika kuwafungia tu," alisema Waziri Kalemani.

Alisema serikali ya awamu ya tano ni ya Viwanda, kwa hiyo viwanda bila umeme haiwezekani, ndio maana Wizara yake iko mstari wa mbele kukamilisha zoezi la uwashaji umeme.

Mbali na hilo aliwasisitiza Tanesco kuanzisha vituo vidogo katika vijiji ili kuepusha usumbufu kwa wananchi kufuata huduma.

Alisema kila kijiji ambacho kiko mbali wanapaswa kuanzisha vituo ili kuwasaidia wananchi wake katika harakati za kuunganisha umeme.

Alisema katika Wilaya ya Mpwapwa zoezi linakwenda vizuri ambapo vijiji 48 vimepatiwa huduma ya umeme, huku ikibaki katika vitongoji.

Naye Mbunge wa Bahi, Omary Badwel, alimshukuru Waziri Kalemani kutokana na vijiji vyake kupatiwa umeme.

Alisema anaamini hadi mwakani kila kijiji kitakuwa kimepatiwa huduma hiyo kutokana na zoezi hilo kutekelezwa kwa kasi.

Katika ziara hiyo alipita katika vijiji vya Chipanga, Chikori, huku Chimendel, Nkuragan vyote vilivyopo Kata ya Chikula navyo vitapitiwa kwa ajili ya ukaguzi.

Baduel aliwataka wakazi wa jimbo lake kuwa na subira kwa kuwa zoezi la ufungaji umeme linaendelea vizuri.

# 'Imani potofu unyonyaji damu ni za kupuuzwa'

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama cha Msalaba Mwekundu mkoa wa Dodoma, Dk. Mohamed Yuru, ameitaka jamii kuondokana na imani potofu iliyojengeka miongoni mwa Watanzania wao ni wanyonya damu za watu.

Dk. Yuru alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye maadhimisho ya siku ya Msalaba Mwekundu Duniani yaliyofanyika kimkoa jijini hapa.

Alisema kazi ya chama hicho ni kusaidia serikali na jamii pindi inapotokea majanga mbalimbali ya asili na kibinadamu na siyo dhana hiyo iliyojengeka ambayo imekuwa na sura mbaya miongoni mwa wananchi.

"Ni kweli hapo zamani watu waliaminishwa vibaya na kusema kuwa kuna wanyonya damu kwanza hakuna wanyonya damu pia huwezi kunyonya damu bila ridhaa yake na damu ikihitajika lazima itolewe kwa watalaamu hivyo tunaendelea kutoa elimu ili watu wajitokeze," alisema.

Alisema anawaomba wananchi kujitolea kwa moyo wa kibinadamu wao wenyewe kwa vitu na mali zao ili kuleta maana halisi ya kazi inayofanywa na chama hicho.

Kwa upande wake Hadija Mgoya kutoka kitengo cha mafunzo Chama cha Msalaba Mwekundu mkoa wa Dodoma, alisema taasisi hiyo inafanya kazi yake bila kujali dini, kabila ikiwemo katika kukabiliana na maafa kwa kutoa misaada mbalimbali.

"Red Cross inajishughulisha na majanga ya asili na kibinadamu kama vile tetemeko, kimbunga mafuriko sunami volkano na ukame,na kwa upande wa shughuli za kibinadamu ni vyombo vya usafiri,vya majini na nchi kavu mafuriko,vivuko,meli,magari, wakimbizi, moto na magonjwa,"alisema.

Hata hivyo alisema chama hicho pamoja na kutoa misaada, wanaendelea kutoa elimu kwa Watanzania ili na wao wawe sehemu ya kusaidia jamii pale inapotokea majanga.



## BARAZA LA WAWAKILISHI



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kushoto), akisalimiana na Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, baada ya kuwasilisha bajeti ya Ofisi yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 katika Baraza la Wawakilishi jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kituo cha kumbukumbu ya Karume chaanzishwa

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

KATIKA kuenzi mchango wa Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume, Serikali ya Zanzibar imeazisha kituo cha kumbukumbu yake kilichopo katika mnara wa kumbukumbu ya Mapinduzi Square eneo la Michezani Mjini Unguja.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu suali la Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Juma Nhnunga, alisema katika kituo hicho wananchi wanayo fursa wakati wowote ya kutembelea na kujifunza historia ya kiongozi huyo.

Katika swali aliloulizwa na mwakilishi huyo, alitaka kujua kwanini hakuna nyumba ya kumbukumbu na historia ya kiongozi huyo. Naibu waziri huyo alisema serikali kupitia sheria ya kuwaenzi viongozi wakuu wa kitaifa itaendelea kukusanya na kuzitunza kumbukumbu za kiongozi huyo ili ziweze kuwa ni kielelezo kizuri cha Mapinduzi pamoja na kutoa elimu kwa kizazi cha sasa na cha baadae.

Aidha, alisema kupitia redio ya serikali ya Zanzibar ina utaratibu wa kurusha hotuba za Mzee Karume alizozitoa wakati wa uhai wake.

Alieleza kuwa lengo la kurusha kipindi hicho ni kutoa elimu, kujenga uzalendo, ari na kuwakumbusha vijana juu ya muasisi huyo pamoja na historia ya nchi.

Akijibu suali la nyongeza la Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni, Rashid Makame Shamsi, aliyetaka baiskeli aliyokua akiendesha Mzee Karume iwekwe katika kituo cha kumbukumbu Kisonge badala ya kuwekwa ofisi kuu za CCM Kisiwandui, Mihayo alisema baiskeli hiyo itaendelea kubaki Ofisi kuu za CCM Kisiwandui kutokana na historia ya jengo hilo ambalo Mzee Karume alifikwa na mauti kwa kuuawa kwa risasi.

Aidha, Naibu Waziri huyo aliwataka wananchi wa Zanzibar na maeneo mengine kufika katika mnara wa kumbukumbu kisonge ili kujifunza na kujua historia ya Zanzibar.

"Nikiri kwamba uelewa wa wananchi kujua historia yao bado ni mdogo, hivyo niwaombe kukitumia kituo hicho," alisema Naibu Waziri huyo.

## Serikali sasa yawakumbuka walimu malipo

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema kuwa italipa malimbikizo ya fedha za nauli kwa walimu ambao hawajapewa fedha hizo.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Haji Omar Kheir, wakati akijibu suali la nyongeza lililoulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele, Ali Suleiman Ali.

Mwakilishi huyo katika swali lake hilo alitaka serikali kupitia Wizara ya Elimu na Tawala za Mikoa kukaa pamoja kuhakikisha walimu hao wanawapa nauli hiyo ili kufika kazini kwa wakati.

Waziri Kheir alisema kwa walimu wa shule za msingi suala la nauli linasimamiwa na wizara yake na walimu ambao hawajapatiwa nauli hiyo watapatiwa.

Akijibu suali la msingi lililoulizwa na Mwakilishi huyo wa Kijitoupele, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Muhamed Said, alisema kuwa tokea kuanza kazi kwa mfumo wa ugatuzi wenye dhamana ya malipo ya nauli kwa walimu wa shule za msingi ni Halmashauri, Manispaa, Mabaraza ya miji chini ya usimamizi wa ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Awali mwakilishi huyo wa Kijitoupele alisema kuna malalamiko ya kukosa nauli za usafiri kwa walimu wa Shule za msingi wilaya ya Kati kwa muda wa miezi minne na kusababisha usumbufu kwa walimu hao na nani mwenye dhamana ya kulipa nauli kwa walimu hao.

# Halmashauri zaagizwa ujenzi vyoo kwa wenye uhitaji maalum shuleni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

HALMASHAURI za Unguja na Pemba zimetakiwa kujenga vyoo kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za msingi ili kuwaondoshea usumbufu wanafunzi wenye mahitaji hayo.

Hayo yalisemwa na Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif Abeid, wakati akiuliza suali katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana. Mwakilishi pia alihoji kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inatambua uwapo wa changamoto ya ukosefu wa vyoo katika Shule ya Msingi Konde na hatua gani zimechukuliwa kukabiliana na tatizo hilo.

Akijibu suali la mwakilishi huyo, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Shamata Shaame Khamis, alisema moja ya mipango ya halmashauri hiyo ni kujenga vyoo kwa ajili ya wanafunzi wote wa shule za msingi na maandalizi wakiwamo wenye mahitaji maalum.

Alisema vyoo hivyo hujengwa kupitia fedha za halmashauri, fedha za maendeleo za mfuko wa Jimbo pamoja na fedha za wahisani kwa lengo la kupunguza uhaba wa matundu ya vyoo.

"Sambamba na hilo, serikali imejipanga pia kujenga vyoo vya watu wenye mahitaji maalum kila ambapo itaanzisha ujenzi wa shule mpya," alisema.

Alieleza kuwa hatua za awali ambazo Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imezichukua kukabiliana na tatizo hilo ni kuwataka wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule ya Konde A kuvitumia vyoo ambavyo vimefanyiwa ukarabati vilivyopo katika Shule ya Msingi Konde B.



HUZUNI 1942 - 2019

# MISA YA KUUAGA MWILI WA DK. MENGI – KKKT MOSHI MJINI



Jeneza la mwili wa Dk. Reginald Mengi, likiingizwa katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Moshi Mjini jana, kwa ajili ya misa na baadaye mazishi kufanyika



Mjane wa Marehemu, Jacqueline, akiwa na watoto wake, Ryan na Jayden, wakati wa misa.



Watoto wa marehemu, Regina na Abdiel, wakiwa na baba yao mdogo Benjamini Mengi (katikati), wakati wa misa.



Umati ukiwa katika foleni ya kuaga mwili wa Dk. Mengi,kanisani hapo.



Waombolezaji wakiwa katika foleni ya kuaga mwili wa Dk. Mengi kanisani hapo.

**PICHA ZOTE: SELEMANI MPOCHI**




Wananchi na waombolezaji wakiaga mwili wa Dk. Mengi baada ya misa.

## HABARI KITAIFA

# SMZ: Tutatoa taarifa ya uchunguzi mafuta, gesi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema kazi za utafiti wa nishati ya mafuta na gesi inaendelea na taarifa za matokeo ya uchunguzi huo itatangazwa kwa wananchi.

Hayo yalisemwa na Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, jana, wakati akiwasilisha makadirio, mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2019/2020 katika Baraza la Wawakilishi.

Alisema kazi inayofanyika sasa ni uchambuzi na usafishaji wa taarifa na kutafsiri mistari 14 yenye urefu wa kilomita 329.

Alizitaja kazi zilizofanywa ni pamoja na utafutaji wa mafuta kwa njia ya mitetemo ya maeneo ya nchi kavu na maeneo ya kina kifupi cha maji.

Alisema mikataba muhimu imetiwa saini ikiwemo wa mgawo wa nishati ya mafuta kati ya Zanzibar na kampuni ya Ragkas kutoka Rasilhema.

Alisema mkataba huo ni muhimu ambao ndiyo utakaotoa muelekeo wa mgawanyo wa rasilimali hiyo kama itapatikana.


Aidha, alisema Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati ya mafuta na Gesi ilisimamia kikamilifu kazi hiyo katika vitalu vya Pemba ambayo lilifanywa na kampuni ya BGP ya China.

"Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa ujumla kwamba kazi za utafutaji wa nishati ya mafuta na gesi unaendelea kwa hatua mbalimbali na matokeo ya utafiti huo walengwa watajulishwa," alisema.

Aidha, Balozi Iddi alisema jumla ya kanuni tatu muhimu katika utafiti wa nishati ya mafuta na gesi imefanywa ikiwamo uchimbaji wa mafuta, ada ya vibali pamoja na kanuni za uwasilishaji wa taarifa za kila siku za mafuta.

Alisema katika utafutaji wa mafuta na gesi, masuala ya utafiti mazingira yamepewa kipaumbele cha kwanza na kuona visiwa vya Unguja na Pemba vinakuwa salama.

"Tumezingatia kwa kiasi kikubwa suala la uhifadhi wa mazingira kwa ajili ya kuona Zanzibar inakuwa salama katika zoezi hilo,'" alisema.



Ofisa wa Benki ya DTB-Tanzania, Shahista Adam (kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 12 kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Sullivan Provost, Alex Nicholaus Sibuti, ikiwa ni ada ya watoto watano kutoka katika Makazi ya Taifa ya Watoto Kurasini, waliopata ufadhili wa benki hiyo, katika hafla iliyofanyika shuleni hapo, jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mkurugenzi wa shule ya Sullivan Provost, Rachel Mwalukasa (katikati) na (kushoto) ni Mama Mlezi wa Makazi hayo, Beatrice Mgumiro. **PICHA: DTB**

# Wakulima wasifia mbolea

**Na Mwandishi Wetu,** Tabora

Wakulima wa alizeti na tumbaku katika Wilaya ya Sikonge, mkoani Tabora, wamesifu juhudi za Kampuni ya Petrobena East Africa Limited, kwa kufikisha kwao mapema mbolea na pembejeo za kilimo na kusema kitendo hicho kimeinua kipato cha wakulima na mazao yameongezeka.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelewa na watendaji wa kampuni hiyo katika kata ya Kisanga wilayani Sikonge, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Msingi cha Kisanga, Selemani Msumeno, aliiishukuru kampuni ya Petrobena kwa jitihada zake za kuwasambazia wakulima mbolea ambazo zimeongeza uzalishaji katika eneo hilo.

Petrobena ni kampuni ya usambazaji mbolea na pembejeo za kilimo nchini ambayo pia ni wakala mkuu wa mbolea ya Yara.

Mkulima wa alizeti, Majaliwa Mussa, amepongeza jitihada hizi za Petrobena na kusema zimeboresha kilimo na kuinua kipato cha mkulima mmojammoja na Taifa kwa ujumla. "Hata hivyo tunazidi kuiomba kampuni hii ituletee mbolea mapema zaidi kwa msimu ujao kwa kuwa faida zake tumeziona," alisema Mussa.

Musa Ngazi alisema shamba lake limeboreka zaidi baada ya kuanza kutumia mbolea za Petrobena.

# Korti yapokea hati 11 za Gugai umiliki ardhi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imepokea hati 11 za umiliki wa ardhi wa Mhasibu Mkuu wa zamani wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Godfrey Gugai, kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana na Ilemela mkoani Mwanza kama kielelezo.

Gugai na wenzake watatu wanakabiliwa na mashtaka 43, kati ya hayo, makosa 19 ni ya kughushi, 23 ni utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zilizozidi kipato halali, ambalo linamkabili mhasibu huyo.

Hati hizo zilitolewa na shahidi wa 12, Ofisa Ardhi Mteule wa Nyamagana, Halima Nassoro hati sita na wa 13, Ofisa Mteule wa Ilemela, Grace Massawe (35) hati tano mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Awamu Mbagwa.

Nassoro alidai alifahamu uwepo wa hati za Gugai baada ya kupokea barua kutoka Takukuru wakitaka kujua mshtakiwa huyo kama anamiliki viwanja katika manispaa hiyo.

Alidai aliangalia katika kumbukumbu zake na kubaini kuna hati sita tofauti zenye majina ya umiliki wa mshtakiwa mahali tofauti katika manispaa hiyo.

Shahidi huyo aliomba mahakama kupokea hati hizo kama kielelezo cha upande wa Jamhuri.

Akimhoji shahidi wa 12, wakili wa utetezi Alex Mgongolwa kama ifiatavyo:

Wakili: shahidi umesema jalada lenye jina la mtu mwingine na Gugai alilipia kodi Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Je, ni mmiliki?

Shahidi: Ndiyo ni mmiliki, huwezi kulipia kodi kama si mmiliki wa ardhi.

Naye shahidi 13 Massawe alidai kuwa anaiomba mahakama kupokea hati tano za umiliki wa ardhi wa Gugai katika Manispaa ya Ilemela kama kielelezo cha Jamhuri.

Upande wa utetezi haukuwa na pingamizi dhidi ya hati hizo.

Kesi hiyo itaendelea kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri Mei 23 na 24, mwaka huu.

Mbali na Gugai, washtakiwa wengine katika kesi hiyo, ni George Makaranga, Leonard Aloys na Yasin Katera.

Gugai na mwenzake watatu wanakabiliwa na makosa 43, kati ya hayo, makosa 19 ni ya kughushi, 23 ni utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zilizozidi kipato halali, ambalo linamkabili Gugai.

Katika kesi ya msingi, wanakabiliwa na makosa 43, kati ya hayo 19 ni ya kughushi, 23 ni utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zilizozidi kipato halali, ambalo linamkabili Gugai.

Gugai anakabiliwa na kosa la kumiliki mali kinyume na kipato chake, ambapo alitenda kosa hilo kati ya January 2005 na Decembea 2015.

Inadaiwa akiwa Takukuru Dar es Salaam, Gugai alikuwa akimiliki mali za zaidi ya Sh. bilioni 3.6, ambazo hazilingani na kipato chake huku akishindwa kuzitolea maelezo.




# Jamhuri yaagizwa kasi ya upelelezi kigogo Takukuru

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imeuagiza upande wa Jamhuri kufanya jitihada za kukamilisha upelelezi wa kesi inayomkabili Mkurugenzi wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Kulthum Mansoor (57) ili ianze kusikilizwa.

Mansoor anakabiliwa mashtaka ya uhujumu uchumi ikiwamo manane ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Sh. bilioni 1.477. Jana upande wa Jamhuri ulidai mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Kelvin Mhina, kwamba upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Pendo Temu, ulidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kutajwa na kwamba upelelezi haujakamilika.

Utetezi ulidai kuwa kesi hiyo inapelelezwa na Takukuru wenyewe waharakishe isikilizwe ili kila upande upate haki yake.

Hakimu Mhina alisema jitihada zifanyike kukamilisha upelelezi huo kesi itatajwa Mei 23, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa kati ya Januari 2013 na Mei, 2018 ofisi za Takukuru zilizopo Upanga, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alighushi barua ya ofa ya Agosti 13, 2003 kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa, barua hiyo imetolewa na Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, huku akijua kuwa siyo kweli.

Shtaka la pili, ilidaiwa kati ya Januari 2012 na Mei, 2017 eneo la Upanga Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa akiwa Mkurugenzi wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Takukuru, kwa njia ya udanganyifu alijipatia Sh. milioni 5.2 kutoka kwa Alex Mavika.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alijipatia fedha hizo baada ya kudanganya kwamba angemuuzia kiwanja kijiji cha Ukuni Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani.

Katika shtaka la tatu, la nne, la tano, la sita na la saba tarehe na mahali pa tukio la pili, mshtakiwa alijipatia kwa njia ya udanganyifu Sh. milioni 27 kutoka kwa watu watano tofauti.

Wankyo alidai mshtakiwa alijipatia fedha kutoka kwa Wakati Katondo, Sh. milioni 3, Gogo James, Sh. milioni 5, Ekwabi Majungu Sh. milioni 7, John Amos Sh. milioni 7 na Rose Anatory Sh.milioni 5, wote wanadaiwa kuwa watumishi wa Takukuru.

Katika shtaka la nane, kati ya Januari, 2013 na Mei, 2018 eneo la Upanga, jijini, mshtakiwa alitakatisha Sh.1,477,243,000 wakati akijua kuwa fedha hizo ni zao la kosa tangulizi la kughushi.

Hata hivyo, kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo, mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Kijinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi (kulia), akifungua mafunzo kuhusu kuwapatia elimu wanafunzi wa shule za sekondari na msingi juu ya athari ya ukeketaji, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Ofisa Programu, Harakati na Ujenzi wa TGNP, Anna Sangaina na Afisa Programu Utafiti Zainabu Mmary. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ujenzi yaaswa kasoro taasisi zake

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WABUNGE wameitaka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kurekebisha kasoro zinazojitokeza kwenye taasisi mbalimbali zilizo chini yake.

Wakichangia makadirio ya bajeti ya wizara hiyo bungeni jijini Dodoma jana, wabunge hao walishauri baadhi ya ya miradi ya kimkakati inayotekelezwa na taasisi hizo ifanywe ya kitaifa badala ya kufanywa na wizara hiye pekee.

Mbunge wa Mlalo, Rashid Shangazi (CCM), alitolea mfano Shirika la Ndege (ATCL) kwamba limefanya vizuri nchini, hivyo lifanye hivyo hata nje ya nchi.

"Mashirika kama ATCL yasiachwe peke yake kwenye wizara bali kwa miradi kama hii iwe ya kitaifa na ya kimkakati. Tujifunze kutoka Rwanda Air na Turkish Air na wengine, ingawa tayari ndege nane zimeshanunuliwa, hakuna ndege hata moja ya mizigo," alisema.

Shangazi alisema Kanda ya Ziwa kuna viwanda 14 vya kuchakata minofu ya samaki, lakini inasafirishwa kwenda Nairobi na Kigali, Rwanda kabla ya kusafirishwa kwenda Ulaya.

"Maparachichi pia yanatoka nchini mpaka Kenya kabla ya kuuzwa China, hakuna anayejua kuwa maparachichi yanatokea Tanzania," Shangazi alisema.

Mbunge wa Sumve, Richard Ndasa (CCM), aliiomba ATCL iwe na ndege ya kutoka Dodoma kwenda Mwanza na kurudi.

Ndasa pia aliitaka serikali kukamilisha barabara ilizoziahidi kwa muda mrefu zikiwamo za jijini Mwanza na kuboresha huduma za bandari.

"Kuna kiongozi wa nchi jirani aliwahi kusema akipewa bandari ya Dar es Salaam, ataipa Tanzania bajeti yake," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, Salome Makamba (Chadema), alisema anamshangaa Waziri Kamwelwe kwa kusifia kampuni za mawasiliano za nje wakati TTCL imemshinda licha ya kutengewa fedha na Bunge.

"Katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri, nimemshangaa unashukuru mitandao ya kampuni za nje wakati tulikupa TTCl lakini lakini imeshindwa licha ya kukupa fedha.

"Tunafahamu Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) pale, kuna kazi kubwa sana imefanyika sana pale, nami naomba niwapongeze wafanyakazi, katika eneo lolote la kazi maslahi ya wafanyakazi kwanza.

"Lakini kinachotokea pale, Mkurugenzi wa Bandari anawafanyisha watu kazi mpaka saa saba, sita, saa saba usiku, sisi kama wabunge, maslahi yetu huwa yanakuja kwanza.

## Chanzo mtoto wa kike kunyimwa haki hiki

**Na Zuwena Shame,** KIBAHA

SHIRIKA la Plan International limesema umaskini ndiyo changamoto kubwa katika kuleta maendeleo na haki za mtoto wa kike, pamoja na kupata elimu nchini.

Limesema umaskini ndiyo kikwazo cha mtoto wa kike katika kusikilizwa, kulindwa na kuheshimika miongoni mwa jamii ya Watanzania.

Mkurugenzi wa shirika hilo ukanda wa Kusini mwa Afrika, charles Businge, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati akikabidhi rasmi miradi ya kijamii na kufunga uendeshaji wa miradi hiyo wilayani Kibaha Mkoa wa Pwani.

Businge alisema Plan International limekuwa likifanya shughuli mbalimbali za kijamii na kimaendeleo mkoani humo kwa tarkibani miaka 22, ikiwamo kuinua maisha ya watoto, wanawake na vijana.

"Katika miaka 22 Plan International ilipoanza kufanya miradi yake mkoani Pwani umaskini ndio umekuwa changamoto kubwa kwa wakazi wa mkoa na hivyo kufanya shughuli za kimaendeleo kuwa za kusua sua kwa wakazi wengi," alisema Businge.

Aliongeza kuwa kwa kuiona changamoto hiyo Shirika la Plan International kwa kushirikiana na serikali za mitaa na watekelezaji wa kujitoa katika wilaya ya Kibaha, waliwaelewesha wazazi juu ya umuhimu wa elimu hasa kwa mtoto wa kike.

Alisema Shirika la Plan International lilijenga vyumba vya madarasa 108, nyumba za walimu 18, vyoo vya kisasa na bora 287, ofisi za walimu 11 ili kuboresha elimu.

Alitaja baadhi ya miradi mingine ambayo imeweza kusaidia elimu wilayani humo ni pamoja na ujenzi wa shule za awali kwa watoto wanaojiandaa kujiunga na shule ya msingi, pia ujenzi wa vituo sita ya elimu ya awali wa watoto chini ya umri wa miaka mitano na ujenzi wa uwanja wa watoto katika shule za msingi Ruvu JKT na Msongola.

Alisema kwenye sekta ya afya Plan Intenational imeweza kujenga zahanati sita maeneo ya Magindu, Ruvu, Ngeta, Mwanabwito, Kikongo, Visiga na Mlanidizi na ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya ili kuwajengea uwezo na ufanisi wa kazi wilaya ya Kibaha.

Mwenyekiti wa jamii ya wamasai wa miradi ya elimu ya Plan International wilayani humo, Lenetica Kavuki, alisema shirika la Plan Intenational limeweza kuwasaidia wafugaji wilayani humo katika kupata elimu na haki ya mtoto wakike.

Kavuki alisema kuwa kabla ya shirika hilo kuingia wilayani humo watoto wa kike walikuwa wakifanyiwa ukatili wa kijinsia kwa kukeketwa ambapo takribani watoto 1,000 walikuwa wakikeketwa kwa mwaka, lakini tangu Shirika la Plan International lilipoanza mafunzo hakuna mtoto aliyekeketwa.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.
Baruapepe: ceo@kses.co.tz.

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311**

## CHETI KIMEPOTEA



115221302

**GRACE JOHN MUNTHALI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0316/0012 kilichotolewa na KIBASILA SEKONDARI mwaka 1981.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/MSI/RB/8676/2019.**

## PASSPORT IMEPOTEA



115220002

**EMILIANA ELIFALETI KWEKA** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba AB 767299 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 20/10/2015.

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi WMB/RB/2781/2018.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI Na.138 YA2018 BAINA YA**
**MALICK ALLY MASOUD ......................MUOMBAJI DHIDI YA**

1. YORAM DAUDI NGALI
2. TANZANIA POSTAL BANK
3. LADISLAUS RWASIGE
4. ELIAS CHARLES NYAGAWA ................WADAIWA

**KWA ELIAS CHARLES NYAGAWA POPOTE PALE ULIPO**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 13/06/2019

Angalizo: kama hukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri wa Baraza hili leo tarehe 9/5/2019

115221202

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

# JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# POCHETTINO: SIAMINI KILICHOTOKEA

**AMSTERDAM,** Uholanzi

KIKOSI cha Tottenham kimefanikiwa kutinga hatua ya fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kuwafunga Ajax mabao 3-2 katika mchezo wa nusu fainali na matokeo ya jumla kuwa magoli 3-3 na hivyo Spurs kufanikiwa kusonga mbele kutokana na mabao hayo ya ugenini.

Ushindi wa Spurs hautofautiani sana na ule wa Liverpool kwani hakukuwa na mtu yoyote aliyeamini kuwa timu hizi mbili kutoka England zingeweza kutinga hatua hiyo ya fainali hasa kutokana na matokeo yao mabovu waliyopata katika michezo yao ya kwanza ya michuano hiyo.

Akizungumza kwa furaha mbele ya vyombo vya habari mara baada ya ushindi huo Kocha Mkuu wa Tottenham, Mauricio Pochettino ameeleza hisia zake.

"Ni vigumu sana kufafanua hisia zangu za ndani kupitia maneno, ila nafikiri ulikuwa usiku muhimu sana katika maisha yangu." Amesema Pochettino

Pochettino ameongeza"Kwa namna mechi ilivyokwisha na kila kitu kilichotokea na vile tulivyopanga kucheza kwenye kipindi cha kwanza, nafikiri kila kitu kilikuwa cha ajabu."

"Kipindi cha pili tulipanga kufanya kidogo mabadiliko na kucheza kwa njia nyingine mbadala kila siku naamini kutokata tamaa. Kuna mambo mengi sana kwenye kichwa changu ila nataka kuwapongeza sana wachezaji wangu kwa kuumiliki mpira na kufanya kazi nzuri kwangu mimi nafikiri ni mashujaa, niliwaambia nafikiri miezi sita iliyopita narudia tena sentensi hii kuipeleka klabu fainali ya Ligi mabingwa ya Ulaya ni miujiza."

Alipoulizwa kama kuna kitu chochote ambacho amejifunza kutoka kwa wachezaji wake kutokana na mechi hiyo na Ajax, Pochettino amesema ni kweli kipo.

"Nimejifunza mengi, kila kipindi unajifunza kutoka kwa wachezaji wako, wao ni walimu bora zaidi, wanaumiliki mpira na sio sisi makocha ninawashukuru sana na nina bahati kwakuwa nina kundi la wachezaji ambao kwangu ni mashujaa."

Waandishi wa habari walipomuuliza Pochettino atawezaje kumfunga Liverpool kwenye mchezo huo wa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambao umewakutanisha Waingereza watupu alisema.

"Naomba mniruhusu ni pumzike kiasi, nitahitaji muda wa kulizungumzia hilo kuhusu Liverpool. Nahitaji kumpongeza, Jurgen Klopp na wachezaji wake wote na Liverpool nafikiri walifanya maajabu."

"Tulifurahi vya kutosha, kuangalia namna gani walivyowashinda Barcelona, wao ni mashujaa pia na naamini itakuwa fainali ya maajabu sana kwa timu mbili za Uingereza na hakika tutakwenda kufurahia hilo."

Hata hivyo kocha huyo wa Tottenham amezungumzia maisha yake ya baadae ndani ya timu hiyo mara baada ya kuulizwa na waandishi wa habari kama ana mpango wowote wa kuondoka kama atashinda taji hilo la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Ndiyo nitaondoka nikishinda na pengine hata nikipoteza pia." ameyasema maneno hayo huku akitabasamu.

# Mourinho awalinganisha Barcelona na watoto wadogo

**LONDON,** England

ALIYEKUWA Kocha wa Real Madrid, Jose Mourinho amesema kuwa anashindwa kuamini kwa matokeo waliyopata Barcelona dhidi Liverpool katika mchezo wa nusu fainali ya ligi ya mabingwa Ulaya usiku wa hapo juzi kwenye uwanja wa Anfield.

Kupitia mahojiano yake na chombo cha habari cha beINSPORT, Mourinho amewalinganisha Barcelona na watoto wa dogo wa umri chini ya miaka 14.

"Kama unaangalia bao lile kwa watoto wa chini ya umri wa miaka 14 au 15 ungeweza kusema, watoto wamelala, watoto hawapo sawa kiakili kucheza mpira, watoto wanahitaji kujifunza zaidi kuhusiana na msingi wa mechi." Mourinho ameiambia beIN SPORTS.

Mourinho ameongeza "Lakini tunazungumzia wachezaji bora kabisa ulimwenguni, bao ambalo hukuonyesha kwamba hakukuwa sawa kiakili."

"Katika kipindi cha mapumziko nilisema kama Liverpool watafunga bao la pili basi hali ya uwanja itabadilika, na hakika yakibadilika yatakuwa mazingira magumu sana kwenda nayo sawa."

"Lakini Barcelona wana baadhi ya wachezaji bora kabisa ulimwenguni, wenyewe asili yao ni kucheza daraja lile lile, asili yao kucheza dhidi ya Real Madrid, kuingia fainali, nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kila msimu kwao ni kitu cha kawaida."

"Ni kitu kigumu sana kwangu kukielezea, ni vigumu sana kuamini kwamba timu yangu imeshinda mabao 3-0 kwenye mchezo wa kwanza alafu nakuja kupoteza 4-0 mechi ya marudiano. Ningelipenda kuona Valverde akijaribu kuelezea lakini naamini itamwia ugumu kwake kuzungumzia."


Kwa matokeo hayo ya jumla ya mabao 4 – 3, Liverpool sasa itakutana na Tottenham katika fainali ya michuano hiyo baada ya juzi usiku kuwafunga Ajax mabao 3-2.

Mourinho amewahi kuikabili mara kadhaa Barca wakati akiwa kocha wa Madrid kati ya mwaka 2010 hadi 2013.



## HABARI MICHEZO

# Wenger aliwaonya Barcelona mapema



**PARIS,** Ufaransa

UNAAMBIWA hivi kama Barcelona wangesikiliza alichosema Arsene Wenger kuhusu Liverpool basi wasingeenda kukutana na aibu ile kubwa iliyowakuta huko Anfield.

Barca baada ya kuwachapa Liverpool mabao 3-0 katika mchezo wa kwanza huko Nou Camp waliamini wamemaliza kila kitu katika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya kwenda kukumbana na udhalilishaji mkubwa wa kupigwa 4-0 huko Anfield na kutupwa nje ya michuano hiyo.

Liverpool imetinga fainali kwa ushindi wa jumla ya mabao 4-3.

Lakini, kabla ya wababe hao kukutana katika mechi ile ya kwanza, kocha huyo wa zamani wa Arsenal, Wenger alisema kuhusu hatari ya Liverpool ni kwamba wanapokwenda kucheza kwenye Uwanja wake wa Anfield.

Barcelona wangemsikiliza kocha huyo mkongwe pengine wangeenda kwa heshima kubwa huko Anfield.

Akichambua kwenye televisheni ya BeIN Sports, Wenger alisema: “Liverpool ni bora pale kwenye udhaifu wa Barcelona. Wanapokuwa Ulaya wanafanya vizuri sana. Unajua wapi? Anfield.

“Huu ni uwanja wa moto zaidi Ulaya hasa kwenye mechi za marudiano. Hakika Anfield si mahali unapopaswa kwenda. Hali ya pale imekuwa ya kipee kabisa, zile kelele ni balaa.”

Hakika kile alichokisema Wenger huko ndicho kilichokwenda kutokea, Barcelona wakichapwa mabao 4-0 na hivyo kukomea hapo kwenye hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.




# SOLSKJAER MAMBO MAGUMU UNITED

**MANCHESTER,** England

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer, amewaweka kikao wachezaji wake na kisha kuwauliza kama wanajisikia vizuri kutokana na kufanya hovyo kwa timu yao ya Manchester United.

Kocha huyo aliwaita wachezaji wake watu wa ovyo kabisa baada ya kushindwa kuwafunga Huddersfield kwenye mechi ya Ligi Kuu England Jumapili iliyopita na hivyo timu hiyo kushindwa kutinga kwenye ‘Top Four’ na kupoteza nafasi ya kucheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Ole aliwauliza wachezaji wake kama wanajali japo hata chembe tu ya kila kinachotokea kwenye timu hiyo kwa sasa, huku akisema kuna wachezaji hapo wanapaswa kuona aibu kwa sababu hawastahili kuvaa jezi za United.

Halafu akawaambia kwa heshima ya mashabiki na klabu basi wahakikishe wanashinda mchezo wao wa mwisho wa ligi dhidi ya Cardiff utakaochezwa keshokutwa Jumapili.

Kocha Solskjaer alikuwa mwenye hasira baada ya wachezaji wake kushindwa kuifunga timu ambayo ilishashuka daraja tangu wiki iliyopita.

United watamaliza msimu wao kwa kucheza dhidi ya timu hiyo iliyoshuka daraja huku wakifahamu wazi msimu ujao watacheza Ligi ya Europa na si Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambayo wapinzani wao Liverpool wametinga fainali kwa msimu wa pili mfululizo.




# *Arsenal sasa kuuza nyota wake wote*

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal inataka kuanza upya na kitu cha kwanza ni kupiga bei mastaa wote mizigo kwenye kikosi chao wakianza na masupastaa, Mesut Ozil na Henrikh Mkhitaryan.

Ripoti za kutoka Emirates zinafichua kwamba kocha Unai Emery anajipanga kuwafungulia milango ya kutokea mastaa wasiopungua watano kwenye kikosi hicho huku Ozil na Mkhitaryan wakiongoza mchakato huo.

Kocha Emery anataka kutengeneza kikosi chake mwenyewe na hivyo kuachana na baadhi ya wachezaji ambao aliwarithi kutoka kwenye kikosi kilichokuwa chini ya kocha Mfaransa Arsene Wenger.

Kutokana na kikosi hicho kushindwa kumaliza katika nafasi nne za juu katika Ligi Kuu England msimu huu maarufu kama Top Four, jambo hilo linamfanya Emery kuamini kwamba hakuna namna zaidi ya kuachana tu na wachezaji ambao wamekuwa wakimbana tu asifanye mambo yake kwa uhuru kwenye timu hiyo.

Mpango wa Arsenal ni kuondoa wachezaji ambao inawalipa mishahara mikubwa, lakini michango yao ya ndani ya uwanja ni midogo sana.

Ozil anapokea mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki na Mkhitaryan anaweka kibindoni pauni 180,000 kwa wiki, hivyo kwa wiki hiyo ni sawa na pauni 530,000 watakuwa wameziokoa kama watawafungulia mlango wa kutokea mastaa hao kwa kuwauza.

Wachezaji wengine ambao ni rasmi wataondoka ni Danny Welbeck, Aaron Ramsey na kipa, Petr Cech huku Mohamed Elneny, Shkodran Mustafi na Carl Jenkinson ikiaminika kwamba watapigwa bei.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KANE: NITAIWAHI LIVER FAINALI UEFA

●●● Aweka wazi kwamba anatumai atakuwapo uwanjani kwenye mchezo wa fainali jijini Madrid…

**AMSTERDAM,** Uholanzi

STRAIKA Harry Kane amefunguka kuwa anatumai kuwa fiti wakati Tottenham itakapokutana na Liverpool kwenye mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuwa jukwaani akikitazama kikosi chao kikiichapa Ajax kwenye mechi ya nusu fainali.

**Kane, ambaye hajaichezea Spurs tangu Aprili 9, mwaka huu kutokana na kuwa majeruhi wa kifundo cha mguu, alikuwa katika Uwanja wa Johan-Cruyff Arena wakati Lucas Moura akikamilisha hat-trick yake walipotokea nyuma, na kukata tiketi ya kucheza fainali kwa bao la ugenini kufuatia matokeo ya jumla kuwa mabao 3-3.**

Straika huyo wa England, Kane alikimbia uwanjani baada ya kipenga cha mwisho akishangilia na wachezaji wenzake sambamba na kocha.

Na sasa ameweka wazi kwamba anatumai atakuwapo uwanjani kwenye mchezo wa fainali jijini Madrid hapo Juni Mosi, mwaka huu.

"Natumai [nitakuwa fiti kwa wakati]," Kane aliiambia BT Sport. "Matibabu yanakwenda vizuri hadi sasa. Nimeanza kukimbia moja kwa moja wiki hii."

Spurs ilionekana kuaga Ligi ya Mabingwa kutokana na hadi mapumziko Ajax kuwa mbele kwa mabao 2-0, hivyo kufanya jumla kuongoza kwa tofauti ya 3-0 katika mchezo huo uliopigwa huko Amsterdam, lakini hat-trick ya kipindi cha pili kupitia kwa Lucas iliifanya Spurs kutinga fainali kwa staili ya aina yake.

"Ni ajabu tu," alisema Kane. "Kipindi cha kwanza kilikatisha tamaa, hatukuanza vizuri na kuwaacha wacheze wao kisha wakafunga mabao mawili. Wakati wa mapumziko tulisema ni dakika 45 za kujitoa kwa kila kitu. Inaweza kuwa ya pili kwetu kwa mchezo wa mwisho wa msimu, hatukupaswa kuhofu kuhusu kucho-ka, jitoe tu kwa kila kitu.

"Wakati Lucas alipopata mawili kisha tulidhani tunakwenda kufunga, halafu Jan [Vertonghen] akagongesha mwamba na unadhani hilo ndiyo, haikuwa siku yetu, lakini Lucas alimalizia vizuri kwa kufunga mwishoni.

"Mimi ni shabiki kwanza na zaidi, ninajua ni kwa namna gani inamaanisha kwa klabu na kila mmoja anayehusika na klabu, wachezaji, kocha, uongozi, mwenyekiti, kila mmoja, na kama mchezaji ninatazama mchezo na kufikiri nini ningefanya ikiwa nilikuwa nje na vitu kama hivyo."

Akizungumza katika mjadala, Tim Sherwood alikisifu kikosi chake cha zamani, Tottenham kwa kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa.

"Hadi sasa ni nzuri, tutaona. Kama itaendelea kama ilivyofanya hivyo natumai kuwa, lakini bado kuna wiki chache kufika."

## ZISIKUPITE

### BARCA YAANZA NA COUTINHO

MSHAMBULIAJI Mbrazil, Philippe Coutinho (26), atakuwa mchezaji wa kwanza kuwajibika kutokana na kichapo walichopokea katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kutoka kwa Liverpool. Bodi ya klabu hiyo inajiandaa pia kukutana kufanya uamuzi juu ya hatima ya kocha, Ernesto Valverde. ***(ESPN)***

### HAZARD MAMBO MAGUMU

KIFUNGO cha kusajili wachezaji ambacho imekipata Chelsea, "imekuwa ni habari mbaya" kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Eden Hazard (28), ambaye alikuwa ameshaanza mchakato wa kuelekea Hispania kujiunga na Real Madrid. ***(AS)***

### HUDSON-ODOI HAKIJAELEWEKA

CHELSEA bado haijafanya mazungumzo na winga wa Timu ya Taifa ya England, Callum Hudson-Odoi na bado ikiwa haijafanya uamuzi wa kumuuza nyota huyo mwenye umri wa miaka 18 au kujiweka katika hatari ya kuondoka bure mwakani baada ya mkataba wake utakapokuwa unamalizika. ***(Mail)***

### ALLEGRI, JUVE KUMALIZANA

JUVENTUS na Kocha Massimiliano Allegri, wanajiandaa kuvunja mkataba baada ya kuitumikia kwa misimu mitano na kushinda mataji matano. Kocha na mchezaji wa zamani, Antonio Conte, anahusishwa na mipango ya kurejea klabuni hapo. ***(La Stampa - in Italian)***

### WAKALA AMKWAMISHA POGBA

KIUNGO wa Manchester United na Timu yaTaifa ya Ufaransa, Paul Pogba, hatorejea Juventus katika kipindi cha majira ya joto kwa sababu wakala wake, Mino Raiola, amefungiwa kufanya kazi zake nchini Italia hadi Agosti 9, mwaka huu. ***(Gazzetta dello Sport, via Express)***

### HERRERA RASMI PSG

KIUNGO wa Manchester United, Ander Herrera (29), anatarajia kujiunga na Paris St-Germain akiwa mchezaji huru katika majira ya joto na atakuwa analipwa mshahara wa pauni 160,000 kwa wiki na mabingwa hao wa Ufaransa. ***(Mirror)***

### BALE AIGANDA MADRID

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale, anataka kubakia Real Madrid lakini hataki kuona anapata upendeleo kutoka kwa Zidane. ***(Sky Sports)***

### MAKOMBE MAWILI EPL

KOMBE la mfano la ubingwa wa Ligi Kuu England, litapelekwa kwenye Uwanja wa Anfield wakati Liverpool itakapocheza na wakati lile halisi litakuwa kwenye Uwanja wa Amex Stadium kati ya vinara wa ligi hiyo Manchester City watakapoikabili Brighton. ***(Times)***

### OZIL, MKHITARYAN KUTEMWA

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery anataka kuwaacha wachezaji wakongwe watano katika kipindi cha majira ya joto akiwamo kiungo mchezeshaji Mjerumani Mesut Ozil na kiungo Henrikh Mkhitaryan. ***(Sun)***

### ORIGI KUULA LIVERPOOL

LIVERPOOL inajiandaa kumpa mkataba mpya straika wake Mbelgiji Divock Origi (24), ambaye juzi alifunga mabao mawili katika mechi ya marudiano ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambayo walipata ushindi wa 4-0 dhidi ya Barcelona. ***(Star)***

## HABARI MICHEZO

# Shonza kufunga michuano Lugalo

**Na Selemani Semunyu**

NAIBU Waziri katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika ufungaji mashindano ya wazi ya gofu ya TANAPA yatakayofanyika leo kwenye viwanja vya Lugalo jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Klabu ya gofu ya Lugalo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo, alisema kuwa mashindano hayo mwaka huu yamefanyika kwa ufanisi kwa wanafurahi kuona yanafungwa na kiongozi kutoka wizara husika.

"Tumekuwa na wageni rasmi kila mara, lakini kutoka katika wizara husika kupata kiongozi wa juu ni fursa itakayowawezesha kuufahamu mchezo na changamoto zake kwa ukaribu," alisema Luwongo.

Aliongeza kuwa mashindano hayo ni moja kati ya mashindano makubwa ya mchezo huo ambayo yako katika ratiba na yanasimamiwa na Chama cha Gofu Tanzania (TGU).

Kiongozi huyo alisema kuwa klabu yake imepewa dhamana ya kuendesha mashindano hayo kwa kushirikisha wachezaji kutoka klabu mbalimbali hapa nchini.

" Licha ya kuwa wazi, lakini klabu mwenyeji ni Lugalo na klabu nyingine zilizoleta wachezaji ni Gymkhana Dar es Salaam, Arusha Gymkhana, Moshi Gymkhana, TPC Moshi, Morogoro Gymkhana na Mufindi, pia kuna wachezaji wengine wamejitokeza kutoka nje ya nchi,"Brigedia Luwongo alisema.

Afisa Tawala wa klabu ya Lugalo, Kapteni Amanzi Mandengule, alisema kutokana na ukubwa wa mashindano hayo, wameyagawa katika makundi matatu ambayo ni ya wachezaji wa kulipwa, ridhaa na kwa wachezaji wasaidizi.

Naye Mwakilishi wa TANAPA, Dattomax Sellanyika, alisema hifadhi hiyo imeahidi kuendelea kudhamini mashindano hayo kwa lengo la kutoa fursa kwa wadau wa mchezo huu kupata taarifa na kutembelea hifadhi na vivutio kutokana na kuchezwa na wageni wengine kutoka nje ya Tanzania.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 31 | 26 | 3 | 2 | 69 | 13 | 81 |
| 2. Yanga | 34 | 25 | 5 | 4 | 54 | 24 | 80 |
| 3. Azam | 34 | 19 | 10 | 5 | 50 | 21 | 67 |
| 4. Mtibwa Sugar | 34 | 14 | 7 | 13 | 36 | 28 | 49 |
| 5. Lipuli | 34 | 12 | 12 | 10 | 30 | 31 | 48 |
| 6. Kinondoni MC | 34 | 10 | 15 | 9 | 35 | 25 | 45 |
| 7. Ndanda | 34 | 11 | 11 | 12 | 22 | 31 | 44 |
| 8. TZ Prisons | 35 | 10 | 13 | 12 | 27 | 28 | 43 |
| 9. Singida United | 34 | 11 | 10 | 13 | 26 | 33 | 43 |
| 10. Coastal Union | 34 | 9 | 14 | 11 | 30 | 41 | 41 |
| 11. Mbeya City | 33 | 11 | 7 | 15 | 32 | 36 | 40 |
| 12. Kagera Sugar | 34 | 9 | 13 | 12 | 30 | 37 | 40 |
| 13. JKT Tanzania | 35 | 9 | 13 | 13 | 22 | 32 | 40 |
| 14. Stand Utd | 34 | 11 | 7 | 16 | 31 | 42 | 40 |
| 15. Mbao | 34 | 10 | 10 | 14 | 20 | 33 | 40 |
| 16. Ruvu Shooting | 34 | 9 | 12 | 13 | 31 | 40 | 39 |
| 17. Alliance | 34 | 9 | 11 | 14 | 25 | 37 | 38 |
| 18. Biashara United | 33 | 9 | 10 | 14 | 25 | 31 | 37 |
| 19. Mwadui | 34 | 10 | 7 | 17 | 37 | 45 | 37 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# MGUNDA: COASTAL UNION TUMEVUNA TULICHOPANDA

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya timu yake kupata kichapo cha aibu cha mabao 8-1 kutoka kwa vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara Simba, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amesema kuwa "wamevuna walichokipanda".

**Akizungumza baada ya mechi hiyo iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Uhuru, Mgunda, alisema kuwa kichapo hicho kilitokana na wachezaji wake kurudia makosa ya aina moja mara kwa mara na wachezaji wa Simba ambao ni wazoefu walitumia nafasi hiyo kuwaadhibu.**

Mgunda alisema pia uchovu wa safari waliokuwa nao wachezaji wa timu yake ulichangia kusababisha matokeo hayo ambayo mara ya mwisho walifungwa idadi kubwa ya mabao kama hayo ilikuwa ni mwaka 2015 walipokutana na Yanga.

"Kikubwa ninachoweza kusema, huu ni mwezi wa Ramadhan, kwa tumevuna tulichokipanda, hata ukiniambia mara 100 nitakwambia hivyo...sina sababu ya kusema maneno mengine zaidi ya haya, mimi kama mwalimu na mkuu wa Coastal Union, mkuu wa benchi la ufundi la Coastal Union, kwa matokeo haya, tumeadhibiwa, tumevuna tulichokipanda," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema kuwa matokeo hayo hayakuwa mazuri kwake lakini bado kikosi chake kitaendelea kupambana na kujipanga ili kupata matokeo mazuri kwenye mechi zilizosalia ili waweze kubakia katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Napenda niseme ukweli, tumekuja muda ambao si mzuri," aliongeza Mgunda ambaye timu yake iliingia jijini Dar es Salaam ikitokea Tanga muda mchache kabla ya mchezo huo ikitumia usafiri wa basi aina ya Coaster.

Emmanuel Okwi na Meddie Kagere, kila mmoja alifunga hat-trick katika mchezo huo huku mengine yalipachikwa wavuni na Hassan Dilunga na Clatous Chama wakati bao pekee la Coastal Union katika mchezo huo lilifungwa na Raizin Hafidh.

Mshambuliaji Hafidh, alifunga pia bao pekee katika mechi ya kiporo iliyochezwa Aprili 17 mwaka huu kwenye Uwanja wa Mkwakwani wakati Simba ikipata ushindi wa magoli 2-1 katika mchezo huo.

Coastan Union yenye pointi 41 iko katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi hiyo, imebakiza mechi nne ili kumaliza msimu huu wa mwaka 2018/19.



Beki wa Ajax, Matthijs De Ligt (kushoto), akipambana na straika wa Spurs, Fernando Llorente, aliyeingia kuchukua nafasi ya Victor Wanyama, katika mechi ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi. Spurs ilishinda mabao 3-2 na kutinga fainali ya michuano hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# Kipanga kusajili wakali Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

ILI kukiimarisha kikosi chake kwa ajili ya kushiriki Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao, uongozi wa Kipanga umesema kuwa umejiandaa kusajili wachezaji wenye uzoefu na wenye uwezo wa juu ili wafanye vema katika ligi hiyo ya msimu wa 2019/ 2020.

Kipanga imepanda daraja katika msimu huu na itacheza Ligi Kuu Zanzibar kwa mara nyingine baada ya kushuka daraja msimu uliopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kipanga, Juma Shamuhuna, alisema kuwa hawatarajii kusajili wachezaji kutoka katika klabu zinazoshiriki ligi hiyo ya juu Zanzibar, bali wataangalia nyota wenye uwezo waliong'ara katika timu za chini ambazo anaamini zina nyota watakaowasaidia kufanya vema.

Shamuhuna alisema kuwa Kipanga itakuwa makini katika kuwasajili wachezaji wenye uwezo na wazoefu wa Ligi Kuu ili kuinusuru timu hiyo kushuka tena daraja.

"Tutakuwa makini katika usajili wa mara hii, na macho yetu tumeona tuyatupie zaidi katika klabu za madaraja ya chini kuanzia daraja la kwanza, la pili na hata daraja la kati, kuna wachezaji wazuri na wenye viwango, lengo letu ni kuona Kipanga inafanya vizuri katika Ligi Kuu ili kuondoa yale mazoea ya kucheza msimu mmoja ligi hiyo na halafu tunashuka," alisema Shamuhuna.

Hata hivyo hakuweka wazi hatima ya wachezaji watakaotemwa ambao walishiriki kuipandisha timu hiyo lakini hawawezi kuacha kusajili nyota wapya kwa sababu wanahitaji kuongeza nguvu kwenye kikosi hicho.

Mbali na Kipanga kutoka Kanda ya Unguja, timu nyingine itakayopanda daraja itatoka kwenye Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba ambayo imebakisha michezo nane.

# Michezo

Ijumaa Mei 10, 2019

Nipashe




Kane: Nitaiwahi Liver fainali Uefa HABARI UK.30



Golikipa wa Spurs, Hugo Lloris, akiruka bila mafanikio kudaka shuti lililopigwa na nyota wa Ajax, Hakim Ziyech na kuitunga wavuni moja kwa moja katika mechi ya marudiano ya hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi usiku. Spurs ilishinda mabao 3-2 na kusonga mbele. **PICHA: MAIL**

# Simba, Yanga vitani

## ●●● Ni katika mbio nyingine za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ambao...

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

VIGOGO wa soka Tanzania, Simba na Yanga wanatarajia kushuka katika viwanja tofauti nchini ili kuendelea na mbio za kuusaka ubingwa wa Ligi Kuu Bara msimu huu.

**Mabingwa na vinara wa ligi hiyo, Simba, wao watawakaribisha Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam wakati Biashara United yenyewe itawakaribisha Yanga katika mchezo mwingine wa ligi hiyo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Karume uliopo Musoma, Mara.**

Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, alisema jana kuwa timu yake inatarajia kuendelea na kasi ya kunyakua pointi tatu ingawa wanafahamu mechi ya leo itakuwa ngumu na yenye ushindani kama michezo mingine waliyocheza ya ligi hiyo.

Aussems alisema pia Kagera Sugar wataingia uwanjani wakijiamini zaidi, kutokana na kukumbuka ushindi walioupata mara ya mwisho walipokutana, lakini kwao hiyo haiwakatishi tamaa.

"Hii mi mechi mpya, ile ilishapita, kila mechi ina malengo na mbinu zake, hapa tutakuwa nyumbani na tuna nafasi ya kucheza tofauti na tulivyocheza Bukoba," alisema kocha huyo.

Mecky Maxime, Kocha wa Kagera Sugar, aliliambia gazeti hili kuwa bado kikosi chake hakiko mahali salama na wamejipanga kupambana ili kuendeleza "ubabe" dhidi ya mabingwa hao watetezi.

"Katika mechi ya Bukoba ilitukuta tuko mahali pabaya sana, kwa hiyo tutaendelea kutumia mbinu zile zile ili kufikia malengo yetu, ni hatari kusubiri kujua hatima yako siku ya mwisho," Maxime alisema.

Naye Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema kuwa kikosi cha timu yao kiko tayari kwa mchezo huo na wamekwenda Musoma kwa kazi moja ya kusaka ushindi.

"Tunashukuru tumepata mapokezi mazuri sana, tumesimamana sana Bunda, watu walikuwa na hamu sana na timu yao, haijaja huku kwa muda mrefu, tunaamini tutawapatia furaha ambayo wanaisubiri," alisema Saleh.

Alimtaja mchezaji atakayekosekana katika mchezo huo kuwa ni mshambuliaji, Ibrahim Ajibu, ambaye ni mgonjwa na alibakia Dar es Salaam mara baada ya timu kutoka Iringa.

**WALAKIWA BUNDA**

Mamia ya mashabiki, wapenzi na wanachama wa Yanga wa wilaya ya Bunda walijitokeza kwa wingi kuipokea timu yao juzi wakati ikipita kuelekea mjini Musoma kwa ajili ya kucheza mchezo wa ligi kuu Tanzania bara na timu ya Biashara United ya mkoani hapa.

Mashabiki hao waliipokea timu katika eneo la kijiji cha Serengeti kilichoko kwenye mpaka wa wilaya ya Busega mkoani Simiyu na Bunda, Mara huku wakiwa na msafara mkubwa wa magari pamoja na pikipiki.

"Bunda mmeitendea haki timu yetu maana kujitokeza kwa wingi katika kutupokea, hivyo ninawaomba siku ya mechi kati yetu na Biashara United pia mjitokeze kwa wingi, kwa ajili ya kutupa sapoti," alisema Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera.

Kocha huyo pia alipata fursa ya kufungua tawi la Yanga, lililoko mjini Bunda, na kutoa pongezi kwa hatua hiyo huku beki, Juma Abdul, akishukuru kwa niaba ya wachezaji wenzake kutokana na mapokezi hayo, kupokea kiasi cha Sh. milioni moja na chakula cha pamoja.

# Aussems atamani ubingwa mapema

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema kuwa malengo yake ni kuona wanafanikiwa kutetea taji la Ligi Kuu Tanzania Bara kabla ya kufika mechi za mwisho za msimu huu wa mwaka 2018/19.

Aussems alitoa kauli hiyo juzi baada ya timu yake kufanikiwa kukaa kileleni katika msimamo wa ligi ikiwa na pointi 81 na mechi tatu mkononi wakati nafasi ya pili inashikiliwa na Yanga wenye pointi 80 na wamecheza mechi 34.

Kocha huyo Mbelgiji alisema kuwa mafanikio ambayo timu yake inayapata yanatokana na uwezo wa wachezaji wake mmoja mmoja na kitimu kuwa wa juu tangu walipotolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Aliongeza kuwa bado kikosi chake kina kazi ya ziada ya kufanya vema kwa sababu ratiba ya mechi zao zilizobakia ziko kila baada ya siku moja au mbili.

"Bado kuna changamoto ili kutwaa ubingwa, tuna mechi tano ndani ya siku 12, sio jambo rahisi, tunatakiwa kufanya juhudi zaidi ili kufikia malengo yetu, leo (juzi) tumepata ushindi wa mabao 8-1 lakini baada ya siku moja tutakuwa tena hapa tunacheza," Aussems alisema.

Hata hivyo kocha huyo alisema kuwa hakuridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na timu yake katika kipindi cha kwanza ambacho walikwenda mapumziko wakiwa mbele kwa mabao 2-1.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >